# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Sita – Tarehe 21 Juni, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 48

**Upatikanaji wa Maji Vijijini**

**MHE. JUMA SAID OMAR** aliuliza:-

Kwa kuwa maji ni uhai na kwa kuwa upatikanaji wa maji Vijijini ni mgumu kiasi kwamba wananchi wanatumia maji ambayo si safi na salama kwa matumizi ya binadamu:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu utumiaji wa maji ambayo yanahatarisha afya na maisha ya wananchi?

(b) Je, Serikali inajiandaa vipi au ina mpango gani kuhakikisha kwamba maji safi na salama yanapatikana kwa uhakika Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Jimbo la Mtambwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa maji ambayo si safi na salama yanahatarisha afya na maisha ya wananchi. Ukosefu wa maji unawafanya wananchi kutafuta na kuchota maji yasiyokuwa salama. Matukio ya magonjwa yanayosababishwa na maji ambayo si salama, ni kielelezo kuwa bado wananchi wanatumia maji hayo. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine imekuwa ikihamasisha wananchi kuzingatia kanuni za afya kuhusu usafi wa mazingira na usafi

binafsi ikiwa ni pamoja na kuchemsha maji ya kunywa. Wananchi pia wamekuwa wakihimizwa kutunza vyanzo vya maji ili kuepusha kuchafuliwa au kukauka. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha huduma za afya ya jamii na mkazo utawekwa kwenye mipango ya pamoja inayojumuisha utoaji wa huduma za maji, usafi wa mazingira na elimu ya afya.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa upatikanaji wa maji safi na salama ni hitaji la msingi na haki ya kila mtu, Serikali kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002, imeandaa programu ya ujenzi wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira pamoja na utoaji wa elimu ya afya kwa wananchi.

Aidha, Serikali imebuni Programu ya Kitaifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini yenye lengo la kuwapatia maji safi asilimia 65 ya wananchi wa Vijijini ifikapo mwaka 2010. Msingi wa programu hii ni Sera ya Maji ambayo madhumuni yake yanazingatiwa kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwashirikisha wananchi katika kubuni, kupanga na kusimamia miradi ili iwe endelevu na inayomilikiwa na jamii kisheria;

(ii) Kuhakikisha kwamba wananchi wanachagua teknolojia inayowafaa kwa kuzingatia kiwango wanachoweza kumudu, na uwezo wa uendeshaji na matengenezo ya miradi yao;

(iii) Kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma ya maji Vijijini ili kuongeza kasi ya kupanua huduma hiyo Vijijini ambayo ni endelevu; na

(iv) Kuhamasisha na kuelimisha wananchi, hususan katika maeneo kame, kuhusu uvunaji wa maji ya mvua ambayo ndiyo chanzo muhimu cha maji cha kuaminika wakati wa kiangazi.

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, maji ni uhai na hasa yanapokuwa safi. Je, Serikali ina mikakati gani kwa kushirikiana na viwanda vinavyotengeneza maji kupunguza gharama za maji ya kunywa ya chupa ili angalau asilimia kubwa ya Watanzania waweze kumudu kununua maji hayo safi ya kunywa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, maji yanayotengenezwa na wazalishaji binafsi ni maji ambayo wananchi wenyewe wana uhuru wa kuweza kuyatumia au kuyaacha. Lakini hata hivyo, siyo rahisi kuwambia hao watengenezaji wa maji ya kunywa wapunguze bei hizo za maji kwa sababu maji hayo wanayatengeneza kwa gharama ambazo wakishaziandaa zote na kuzifanyia upembuzi wa bei ndiyo unakuta kwamba bei inakuwa kama hiyo. Kwa hiyo, mimi napenda kusisitiza kwamba wananchi wanywe maji na wahakikishe kwamba maji wanayotumia yachemshwe ndiyo njia salama zaidi. Ahsante.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kumuuliza Naibu Waziri wa Maji, kwamba kwa kuwa, Serikali ina mpango mzuri tu wa kutengeneza malambo kwa ajili ya mifugo na kuthamini mifugo zaidi kuliko wafugaji kupata maji salama. Je, ni lini Serikali itatengeneza mpango kabambe wa kutenga maji kwa mifugo na maji kwa ajili ya binadamu kwenye maeneo ya wafugaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, katika programu ya Maji na Usafi wa Mazingira kitu kimojawapo ambacho kinahamasishwa na kutolewa elimu ni kwamba miradi hii ni miradi ambayo inawekwa sehemu ya maji ya binadamu na pia kwa mifugo.

Lakini hata hivyo, nashauri Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati kijiji kinaandaa na kuchagua aina gani ya teknolojia ya mradi wanaohitaji ni hapo basi ndipo wanaweza wakaamua kuwe na sehemu ya kunyweshea ng'ombe na wanyama wengine na pia sehemu ya maji ya binadamu. Mfano, huo nimeuona katika Kijiji cha Chiseyu, Wilaya ya Mpwapwa ambapo katika miradi hiyo hiyo wamefanya vizuri sana. Wametenga sehemu ya maji ya binadamu na sehemu ya maji ambapo wananywesha ng'ombe kwa gharama ambayo wamekubaliana ng'ombe walipe shilingi ngapi?

Na. 49

**Kufufua Miradi ya Maji Vijijini**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika miaka ya 1960 na 1970 Serikali ilijenga miradi ya Maji Vijijini ambayo iliendeshwa na Halmashauri za Wilaya lakini mingi kati ya miradi hiyo imesimama kwa sababu mbalimbali na kwa kuwa, Serikali imekuwa na nia ya kuifufua miradi hiyo kama ilivyowekwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ambayo imelenga kupeleka Maji Vijijini kwa asilimia 65 ifikapo mwaka 2010:-

(a) Je, ni lini Serikali itaifanyia matengenezo na kuifufua Mradi wa Maji ya Nyamtukuza, Kakora, Nyarubele, Kitongo, Ikangala, Kharumwa, Izunya, Kayenze hadi Bukwimba?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuchimba visima virefu katika Vijiji vyote vya Jimbo la Nyang'hwale ambalo lina tatizo kubwa la ukame kila mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa katika miaka ya 1960 na 1970 Serikali ilijenga Miradi ya Maji Vijijini ambayo iliendeshwa na Serikali lakini mingi kati ya miradi hiyo imesimama kwa sababu mbalimbali, zikiwemo ukosefu wa fedha za kuifanyia matengenezo, ukarabati na upanuzi na ushirikishwaji mdogo wa watumiaji wa maji katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha huduma ya maji Vijijini, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, inatekeleza Mpango wa Maji na Usafi wa Mazingiara Vijijini ambao unajumuisha Wilaya zote nchini ikiwemo Wilaya ya Geita na Jimbo la Nyang'hwale. Hata hivyo, kwa vile Wilaya ya Geita tayari imeteua vijiji 10 na kuviingiza katika mpango vikiwemo vijiji vya Idetenya, Nyang'hwale, Busolwa an Lubando vya Jimbo la Nyang,hwale napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Geita ili Vijiji vya Nyamtukuza, Kakora, Nyarubele, Kitongo, Ikangala, Kharimwa, Izunya, Kayenze, na Bukwimba, viingizwe katika Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira kwa mwaka 2007/2008.

(b) Mpango wa Serikali ni kama nilivyoeleza hapo juu, ambao utekelezaji wake utategemea vyanzo vya maji, ukiwemo uchimbaji wa visima. Hata hivyo, ni vigumu kutabiri ni lini vijiji vyote vya Jimbo la Nyang,hwale vitapatiwa maji, kwa vile upatikanaji wa huduma ya maji unategemea upatikanaji wa fedha. Isipokuwa kuwa kama tulivyomshauri Mheshimiwa Mbunge ni kwamba ajitahidi kuviingiza katika programu na nina uhakika baada ya miaka mitano vijiji vyake vingi vitakuwa vimepata maji.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Moja, kwa kuwa tayari, nimeshawasiliana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita kuhusu Mradi wa Nyamtukuza hadi Bukwimba kupitia Kharumwa, Izunya na Nyarubele kuingiza kwenye Mpango huu. Je, Serikali sasa itatenga fedha za kutosha ili miradi yote hii 10 aliyosema ya Geita ikamilike kufuatana na uzito wa tatizo la maji Geita?

Pili, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufuatana na mimi na kuona miradi hiyo pamoja na ule wa Nyang'hwale na tatizo la maji la Geita na yeye aweze kunywa maji hayo ambayo ni ya visima vifupi ambayo si salama ambayo wananchi wa Geita wanakunywa, watu 800,000 na Wabunge wao, atakuwa tayari kunywa maji hayo?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema katika jibu la msingi ni sahihi kama ilivyoelezwa na Naibu Waziri tunachukua vijiji 10 kutoka kila Wilaya ya Tanzania kwa mwaka wa kwanza. Tumekwishapokea orodha ya vijiji 10 kutoka Wilaya Geita na hivyo ndivyo vitakavyoingizwa katika Mpango wa kwanza. Isipokuwa kama Halmashauri ya Wilaya ya Geita itataka kufanya mabadiliko, mfanye mapema kabla ya Mpango wenyewe haujaanza.

Kwa hiyo, kama kuna vijiji ambavyo vina umuhimu zaidi kuliko vile 10 ambavyo vimesomwa. Namshauri Mheshimiwa Mbunge aiambie Halmashauri ituandikie kwamba

inabadili kutoka vijiji 10 vya awali na kuingiza vijiji 10 vya sasa. Vinginevyo tunamshauri Mheshimiwa Mbunge avilete kwa ajili ya mpango huo huo kwa mwaka 2007/2008.

Kuhusu hali ya maji katika Wilaya ya Geita tunatambua kwamba Wilaya ya Geita kama zilivyo Wilaya nyingi nchini zina matatizo makubwa ya maji. Ndiyo maana katika majibu ya swali la msingi tumeshauri kwamba kabla ya Mpango huu haujawapatia wananchi maji, maji yanayopatikana yachemshwe ili kuhami afya za wananchi.

Kuhusu kukaribishwa katika Wilaya ya Geita namhakikishia Mheshimiwa James Musalika kwamba tutatembelea Wilaya ya Geita ili kushirikiana naye kuona jinsi tunavyoweza kuharakisha kule tunakoanzia na kuendelea kwa haraka zaidi.

Mwisho, ningependa kuwashauri Waheshimiwa Wabunge wote kushirikiana na Wizara yangu katika jambo hili, kwa sababu ni kubwa na ndiyo ukombozi pekee utakaowasaidia wananchi wa nchi yetu kupata maji. Kwa hiyo, kila mahali tukisimamia vizuri na utekelezaji ukaenda vizuri mwaka unaofuata tutaongeza vijiji. Lakini wale wanaotupatia fedha wakigundua mahali fulani utekelezaji uko nyuma watashindwa kutoa fedha zingine. Kwa hiyo, jambo la msingi ni kusimamia kuhakikisha kwamba huko tunakoanzia mambo yanaenda vizuri ili tuweze kupiga hatua zaidi. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni kweli kama swali la msingi lilivyo kwamba miaka 1960 na 1970 visima vingi vilisaidia sana kuleta neema ya maji katika maeneo mengi ya Wilaya ya Mpwapwa. Hali ilivyo sasa kwa kutegemea maji ya mtiririko na hali ya ukame na hali si nzuri kuanzia mwezi Septemba. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvifufua visima vilivyokuwepo ili viweze kuwa kama zamani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kwanza kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge katika Wilaya ambazo zinajitahidi na zina miradi mizuri inayotunza maji ni Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, napenda pia kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Serikali iko mbioni na inajitahidi katika kufanya kila njia kufufua miradi iliyokufa. Na pia hata hivyo, kila Halmashauri imekuwa ikileta maombi yake ambayo tunaita *immediately measure* au wakati mwingine tunaita *quick wills* kwa miradi ambayo Halmashauri inaona kwamba wanataka iboreshwe au aidha,ifufuliwe.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge afuate utaratibu kama huo kwa kushirikiana na Halmashauri yake ndipo masuala haya yote yatafika kwetu Wizarani. Ahsante sana.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ambayo yametolewa na Naibu Waziri na Waziri. Katika programu hiyo 1960 na 1970 ya maji Vijijini mmoja ya mradi maarufu kabisa katika Wilaya ya Kisarawe ni Mzenga, na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye

alikuwa Waziri wa Maji mara mbili alijibu akiahidi kwamba mradi huu utatekelezwa. Je, hivi sasa Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba Mradi wa Maji wa Mzenga unatekelezwa kutimiza ahadi ya Waziri Mkuu sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tu mwezi uliopita mimi nilikuwa ni mojawapo ambaye nimetembelea Jimbo la Kisarawe kuangalia huduma za miradi ya maji. Na ni kweli kwamba mradi wa Mzenga ni mradi mkubwa ambao ukifufuliwa, ni mradi ambao kwa kweli utasaidia kwa kiasi kikubwa kwa sehemu nyingi za Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba aje tujadiliane tuone sasa hiyo ahadi tutaweza kuitimiza namna gani kwa wakati muafaka ambapo fedha zitakapokuwa zimepatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu zaidi. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Maji kwa suala kubwa la maji.

Mheshimiwa Spika, lazima tukiri kwamba matatizo ya maji kwa kweli ni makubwa karibu sehemu kubwa sana nchini na miradi hiyo mingine ni mikubwa tuliahidi. Kwa mfano, jana Mheshimiwa Raynald Mrope, ule mradi wa Masasi pale ni kubwa sana wa siku nyingi uliahidiwa lakini haujatekelezwa na huu wa Mheshimiwa Athumani Janguo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na kuahidi kwamba Serikali inafanya Mpango Maalum wa kutafuta fedha za kutosha kushughulikiwa miradi hii mikubwa ya maji ambayo tuliahidi itekelezwe ili itekelezwe katika kipindi cha uongozi wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana. Lakini bado Waheshimiwa Wabunge wanaendelea kuuliza kuhusu maji. Mheshimiwa Kajege.

Na. 50

**Programu ya *National Rural Water Supply and Sanitation***

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, chini ya Programu ya *National Rural Water Supply and Sanitation* Vijijini kumi vya Wilaya ya Bunda vitapatiwa maji:-

(a) Je, ni vijiji vingapi vya Jimbo la Mwibara vitanufaika na Programu hii?

(b) Je, Programu hiyo itaanza kutekelezwa lini?

(c) Je, Programu hiyo inategemewa kuwa ya muda gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kajege, Mbunge wa Jimbo la Mwibara, kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake wa karibu kuhusu mwenendo wa Programu ya Kitaifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini itakayotekelezwa kwenye Wilaya zote za Tanzania Bara. Naamini ufuatiliaji wake utasaidia kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Programu hii katika Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli vijiji kumi vya Wilaya ya Bunda vitapatiwa maji kupitia Programu ya Taifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Vijiji hivyo ni Kinyambwiga, Kibara, Karukekere, Mumagunga, Salama kati, Nyamswa, Bunda Mjini, Nyang'aranga/Mugeta, Bulamba na Ligamba A. Katika Jimbo la Mwibara, ni vijiji vinne vitakavyonufaika na Programu hii navyo ni Bulamba, Kibara, Karukekere na Mumagunga.

(b) Mheshimiwa Spika, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini itatekelezwa na Halmashauri za Wilaya kwa kuzingatia Sera ya Maji ya Mwaka 2002. Programu hii itaanza kutekelezwa mwaka wa fedha wa 2006/2007.

(c) Mheshimiwa Spika, lengo la Programu ya Taifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ni kupunguza umaskini na kuboresha afya na maisha ya wananchi waishio Vijijini. Lengo mahsusi ni kuhakikisha kuwa asilimia 65 ya wananchi waishio Vijijini wanapata huduma ya maji iliyo endelevu ifikapo mwaka 2010 (ambalo ni lengo la MKUKUTA), asilimia isiyopungua 74 ifikapo 2015 (ambalo ni mojawapo ya malengo ya milenia) na asilimia 90 ifikapo 2025 (ambalo ni lengo la Dira za Maendeleo ya Taifa).

Programu hii itaendelea kutekelezwa kwa muda wa miaka 20, lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa wananchi wote waishio Vijijini wanapata maji safi na salama kwa umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye makazi yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama, kabla hujauliza swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, niwatoe wasiwasi hivi sasa kuna mtikisiko unasikika sikika hapa tulipo hili siyo tetemeko la ardhi, hapana. Nimeuliza sasa hivi Serikali wamenijibu kwamba barabara itakayowezesha wananchi wanaokuja Bungeni waweze

kupita kwenye upande huu sasa hivi inashindiliwa na mashine ambayo ni nzito kidogo. Kwa hiyo, tuvumilie hakuna tatizo kuhusu maisha yetu hapa. Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama, uliza swali la nyongeza.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa programu hii ya kuwapatiwa maji huwa ni Kiwilaya na kuna Wilaya zingine zina Halmashauri mbili. Je, ikiwa Wilaya haijashirikisha Halmashauri moja na ikashirikishwa Halmashauri moja tu, Wizara inasemaje kwa Halmashauri ile ambayo ilishirikishwa na ikashirikisha si vijiji inavyovikubali?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, hili sidhani kama ni tatizo kubwa sana sijui. Lakini utaratibu unaofuatwa ni Wilaya za Serikali. Wilaya za Serikali ndizo zinazoamua Vijiji 10. Kuna mahali pengine *Municipal* inakuwa ni Wilaya kamili na hata *municipal* za Mjini ambazo zimezungukwa na vijiji vinaruhusiwa vilevile kuchagua vijiji 10. Sasa kwa Wilaya ya Kibaha mimi nadhani Kibaha siyo *Municipal.* Kwa hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ni moja na ndiyo inayochagua. Sasa uchaguzi wa hivyo vijiji ulifanywa kabla ya Uchaguzi Mkuu uliopita. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge ana tatizo lolote pale ni vizuri ashauriane na ile Halmashauri ione kama kuna vijiji vingine ambavyo vina umuhimu zaidi viingizwe kabla ya *consultant* yaani washauri hawajaanza kazi yao ya kuvipitia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali linalofuata si la Wizara ya Kazi, Ajira, na Maendeleo ya Vijana kama ilivyotokea kwenye Orodha ya Shughuli za Leo ni la Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Lwanji aulize.

Na. 51

**Walemavu Kuteuliwa kuwa Viongozi**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni walemavu walimwomba Mheshimiwa Rais awafikirie kwa kuwateua kushika nyadhifa kadhaa za uongozi na uwakilishi:-

(a) Je, ni walemavu wangapi wa kuzaliwa, Watanzania ambao wana Shahada au Stashahada walioko nchini na nje ya nchi?

(b)Je, ni walemavu wangapi Mameneja, Wakurugenzi, Wawakilishi, Wabunge, Makatibu Wakuu na Mawaziri?

(c) Je, Serikali haioni kwamba, maombi hayo ya walemavu ya kutaka wafikiriwe katika nyadhifa za juu ni la msingi kwa kuwa, ni akili ndizo zinazopanga mipango ya maendeleo na sera mbalimbali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya sijajibu swali la Mheshimiwa Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, watu wenye ulemavu wapo katika makundi na aina mbalimbali. Wapo walemavu wa viungo, wasiona, viziwi, maalbino, viziwi – wasioona, walemavu wa akili na aina nyinginezo. Pamoja na aina hizi mbalimbali zipo pia tofauti miongoni mwao kwa mfano miongoni mwa walemavu wa viungo wapo wenye athari mwili wote, au mkono au mguu na kadhalika. Miongoni mwa viziwi wapo wasio na usikivu na wengine wana usikivu mdogo. Kadhalika kwa wasioona wapo wasioona kabisa na wenye uoni mdogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina idadi kamili ya watu wenye ulemavu wenye Shahada au Stashahada waliopo ndani na nje ya nchi. Serikali inafahamu hata hivyo kwamba kati ya mwaka 1978 na 2006 watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali 154 walipata Shahada kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Miongoni mwao 144 walipata Shahada ya Kwanza, 9 walipata Shahada ya Uzamili na mmoja Shahada ya juu ya Falsafa *(Ph.D.).* Mwenye Shahada ya Juu ya Falsafa ni Bwana T. Bagandashwa asiyeona ambaye sasa ni Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kadhalika Bi. Ellie Macha, asiyeona mwenye Shahahda ya Juu ya Falsafa *(Ph.D.)* kutoka Chuo Kikuu cha Manchester, Uingereza yuko nchini Kenya (Nairobi) akiwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa *African Blind Union* na kumfanya awe Mkuu wa Shughuli za Wasioona katika nchi zote 53 za Afrika. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haina idadi kamili ya watu wenye ulemavu ambao ni Mameneja, Wakurugenzi, Wawakilishi, Makatibu Wakuu au Mawaziri. Hata hivyo, tunafahamu kwamba katika Bunge lako Tukufu tunao Waheshimiwa Wabunge wawili wenye ulemavu wa viungo kutoka CCM ambao ni Mheshimiwa Margreth Mkanga wa Tanzania Bara na Mheshimiwa Zulekha kutoka Tanzania Zanzibar.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba wapo wenye ulemavu wengi wenye sifa na uwezo wa kushika nyadhifa mbalimbali katika Taasisi na Serikali. Na pale inapopatikana nafasi huwa wanaajiriwa. Kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu na mkakati wake wa utekelezaji na Kanuni za msingi kuhusu haki na usawa wa fursa kwa watu wenye ulemavu nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la kuwajumuisha watu wenye ulemavu katika masuala yanayowahusu ikiwa ni pamoja na kushiriki katika uongozi wa nchi ni la msingi.

Na. 52

**Miradi Mikubwa ya Machimbo Kuchangia Huduma za Jamii**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ipo miradi mikubwa ya machimbo ya madini, hasa ya dhahabu inayochangia huduma za jamii kama vile Afya, Elimu, Maji na kadhalika na kwa kuwa Kampuni kama *Kahama Mining Corporation* – Bulyanhulu, *Pangea Minerals* – Tulawaka, Geita *Gold Mining* – Geita *Resolute Tanzania Limited* – Lusu – Nzega, *Kiwira Coal Mine*- Kiwira na kadhalika, yamekuwa yakichangia huduma hizo kwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo:-

(a) Je, ni kitu gani kinachosababisha wananchi wa Kilwa Kusini nao wasifaidike na huduma kama hizo kutokana na mradi wa *Songa Gas?*

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mazungumzo na wamiliki wa mradi wa *Songa Gas* ili nao waanze kuchangia huduma hizo za jamii kwa wananchi wa Kilwa Kusini kama inavyofanyika katika maeneo mengine niliyotaja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kabla hujajibu leo ukumbi umekuwa giza kiasi kwamba nashindwa hata kuwatambua Waheshimiwa Wabunge sasa ningeomba wahusika mafundi watusaidie kwa sababu afadhili tuonane kuliko tuwe hatuonani. Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu**. (***Kicheko***)**

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la baada ya kutoa utangulizi huo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbasi Dewji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ya Songosongo ni mmoja wa miradi mingi iliyobuniwa Kitaifa kwa lengo la kuendeleza chanzo cha gesi ya Songosongo. Gesi asilia ya Songosongo ilianza kuzalishwa mwezi Julai, mwaka 2004. Mauzo ya gesi asilia kwa kipindi cha miezi ishirini ni shilingi 4,955,634/=, na fedha hizo ziliwasilishwa Hazina. Aidha, Jimbo la Kilwa Kusini ni miongoni mwa maeneo yanayopokea sehemu ya ruzuku kutoka katika mfuko mkuu wa Serikali kama sehemu ya fidia ya kutoza mrabaha na kodi zenye kero kwa wananchi.

Serikali katika mantiki ya kupunguza mzigo wa bei ya gesi kwa mtumiaji wa umeme, ilitoa tamko namba 246 linalohusu msamaha wa kodi, ushuru au malipo yoyote kwenye gesi asilia na miundombinu inayotumika kupitisha gesi katika Wilaya za Kilwa, Utete, Rufiji, Mkuranga, Temeke, Ilala na Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, licha ya kupata makusanyo ya gesi asilia, vilevile Serikali inatekeleza mradi wa umeme Vijijini *(Wayleave Village Electrification Scheme (WVES)* ambao ni sehemu ya mradi mkubwa unaolenga kuboresha maisha ya wakazi katika mkuza wa bomba la gesi asilia. Miradi inayotekelezwa ni:-

(i) Uchimbaji wa visima vya maji 44 katika vijiji vilivyoko katika eneo la mradi ambapo Kampuni ya *OCI* ya Dar es Salaam ndiyo inayofanya kazi hiyo na iko katika hatua za mwisho.

(ii) Uzalishaji wa umeme kutokana na gesi kwenye kituo kipya cha kuzalisha umeme wa *MW* 6 huko Somanga Funga, ujenzi wa mfumo wa kusafirisha umeme wa *KV* 33 na usambazaji wa umeme katika Wilaya za Kilwa na Rufiji ambapo hivi sasa ujenzi wa jingo la kuweka mitambo na nyumba za wafanyakazi unaendelea sambamba na maandalizi ya uagizaji wa mitambo (*generator*).

(iii) Huduma mbalimbali kama maji, umeme, upanuzi wa zahanati ujenzi wa gati na kituo cha Polisi kitajengwa Kisiwani Songo songo.

(iv) Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishafanya mazungumzo na Kampuni ya Songas mwaka 2001 na kukubaliana kuwa Kampuni ya Songas itachangia kuboresha huduma za jamii. Hivi karibuni kwa hiari yao, Songas imechangia maeneo kadhaa katika kuboresha huduma za jamii ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kugharamia upanuzi wa zahanati Kisiwani Songo Songo;

(ii) Utoaji wa huduma za umeme na maji safi kiasi cha mita za ujazo 30,000 kwa mwezi kwa wakazi wa Songo Songo;

(iii)Kuhamasisha na kusimamia uanzishaji wa *Credit Society* katika vijiji vilivyo katika maeneo ya mradi;

(iv) Kuchangia ada kwa kuwalipia wanafunzi wawili wanaofaulu katika shule ya msingi Songo songo.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili madogo. La kwanza Naibu Waziri alisema kwamba kuna Kata nyingine hazijaweza kusaidiwa kijamii bado na huu msaada anaosema yeye wa zahanati na mashule umefanyika pale Songosongo peke yake bado Kata nyingine hazijafaidika. Je, ana mpango gani wa kulisaidia Jimbo langu ili Kata nyingine zifadike kutoka na mradi wa Songosongo?

Swali la Pili, wenzetu wa migodi mikubwa ya dhahabu wanafaidika kwa kupata dola 200 kwa kila mwaka. Je, Halmashauri yangu itafaidikaje kutokana na gesi hiyo ambayo ni mkombozi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, sera ya madini ya mwaka 1997 inawahamasisha wawekezaji katika sekta za madini ikiwemo na gesi asilia kuchangia katika shughuli za jamii katika maeneo ambapo wanafanyia kazi Wizara yangu itaendelea kuhamsisha wawekezaji katika eneo la Songosongo kuhakikisha kwamba wanaendeleza shughuli za kijamii katika hizo kata ambazo hazijapata mpaka hivi sasa. Ningekuomba Mheshimiwa Mbunge tukutane baadaye ili tujue ni Kata zipi

ambazo hazijapata huo msaada ili tuweze kuendeleza mazungumzo na wamiliki wa Kampuni ya Songas kuhakikisha kwamba maendeleo ya jamii yanapatikana katika hizo Kata husika.

Kuhusu suala la dola 200,000 ambazo zinapatikana kutokana na migodi ya dhahabu, kwa hivi sasa Wizara yetu inaangalia mikataba ya madini yote na tungeomba kwamba Mheshimiwa Mbunge avute subira Kamati ambayo inatathimini mikataba ya madini imalize kazi yake ili iweze kuendelea na majadiliano na makampuni mbalimbali.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwanza kabisa naishukuru Serikali kwa kuweza kufanya makampuni ambayo yamewekeza katika machimbo kuweza kutoa kiasi cha dola 200,000 kila mwaka. Ningependa kujua kutoka kwa Naibu Waziri hizo dola 200,000 ni kama msaada ua ni mrabaha ambao wananchi wa maeneo hayo wanapaswa kupata na kama ni haki yao.Je, hicho kiasi kinatosha kulingana na kiasi ambacho wanavuna kutoka katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza hizi dola 200,000 ambazo zimepatikana sio mrabaha, hizo 200,000 ni kodi ambayo inalipwa kwenye Halmashauri husika katika maeneo ambayo migodi inafanya kazi na ningependa kuweka sawa kwamba hizo dola 200,000 zinatokana na mkataba baadhi ambayo iliyopo. Kuna makampuni mengine ambao watakuwa wanalipa zaidi kutoka na mkataba ambao watakuwa waliokuwa wameingia na kuhusu suala la kwamba hizo dola 200,000 zinakidhi, hizo 200,000 zinatokana na mikataba ambayo ilikuwepo kwa wakati huo kama nilivyosema katika sehemu yangu ya kwanza, kwamba hivi sasa Kamati ambayo inatathimini mikataba ya awali na sera ya madini kwa ujumla inafanya kazi yake, ripoti ya awali iko tayari tunataraji kwamba tutamaliza katika mwezi huu ujao. Ningeomba Mheshimiwa Mbunge avute subira ili Wizara yangu iendelee kushughulikia suala hilo. *(Makofi)*

Na. 53

**Wazungu Walioko Lugunga – Wilayani Bukombe**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika kijiji cha Nyakafulu, Kata ya Masumbwe na kijiji cha Wangimagi kata ya Lugunga wilayani Bukombe wapo wawekezaji – Wazungu ambao wamekaa kwa zaidi ya miaka 8 wakidai kuwa wanafanya utafiti wa Madini:-

(a) Je, Serikali inaweza kuliarifu Bunge kama inafahamu kuwepo kwa Wazungu hao katika maeneo hayo?

(b) Kama Serikali inatambua kuwepo kwa Wazungu hao, Je, imechukua hatua gani dhidi yao na pia kulieleza Bunge hatua waliyokwishafikia katika utafiti wao ili wananchi wa maeneo hayo waweze kuondokewa na wasiwasi na pia wategemee kufaidika kwa kuwepo kwao ikiwa watafanikiwa kufungua mgodi rasmi?

(c) Kama wameshindwa kugundua Madini katika maeneo hayo, si vema wakatoka ili maeneo hayo yatumiwe na wananchi kwa uchimbaji mdogomdogo ili wajikimu maisha yao kuliko kuendelea kusumbuliwa na utafiti ambao hauwasaidiii?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a), (b), na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inafahamu kuwepo kwa kampuni za kigeni zinazofanya utafutaji wa madini katika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, Kampuni hizi ni *Sukuma Mines Limited Nyakafulu Joint Venture* na *Sub Sahara Resourses (T) Limited* kama nilivyoeleza hapo juu.

(b) Mheshimiwa Spika, kampuni hizi zinafanya utafutaji wa madini katika maeneo ya leseni zao kwa kuzingatia masharti ya leseni hizo. Hivyo Wizara yangu haijabaini ukiukwaji wowote wa Sheria unaopaswa kuchukuliwa hatua. Aidha, shughuli za utafutaji wa madini zinahitaji mtaji na muda wa kutosha hadi kufikia kugundua mashapo ya kutosha kuchimbwa kwa faida na kisha kujenga na kufungua mgodi. Kama kiasi cha mashapo ya madini kilichogunduliwa hakiwezi kuchimbwa kwa faida. Kampuni husika inaweza kuchukua uamuzi wa aidha kuendelea kufanya utafutaji wa madini hadi itakapofanikiwa kugundua mashapo ya kutosha, au kusitisha shughuli zake na kuliachia eneo hilo. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira ili kampuni zinazoendelea na utafutaji wa madini katika maeneo ya Jimbo lake zikamilishe kazi zao za utafutaji wa madini.

Manufaa yanayotarajiwa kwa wananci wa Bukombe na Taifa kwa ujumla kama kampuni hizo zitafanikiwa kufungua migodi mikubwa ni pamoja na ajira na malipo ya mrabaha na kodi mbalimbali. Vilevile, makampuni hayo yatatumia bidhaa pamoja na huduma zitolewazo na kampuni za hapa nchini.

(c) Mheshimwia Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, shughuli za utafutaji wa madini katika maeneo aliyoyataja Mheshimwa Mbunge bado zinaendelea. Tayari kampuni husika zimegundua madini aina ya dhahabu katika maeneo hayo. Shughuli za utafutaji wa madini zinazofanyika sasa zimelenga kugundua kiwango cha kutosha cha mashapo ya madini kitakachowezesha kuchimbwa kwa faida.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana kwa kunipa niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa utafiti huo umechukua muda mrefu bila mafanikio yoyote wakati kampuni ya *Resolute Limited* walisema wakati mnatembelea pale wakasema hawajapata dhahabu ya kutosha kufungua mgodi katika eneo hilo. Je Serikali inaweza ikasitisha

mkataba wao ili wamiliki wa maeneo hayo waweze kuingia na mkataba na makapuni mengine yanayopahitaji katika kuchimba pale?

Pili, je, ni lini mikataba ya makampuni haya itakwisha katika eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuanza ningependa kuweka wazi kwamba wachimbaji katika eneo hilo husika hawana makataba wa madini, wanaleseni ya kuchimbia madini, na leseni yao itakwisha tarehe 4 Julai, 2007. Ningemwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira mapaka hiyo tarehe 4 Julai, 2007, kwa sababu kuna uwezekano kwamba watapata mashapo ya kutosha ili kuingia kwenye uchimbani mkubwa.

Na. 54

**Makato Mbalimbali kwa Zao la Pamba**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, yapo makato mengi yanayofanywa kutokana na Zao la Pamba yakiwemo yale ya kuliendeleza zao hilo, lakini kwa bahati mbaya zao hilo haliendelezwi na makato hayo hayajulikani yanafanya kazi gani, na kuwa kuwa *TCMB* hukata sh.25/= kwa kila kilo moja ya pamba kwa ajili hiyo:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza katika misimu ya 2003/2004; na 2005/2006 imekusanya shilingi ngapi kutokana na makato ya sh.25/= kwa kilo ya Pamba katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga?

(b) Je, kwa *Wilaya* ya Kwimba, *TCMB* ilijizolea shilingi ngapi za fedha hizo zilitumika kwa kazi gani?

(c)Kama fedha hizo hazikufanya kazi iliyokusudiwa. Je kuna haja gani ya kuendelea kuwatwika mzigo wakulima kwa kuilea *TCMB*?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganda Ndassa, Mbunge wa Sumve, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makato ya Mfuko wa Kuendeleza zao la Pamba yalianzishwa kwa uamuzi wa Wadau wa Zao la Pamba mwaka 1999 kwa madhumuni ya kuendeleza zao hilo na kwa lengo la usambazaji wa pembajeo kwa wakulima, ugharimiaji wa shughuli za utafiti wa pamba na utoaji wa taarifa za soko pamoja na utoaji elimu kwa wakulima wa pamba. Kwa kupitia Mfuko huu, mwaka 2003/2004 ulianzishwa Mpango wa Kitaifa wa Pembejeo za pamba ambao uliweka utaratibu wa kutumia Vitabu vya

Akiba *(Pass Books)* kwa wakulima ambavyo humwezesha mkulima kujiwekea akiba ya fedha kila anapouuza pamba yake kwa ajili ya kujinunulia pembejeo wakati wa msimu wa kilimo.

Chini ya Mpango huu mkulima amekuwa akichangia shilingi 20/= , kusema kweli si shilingi 25/= kwa sababu ile 5/= nyingene ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema kwenye sahihisho ni ule ushuru wa Bodi ya Pamba ambao kwa sasa na umeondolewa. Kwa kilo ya pamba anayouza na siyo shilingi 22/= kama inavyosemwa kwenye swali. Fedha hizo zimekuwa zikikusanywa na Mfuko wa Kuendeleza Zao la pamba. Kati ya shilingi 20/= ambazo mkulima huchangia, shilingi 15/= sawa na asilimia 75 huingizwa kwenye kitabu cha mkulima kwa ajili kununulia pembajeo wakati wa msimu wa kilimo, shilingi 5/= ambazo sawa na asilimia 25% hutumika kugharamia usambazaji wa mbegu, kuchangia utafiti, kutoa taarifa za soko na elimu kwa wakulima pamoja na uendeshaji wa Mfuko wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kupitia matumizi ya Mfuko huu wa Kuendeleza Zao la Pamba upatikanaji na matumizi ya viwatilifu yameongezeka kutoka Paketi yenye pembajeo za kuanzia ekari moja (*acre packs)* 100,000 msimu wa 2000/2001 hadi *acre packs* 1,200,000 katika msimu wa 2005/2006. Utaratibu huu umechangia kuongezeka kwa uzalishaji wa pamba kutoka marobota 196,000 msimu wa 1999/2000 hadi marobota 697,390 msimu wa 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika misimu ya 2003/2004, 2004/2005 wakulima wa Mikoa ya Mwanza na Shinyanga walichangia mfuko wa Kuendeleza zao la Pamba kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Mwanza ulikusanya jumla ya shilingi bilioni 4.24; ambapo mwaka 2003/2004 zilikusanywa shilingi milioni 626.1, mwaka 2004/2005 zilikusanywa shilingi bilioni 1.82 na mwaka 2005/2006 zilikusanywa shilingi bilioni 1.84. Kwa Mkoa wa Shinyanga zilikusanywa jumla ya shilingi bilioni 11.17; ambapo mwaka 2003/2004 zilikusanywa shilingi bilioni 2.4, mwaka 2004/2005 zilikusanywa shilingi bilioni 4.09 na mwaka 2005/2006 zilikusanywa shilingi bilioni 4.68.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kwimba, Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba ulikusanya jumla ya shilingi 160,597,905/= katika misimu mitatu kama ifuatavyo:- msimu wa 2003/2004 shilingi 22,425,575, msimu wa 2004/2005 shilingi 63,533,175 na msimu wa 2005/2006 shilingi 74,639,155.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifuatilia kwa karibu sana athari zinazompata mkulima akutokana na makato mbalimbali kutoka kwenye mauzo ya mazao yake yakiwemo yale ya kuchangia Mifuko ya Kuendeleza Mazao hayo na kugharimia Bodi za Mazao zinazohusika. Kutokana na hali hiyo imedhihirika wazi ya kwamba

makato mbalimbali yanayofanywa kwa wakulima yakiwemo yale ya kuchangia ugharmiaji wa Bodi hizo ikiwemo *TCMB* yamekuwa yakipunguza mapato ya wakulima yanayotokana na mauzo ya mazao. Ni kwa kuzingatia hali hiyo kuanzia mwaka wa fedha wa 2006/2007 Serikali imeamua kuwa uendeshaji wa Bodi za Mazao zote ugharmiwe kwa asilimia mia moja (100%) na Serikali. Aidha, makato kwa ajili ya changia Mfuko wa Elimu yaliyokuwa yanakatwa nayo yataondolewa kwa kuzingatia kwamba Serikali imetoa fursa nyingine za kuendeleza elimu kupitia mipango ya MMEM, MMES na *TASAF*.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na maelezo mazuri na marefu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza.Kulingana na utaratibu wa Mfuko huu endapo mkulima hatakwenda kuchukua dawa pamoja na mbegu, mkulima huyu haruhusiwi kwa mwaka ujao kuchukua hizo mbegu. Je, Serikali haiwezi ikabadilisha utaratibu huo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE):** Mheshimiwa Spika, katika maelezo ya jibu la msingi hapa nimeeleza kwamba utaratibu wa pembejeo za pamba kitaifa umeruhusu utaratibu unaowezesha kuanzisha *pass book* ambao unafanya kazi kama *saving account.* Kwa sababu fedha hizi zinawekwa kwenye kitabu cha akiba ya mwanachama.

Kwa hiyo ni imani yangu nadhani katika utaratibu wa ku-*operate* fedha hizi kama *saving account* fedha zitakuwa zinapunguzwa kwenye akaunti ya mwanachama pale tu amabapo atakuwa amezitumia kununua pembejeo na kuongezwa kwenye akaunti ya mwanachama pale ambapo anakatwa kutokana na mauzo yake. Kwa hiyo, kama utaratibu ambao Mheshimiwa Mbunge anaueleza sasa hivi kwamba huenda fedha hizi mtu asipochukua pembejeo zinabakia kulekule ni suala la kufuatilia halafu tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge. Lakini utaratibu ambao nimeueleza hapa nadhani ni muafaka kwa sababu uwekaji wa akiba unaruhusu kutoa na kuweka.

Na. 55

**Kilimo cha Umwagiliaji**

**MHE. KAIKA S. TELELE (k.n.y. MHE. CHRISTOPHER OLE-SENDEKA)** aliuliza:-

Kwa kuwa vijiji vya Kizuiani, Lemkuna, Ngage, Loiborsoit, Ruvu-Remiti na Gunge vinapitiwa na Mto Pangani (Ruvu) na kwa kuwa maeneo hayo yana mabonde mazuri yafaayo kwa kilimo cha Umwagiliaji; na kwa kuwa sehemu kubwa ya Wilaya hiyo inapata mvua kidogo kuweza kustawi mazao ya chakula na biashara na kwa kuwa umwagiliaji unaotumika sasa hauwezi kukidhi mahitaji kwa wakulima na wakazi wa maeneo hayo kwa ujumla:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mifereji ya umwagiliaji katika vijiji hivyo?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga fedha za kuboresha umwagiliaji katika bonde hilo ili kupunguza umaskini uliokithiri katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christropher Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, lenye sehemu (a), na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mpango kamambe wa umwagiliaji maji mashambani *(National Irrigation Master Plan (NMP)* ambao umeyatambua maeneo ya Kizuani, Lemkuna, Ngage, Loiborsoit, Ruvu-Remiti na Gunge katika bonde la mto Pangani kwamba yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashamba ili utaratibu wa umwagiliaji unaotumika sasa katika maeneo hayo haukidhi mahitaji kwa wakulima na wakazi wote wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Waziri yangu imeanza kuchukua hatua za kuyaendeleza maeneo hayo kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya umwagiliaji ya maeneo hayo. Baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa uboreshaji ni pamoja na skimu ya Lemkuna ambapo Serikali ilitumia shilingi milioni 604.47 ili kuboresha miundombinu ya mradi huo katika mwaka wa fedha 2001/2002 chini ya mradi uliojulikana kama *River Basin Management and Smallholder Irrigation Improvement Project*. Aidha Waziri kupitia Kanda ya Umwagiliaji wa Manyara, itasaidiana na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro Kuandaa andiko ili liweze kuingizwa kwenye mpango wa maendeleo wa Wilaya (*DADP*) ambapo utapangiwa fedha kutokana na Basket Fund ya Progamu ya Maendeleo ya *Sector* ya Kilimo (*ASDP*). Maandiko hayo pia yataweza kutumika kuombea fedha kutoka vyanzo vingine vikiwemo vile vya *TASAF*, *Japanese Food Aid Counterpart Fund* pamoja na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali.

(b) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2004/2005, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADP's*) kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani katika baadhi ya maeneo hayo. Kwa mfano; miradi ya *Loiborsoit* ilitengewa shilingi milioni 12, Limkuna shilingi milioni 1.5, Gunge shilingi milioni 1.5 na Ruvu Remiti Shilingi milioni 14. Fedha hizi ni kiwango kidogo lakini kwa kutumia mbinu shirikishi zinafanya kazi nzuri sana.

Aidha, katika Programu ya maendeleo ya kilimo (*ASDP*) ya miaka saba 2006/2007 hadi 2012/2013 ambayo utekelezaji wake unaanza rasmi katika bajeti ya mwaka 2006/2007 jumla ya shilingi *trilioni* 1.4 zimetengwa kwa ajili ya miradi ya kilimo cha umwagiliaji ya ngazi ya Wilaya itakayoibuliwa miongoni mwa wakulima vijijini wakati wa kuandaa *DADPs* itakayopangiwa fedha kutoka kwenye *Basket Fund* ya *ASDP*.

Aidha umeonyesha kwamba pale ambapo maandiko ya ukarabati wa skimu za umwagiliaji yamefanywa kwa makini na kitaalam, kuna uwezekano wa kuomba fedha kutoka katika vyanzo vingine kama vile *TASAF*, *WFP (Food For Work)*, *Food Aid Counterpart Fund* na Mashirika mengineyo yasiyo ya kiserikali

Na. 56

**Malipo kwa Watumishi Walioachishwa Bodi ya Pareto Iringa**

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeahidi kuimarisha Utawala Bora nchini kwa kufuata Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa nchini kote kuanzia ngazi ya Vitongoji hadi Taifa.

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa watumishi waliotumikia Kiwanda cha Pareto Mkoani Iringa na baadaye kuachishwa kazi na Bodi ya Pareto hawajalipwa stahili zao *(Terminal Benefits)* kwa mujibu wa Kanuni na taratibu tangu mwaka 2000?

(b) Je, Serikali inaahidi nini juu ya malipo ya Watanzania hao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Pareto Tanzania (*TPB*) ilianzishwa kwa sheria ya Bunge Na 1. ya mwaka 1997 kusimamia zao la pareto hapa nchini. Kufuatia urekebishaji wa sekta hii, baadhi ya watumishi katika Bodi na Kiwanda ilibidi waachishwe kazi na kulipwa mafao yao kulingana na Sheria na taratibu chini ya Tume ya Rais ya Kurekebishwa Mashirika ya Umma *(PSRC)*. Watumishi hao walilipwa na Serikali stahili zao zote kisheria kama ifuatavyo:-

(i) Mshahara wa mwezi mmoja badala ya *notice*.

(ii) Malipo ya mshahara wa mwezi mmoja kwa likizo iliyokuwa bado haikuchukuliwa na mfanyakazi.

(iii) Malipo ya nauli ya mtumishi, mme/mke na watoto wanne wenye umri chini ya miaka 18 hadi anakotoka,

(iv) Gharama za usafirishaji wa mizigo hadi anakotoka kulinga na cheo cha mtumishi husika. Aidha, wamelipwa pensheni zao kulingana na taratibu za mifuko ya pensheni waliyokuwa wanachangia.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Kiwanda cha Pareto hawakuridhika na malipo hayo wakitaka kulipwa mafao kulingana na mkataba wa hiari ambao haukuwa umesajiliwa kisheria. Hivyo walifungua kesi Na. 16 ya mwaka 2000 katika mahakama kuu Mbeya dhidi ya Bodi ya Pareto na *PSRC*. Kesi hii bado inaendelea. Hivyo kisheria tunalazimika kusubiri uamuzi wa mahakama.

Na. 57

**Matumizi ya Water Guard**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** Aliuliza:- Kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa hapa nchini kumekuwa na dawa ya kusafishia maji iitwayo *Water Guard*, ambapo mwongozo wa matumizi ya dawa hiyo umo katika vichupa vinavyohusika pamoja na matangazo ya biashara yanayotolewa na vyombo vya habari:-

(a) Je, Serikali kupitia *TBS* imeridhika na kuruhusu matumizi ya dawa hiyo?

(b) Je, dawa hiyo haileti madhara kwa mtumiaji atakayekosea matumizi yake?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa kupitia Shirika la Viwango, *TBS*, imeridhika kabisa na kuruhusu matumizi ya *Water Guard* na hii inatokana na *TBS* kushughulikia utengenezaji wa kiwango cha dawa hiyo kijulikanacho kama *TZS* 784:2003. Mwezi Juni, 2003 *TBS* ilikagua ubora wa dawa hii na ikaridhika kuwa imefikia kiwango cha ubora kinachotakiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, dawa hii ya *Water Guard* kama dawa nyingine ni kemikali, ni bora vipimo vilivyoelezwa vizingatiwe. Hata hivyo tahadhari kubwa imechukuliwa kwamba wauzaji wote wameelezwa na kuelekezwa utaratibu mzima wa matumizi ya dawa hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge saa ya maswali imekwisha. Ninalo tangazo tu. Katika Gazeti la leo la Majira kuna Kichwa cha Habari kinachosema: " Dawa za Kichina sasa Marufuku." Sasa mimi nimeomba jibu kutoka Serikalini alilojibu Naibu Waziri kuhusu suala hili.

Ukweli ni kwamba Dawa zilizopigwa Marufuku siyo dawa kutoka China tu, bali ni dawa za aina zote ambazo hazikuhakikiwa na hususan zile za mitishamba! *(Makofi)*

Natoa rai kwa wenzetu Waandishi wa Habari kwamba kwenye mambo kama haya na hususan yale yanayohusu mahusianao ya nchi yetu na nchi nyingine mbali mbali, taarifa kama hizi zinaweza zikaharibu mahusiano baina ya nchi na nchi. *(Makofi)*

Zipo dawa nzuri sana za Kichina zinazopitia uhakiki wa *TFDA*, na mimi hapa Spika, mnaniona sizeeki haraka kwa sababu baadhi ya dawa ninazitumia hizo! Kwa hiyo, naomba wenzetu wa gazeti la Majira kwanza wasahihishe kwa sababu ukweli upo katika jibu ambalo wote tunalo. Liko katika maandishi kwamba ni baadhi ya dawa za mitishamba kutoka China ambazo hazikuhakikiwa. Lakini, nyingine zote zinazoingia kihalali na kupata uhakiki zinaruhusiwa hapa nchini.

Waheshimiwa Wabunge ahsanteni sana! *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2005, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Katika orodha yangu anayetangulia ni Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, ambaye simwoni hapa. Anafuatiwa na Mheshimiwa Fred Mpendazoe, yeye yupo. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Fred Mpendazoe atafuatiwa na Mheshimiwa Shally J. Raymond na Mheshimiwa Mariam Mfaki, ajiandae.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Hoja mbili zilizowasilishwa na Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha. Kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza kwa dhati kabisa Serikali ya Awamu ya nne kwa hatua mbali mbali ilizochukua kuhakikisha kuwa pamoja na misukosuko ya ukame, upungufu wa chakula, umeme na kupanda kwa bei ya petroli, lakini Serikali imetekeleza majukumu yake bila kuyumba. Napenda kuipongeza kwa dhati Serikali ya Awamu ya Nne. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kishapu, naomba nitumie fursa hii kuishukuru Serikali kwa jinsi ilivyoshughulikia tatizo la njaa na matatizo mbali mbali ambayo yamewakabili wananchi.

Mheshimiwa Spika, mpango na bajeti iliyowasilishwa, inatoa matarajio na matumaini makubwa kwa wananchi wa Tanzania. Wananchi wengi wanaiunga mkono bajeti iliyowasilishwa na mimi naomba niungane na wananchi, niungane na wale walitangulia kuzungumza kuiunga mkono hoja hii na pia naomba niwapongeze Mawaziri, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakhia Megji pamoja na watendaji katika Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, bajeti ni bajeti ya kijani, ni nzuri ambayo imezingatia masuala ya mazingira. Tunaipongeza sana Serikali kwa bajeti hiyo. Naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichangie katika sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, maji ni muhimu kwa uhai. Bila maji hapa duniani hatuwezi kuishi. Maji ni muhimu kwa ajili ya maendeleo. Sekta zote, karibu zote muhimu; sekta za kilimo, sekta ya umeme au nishati, sekta nyingi zote kukua kwake zinategemea maji. Nchi ambazo zimeendelea duniani kama nilivyozungumza nilipochangia Hotuba ya Mheshimiwa Rais, nchi zote zilizoendelea duniani, zimewekeza zaidi katika sekta ya maji. Nchi ambazo hazijaendelea ama zina maji mengi lakini hazijawekeza vya kutosha katika sekta ya maji au hazina maji. Kwa hiyo, tunaona umuhimu wa sekta ya maji katika ukuaji wa uchumi katika nchi yoyote.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa hali ya uchumi ulivyoonyesha, mwaka jana au mwaka wa fedha uliopita; sekta ya maji na umeme, zimechangia kwa asilimia 1.6 tu katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Kidogo moyo wangu ungesimama kutokana na uchangiaji huu wa sekta ya maji katika nchi yetu kwa kweli bado ni mdogo.

Lakini, ninachopenda kuishauri Serikali ni kuchukua hatua za makusudi kuongeza bajeti katika sekta ya maji na hasa katika uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji nchini. Ukiangalia bajeti kuanzia miaka ya tisini, kumekuwepo kuongezeka katika bajeti katika sekta ya maji. Ni kweli bajeti inaongezeka katika sekta ya maji, lakini inapoongezeka ni katika huduma za maji, si katika uendelezaji na utunzaji rasilimali za maji. Ndicho ninachokiona kinaweza kikaleta matatizo hapo katika wakati wa usoni. Ukisoma Sera ya Taifa ya maji, inatuonyesha kwamba mwaka 2025, Tanzania itakuwa miongoni mwa nchi ambazo zitakuwa na upungufu mkubwa wa maji.

Kwa hiyo, kuna haja kwa Serikali kuwekeza zaidi katika utunzaji na usimamizi wa rasilimali za maji. Kutunza vyanzo vyetu vya maji. Tusipofanya hivyo, 2025, tunaweza tukajikuta tuko katika matatizo makubwa zaidi. Katika kuwekeza katika utunzaji wa rasilimali za maji, naiomba Serikali kuzingatia vile vile kuimarisha ofisi za maji za Mabonde. Serikali ya Awamu ya Tatu imeweza kuanzisha ofisi za Mabonde zote zilianzishwa, lakini ofisi hizi bado zinawatendaji wachache, vitendea kazi havitoshi na niseme tu kwamba na maslahi ya wafanyakazi wa ofisi za mabonde hayajawa mazuri. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali sana izingatie uwekezaji katika sekta ya maji hususan katika utunzaji wa rasilimali za maji, tuimalishe ofisi za mabonde, tuboreshe maslahi ya Maafisa wa Maji wa Mabonde.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya maji, naomba kuipongeza serikali ya Awamu iliyopita kwa uamuzi wa makusudi wa kuchukua maji Ziwa Viktoria na kupeleka katika Mkoa wa Mwanza, Shinyanga. Naipongeza vile vile Serikali ya Awamu ya Nne kwa makusudi kabisa imeamua kujenga Bwawa la Kidunda kwa ajili ya maji kwa Mji wa Dar es Salaam.

Dar es Salaam ni kioo cha Taifa letu, ni uamuzi mzuri kuamua kujenga Bwawa kwa ajili ya maji kwa ajili ya Mji wa Dar es salaaam. Vile vile naipongeza Serikali kwa ajili ya programu ya maji safi na usafi wa mazingira kwa nchi nzima kwa sasa na kwamba kila Wilaya, vijiji kumi vitachukuliwa kwa ajili ya mradi huu.

Lakini, niiombe Serikali; Kumekuwa na malalamiko katika Awamu iliyopita ya huu mpango wa maji safi na usafi wa mazingira. Malalamiko ambayo yamekuwepo kwa wananchi ni kwamba fedha zilikuwa haziendi kwa wakati muafaka. Ilikuwa inawa-*frustrate* sana wananchi. Kwa hiyo naiomba Serikali ya Awamu hii katika mradi huu ambao unagusa nchi nzima, Wilaya zote, fedha zilizotengwa zifike katika maeneo kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali kwa ajili ya Wilaya ya Kishapu, vijiji vya Sekei, Ididi vimeingizwa katika programu hiyo. Mji wa Maganzo, umeingizwa katika programu hiyo, Lagana, Iboja, Mwamashimba, Kiloleni. Ninachoomba Serikali ipeleke fedha kwa wakati muafaka ili miradi hiyo iweze kutekelezwa kwa wakati unaokubalika.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie sasa sekta ya kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo na zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wa Tanzania ni wakulima na wafugaji. Kilimo kitatukomboa tu kama tutaelekea kama Serikali ilivyoamua kuzingatia kilimo cha umwagiliaji. Kwanza, niipongeze Serikali kwa uamuzi huo wa kutoa kipaumbele katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Kishapu mwaka jana ilipata matatizo makubwa sana ya ukame na upungufu wa chakula. Lakini, nikueleze tu kwamba katika Wilaya ya Kishapu yapo maeneo ambayo yanaweza kufaa kwa kilimo cha umwagiliaji na tukaweza kulima na kujitosheleza kwa chakula. Kwa hiyo, naiomba Serikali izingatie Wilaya ya Kishapu.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ya Itilima, yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, yapo maeneo ya Kata ya Talagadijong, yanafaa kwa ajili ya umwagiliaji, yapo maeneo ya Kata ya Masanga Bulekela yanafaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, yapo maeneo Kata ya Mwakikoya- Ngeme yanafaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, upo Mto Tungu kwa jina langu hili, unafaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji vizuri sana na upo Mto Mumbu na Manonga.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweze kuchukua Wilaya ya Kishapu, moja ya Wilaya ambayo ipewe kipaumbele kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na maeneo hayo yapewe kipaumbele ili tuweze kulima na kujitosheleza kwa ajili ya chakula. Wasukuma hatupendi kulishwa, kuchukua misaada ya chakula. Sisi tunapenda sisi wenyewe kujitegemea. *(Makofi)*

Lakini, tunaiomba Serikali ituunge mkono katika maeneo hayo niliyoyataja iweze kupanua maeneo ya umwagiliaji na kuboresha *scheme* kama ile ya Itilima ambayo inaweza kutoa kama magunia 25 mpaka magunia 40 ya mpunga kama itaboreshwa. kwa hiyo ninaomba Serikali izingatie maeneo hayo. Lakini kwa haraka haraka nizungumzie Kilimo cha Pamba.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha Pamba hakijawasaidia wakulima, sana wanaonufaika sasa ni wanunuzi na wale wenye ma-*ginnery***.** Ukilima Pamba heka moja, unaweza ukapata kilo 300/400, ukiuza kama una bahati unaweza kurudisha gharama,

mkulima. Lakini, mnunuzi akinunua anaenda kupata faida na hajalima. Kwenye *ginnery* anapata faida na wanaoendelea kwenye viwanda ndio wanaonufaika na kilimo cha Pamba.

Tunaomba Serikali isaidie wananchi waweze kunufaika na kilimo cha Pamba. Nakumbuka Mheshimiwa Rais alitumia na msemo wakati wa kuomba kura pale Kishapu, akasema: "Naomba na mimi mnibebeshe suala la Kilimo cha Pamba hasa bei na mimi nione nitalitatua namna gani". Nakumbusha ahadi hiyo na tuone Serikali itatusaidiaje wakulima wa pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia suala la *Passbook*. Tumezungumza katika kikao cha Sekta ya Pamba, tulieleza bayana kwamba utaratibu wa *Passbook* haufai. Haujawasaidia wananchi. Mtu anaweza kuwa amekatwa 100,000/- inawekwa katika *Passpbook, I'm sorry,* nazungumza kingereza kuonyesha msisitizo pale.

Lakini, ninachozungumza ni kwamba *Passbook*, mtu amewekewa laki moja, akaletewa pembejeo ya 25,000/- kwa mwaka huu, mwaka kesho hiyo haitambuliki. Huo siyo wizi kweli! Wakulima hawajanufaika na utaratibu huo. Tuliomba Serikali iangalie mbadala wake, iboreshe utaratibu huo ili iweze kuwasaidia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya kilimo, kingine ninachopenda kuzungumzia ni kuhusu ushirika. Mkoa wa Shinyanga asilimia 1.6 ya wananchi milioni 3, wako katika ushirika wa aina mbali mbali. Wananchi wanajua umuhimu wa ushirika, lakini wamevunjwa moyo na historia ya Vyama vya Ushirika Vikuu vya Mkoa wa Shinyanga.

Katika Sera ya Ushirika, Serikali inawajibika Vyama vya Ushirika vinapata Viongozi waadilifu. Ninaiomba Serikali itekeleze Sera hiyo, ihakikishe Vyama vaya Ushirika hasa Mkoa wa Shinyanga vinapata Viongozi waadilifu.

Wananchi wanapenda kuwa katika ushirika. Tunafahamu umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Tunafahamu kidole kimoja hakiwezi kuvunja chawa. Tunajua uamuhimu wa Ushirika, lakini wananchi wamevunjwa moyo kutokana na historia ya hapo nyuma, sina mbadala wa neno hilo! Lakini ninachoomba ni hivyo, kwamba Serikali itusaidie kutekeleza hiyo Sera. Kama nina muda, naomba kuzungumzia suala la utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Serikaili hasa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Awamu ya Nne kwa kutoa kipaumbele katika suala la uhifadhi na udhibiti wa mazingira. Na katika mpango mzima msisitizo umeonyeshwa katika upandaji miti, nakubaliana nao lakini naomba kuongeza kuishauri Serikali, tuna taka za sumu...

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kumalizika)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na Msemaji anayefuata, yapo matangazo ambayo baadhi yamenifikia sasa hivi hapa mezani, yalichelewa kunifikia ili niwatangazie. La kwanza, Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Lindi, Wabunge wanaotokana na Chama Cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Lindi, wakutane hapo *Canteen* ya Bunge hivi sasa.

Pili, Mwenyekiti wa Kamati aya Mambo ya Nje anawatangazia waumbe wa Kamati yake kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo pamoja na *Inter-Parliamentary Committee For East Africa*, saa tano asubuhi ukumbi Na. 219 Jengo la Utawala Ghorofa ya Pili.Tangazo lingine,

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu na Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa watakutana leo tarehe 21/06 saa 7.00 mchana kwenye Ukumbi wa zamani wa Bunge ambako huko watakutana na *Mobile Operators Association of Tanzania (MOAT)*

Anayefuata, namwita Mheshimiwa Shally J.Raymond ajiandae Mheshimiwa Mariam Mfaki ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Ephraim Madeje. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, namshukuru Mungu ametukutanisha hapa Asubuhi hii, tuweze kuendelea kujadili hoja hii. Nachukua nafasi hii kuunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kwa ridhaa yako niwa rejeshe Wabunge majimboni mwao waweze kuyatupia macho maeneo ambayo wanawake wanafanyia biashara. Hapa nina maana magulio. Ninaamini kabisa ukiondoa Dar es salaam, lakini huko Mikoa mingine, vijijini, wanawake wana maeneo rasmi wanayofanyia shughuli zao ambazo ni kuuza bidhaa zao. Kwa lugha hiyo, tunaita ni magulio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umri huu nilionao sasa, nimeona kwamba maeneo hayo hayajaweza kuboreshwa. Jibu rahisi nitakalopewa hapa, labda nitaambiwa ni kazi ya Halmashauri. Lakini kuna mambo ambayo ni makubwa zaidi na kwa vile unakuta kodi za kule ni kidogo au hakuna kabisa, basi unaona maeneo yenyewe ni duni. Nitasema mfano mmoja:

Maeneo ya Magulio ni maeneo ambayo chakula kinauzwa, ni maeneo ambayo akinamama wanajiandaa kwenda wakijua kwamba watakutana na wenzao. Ni maeneo ambayo watu mbali mbali hukutana na pia kuchukua bidhaa kupeleka mbali kama Dar es salaam, masoko makubwa kama Shimoni Kariakoo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini utakuta bidhaa hizo zinawekwa chini na anapokuja hata mwingine kuuliza bei, anaonyesha kwa mguu. Shilingi ngapi hii, labda ni ndizi, labda ni mboga, labda ni miwa. Lakini kwa vile ni chini basi naye anatumia mguu kuonyesha hii ni shilingi ngapi!

Mheshimiwa Spika, ni hali duni, ni hali ambayo haipendezi. Mwanamama huyu amejiandaa toka asubuhi amevaa vizuri, nadhifu kabisa, wengi wao kwenda kwenye magulio ni *outing*, lakini akifika pale hali anayoikuta haipendezi kabisa.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali pamoja na shughuli nzuri iliyoanza sasa ya kuboresha masoko, itupie jicho pia kwenye magulio. magulio hayo yajengewe vyoo, magulio hayo yawekewe maeneo ya kuweka bidhaa, maeneo hayo yaangaliwe pia kwa usafi.

Mheshimiwa Spika, nitataja baadhi ya magulio. Nitokako mimi katika Mkoa wa Kilimanjaro kuna magulio katika maeneo ya Mashati, Kuna magulio Maore, kuna magulio Sanya, kuna magulio mengine huko Uru, kuna magulio Kiboriloni hilo ni soko kubwa la Kimataifa ndiyo maana wote hapa mnaniambia Kiboriloni.

Mheshimiwa Spika, Lakini nalo pia Kiboriloni hali ya soko hilo ni mbaya. Ukiondoa kule wanakotundika mitumba, huko kwingine kote hakupendezi kabisa. Hivyo basi, naiomba Serikali iweze kutupia jicho eneo hili ili liweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie elimu. Mpaka sasa Serikali imeboresha elimu na maeneo ya elimu na hata kujitahidi kutoa walimu kwa wanafunzi wa *primary* na *secondary*. Huko sina shaka nako. Namuomba Mungu hali iliyoanza iendelee na tuzidi kuboreka. Lakini elimu ninayoizungumzia leo ni elimu ya watu wazima. Siku za nyuma, elimu ya watu wa zima iliwekewa mkazo watu wazima wajue kuandika, kusoma na kuhesabu.

Lakini sijui ni kitu gani kimetokea hivi sasa hata zile ofisi za elimu ya watu wazima, hazionekani tena. Yale madarasa yalikuwa yanaanza saa kumi jioni hivi vijijini kwa elimu ya watu wazima, hayapo tena kabisa. Hivi majuzi tulikuwa tunapiga kura, lugha iliyokuwa inatumika ni kwamba na kama mpiga kura amesahau miwani nyumbani.

Sasa unajiuliza, hivi miwani ni ipi? Basi unaambiwa ni lugha nzuri tu ya kusema kwamba huyu mtu hajui kusoma na kuandika. Hivi kweli hii hali itaendelea mpaka lini!

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iangalie tena upya jinsi gani elimu kwa watu wazima itakuwa endelevu kwa sababu haya yote tunayozungumza kwamba tunataka kuboresha maisha ya watu, tunataka kuondoa umaskini, tunataka kuleta uongozi bora, kwa watu hawa.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA hautaeleweka kama watu wa kawaida hawana elimu. Inabidi watu hawa waelimishwe, watu hawa waweze kusoma hata vile vitabu vya MKUKUTA, vile vyenye makatuni, watu hawa waweze kuzungumza lugha inayoeleweka, watu hawa waweze kuongea na vijana wao ambao wanasoma sasa. Watu wanagharamia shule wanapeleka watoto shule wasome kiingereza, kiswahili na hata lugha nyingine.

Hakuna shaka kwamba mtu anaeanza kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili anatofautiana na mtu mwenye *Masters* anayeanza kujifunza kusoma na kuandika

Kifaransa na Kijerumani. Ninaomba kabisa ziwekwe jitihada mahususi ili watu hawa wawe wanasoma kwa sababu hawakupenda wao kutokwenda shuleni.

Bali labda kwa kukosa ada au kwa mila potofu kwamba kuna mila ambazo mwananmke akisoma ni kwamba atamzidi mwanaume. Hiyo hatuwezi kuzuia lakini nawaomba kabisa, wale jamaa za wafugaji, jaama za wengine ambao wamekaa kwamba shule ni ngumu haitakiwi kusoma, wapewe fursa hiyo wasome wakiwa watu wazima ili waweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nizungumzie suala lingine la afya kwa jamii. Utakuta kwamba tulivyo hapa, nikizungumzia wanawake, Tanzania ina wanawake wa tabaka tatu.

Kuna wenye kipato nafuu, kuna wale wa kati wenye kipato kidogo na kuna wale ambao hawana kabisa. Wanapokwenda hospitali sasa wakati huu imefikia ambapo mtu kama ni mjamzito atapimwa na ataelezwa kama akijifungua mtoto anyonyeshe au asinyonyeshe. Sasa unakuta kati yao, na hapa nizungumzie yule ambaye hana kipato.

Mheshimiwa Spika, sasa anapoambiwa akijifungua asimnyonyeshe mtoto wake maziwa yeke na maziwa yanayopendekezwa ni maziwa ya kopo ambayo yanlauzwa madukani. Mimi najiuliza huyu mama atapata wapi maziwa haya ya kopo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kitu kigumu sana yule ambaye hali yake ni afadhari kidogo atapata kwa sababu ana uwezo yule ambaye ni afadhari pia atapata. Lakini yule ambaye ni hali yake duni kabisa atafanyaje? Mtoto huyu anaweza akazaliwa hakuathirika lakini mama huyu hana namna ya kumnyonyesha mtoto. Mimi nilikuwa naomba niulize hana hana namna ya kumnyonyesha mtoto. Mimi nilikuwa naomba niulize Wizara husika itasaidiaje hali kama hii huko tuendako kwa sababu watoto hawa lazima walelewe ndiyo taifa la kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie kwenye suala la Wizara ya Fedha. Wakati ambapo wanakuja au Serikali inaamua kuuza hisa zake huwa wanafanya kampeni kubwa sana na zitateuliwa benki ambazo ni *agents* watauza hizo hisa na watu watakimbilia sana kununua hisa. Baada ya kununua hisa watu hawa wataandikishwa kama wana hisa na zoezi zima la kampeni linaishia hapo hapo. Sasa najiuliza watu wengine walionunua hisa kwa kupenda tu kusikia labda kampuni fulani inauza hisa kama *TCC, TBL* wao wanakwenda kununua hisa kwa sababu wawe wana hisa au wawekeze ili waweze kupata faida. Majibu ni mengi, kuna wengine wanakwenda kununua hisa kwa sababu faida inayopatikana benki ni kidogo sana kwa hiyo, kwa vile kule kwenye hisa inapatikana hisa kubwa wanaona bora waweke akiba yao kwenye hisa.

Lakini elimu nzima ya hisa haifahamiki Tanzania ndiyo maana utakuta hata wale walionunua hisa za awali hadi kufikia leo hawajarudi kuchukua gawio, *dividend* zimekaa kwenye mabenki hakuna mtu anayekwenda kuchukua anapokea *register* ya *dividend* hana

nafasi ya kwenda kuiulizia na mbaya zaidi *dividend* hiyo kidogo inakatwa kodi ambayo ni asilimia 10.

Sasa mwingine *dividend* hiyo hiyo ndiyo aliitegemea kama kipato chake cha mwaka, hapo hapo inakatwa kodi. Je, atanufaikaje mtu huyu aliyekimbia benki kuwekeza akaenda kuwekeza kwenye hisa? Nilikuwa naomba hili liangaliwe *With Holding Tax*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia hawa watu wa *TRA* inaonekana kwamba wanafanya kazi nzuri nami nakubali wanafanya kazi nzuri. Lakini kazi nyingi wanazofanya ni zile za kupata kodi mahali ambapo hapana usumbufu. Kodi kwa wafanyakazi, kodi kwenye vitu kama *With Holding Tax* na kodi pia kwenye mikopo ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niiombe Wizara ya Fedha iangalie jambo hili kwa sababu anapochukua mkopo mfanyakazi madhalan wafanyakazi wa mabenki anakatwa kodi kwenye ile tofauti anayopatiwa kutoka ile faida ya kwake na kiwango kilichowekwa na *BOT* inakuwa ni uonevu.

Mheshimiwa Spika, *pay as you earn* ya wafanyakazi kama wanaofanya kwenye taasisi za fedha ni kubwa hiyo ingetosha kabisa, lakini kwa vile ni agizo la kodi basi iangaliwe hiyo kodi wanayokatwa kwenye mikopo ipunguzwe watu hawa wanalia wanaandika barua hapa na pale. Ningeomba basi Wizara hiyo iangaliwe.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sasa niiombe Serikali kwa vile tuna nia mahususi kabisa ya kumkomboa mwanamke wa kipato cha chini Wizara ya Fedha, iangalie namna ambavyo itatoa *guarantees* kwa wanawake hawa ili waweze kupata mikopo midogo midogo. Lakini wasimamiwe vizuri waweze kurejesha ili fungu hilo liweze kuwa *revolving fund*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakipata hawa wakishajikomboa ihamie kwa wengine. Vile vile wakishajikomboa ihamie kwa wengine na kwa pamoja tunaweza kukuza uchumi wa nchi yetu na tunaweza pia kuboresha maisha na tunaweza kumkomboa mwanamke wa hali ya chini kiuchumi na pia kimaendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni mengi ya kuzungumzia lakini kwa vile nilikuwa nimeshaunga hoja mkoni nisingependa kengele inigongee, mengine tutaendelea kuzungumza kadri muda utakavyoruhusu. Ahsante sana. (*Makofi)*

**MHE. MARIA S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara zetu mbili zilizowasilisha bajeti zake. Kwanza nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri, wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia shughuli mbalimbali katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, suala la ungozi ni kazi ngumu lakini vile vile ningewaomba viongozi wote tuweze kuiga mfano wa Mheshimiwa Rais wetu pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi wanavyojituma kufanya kazi. Kuongoza ni kuwa na mikakati, kuongoza ni mbinu na kuongoza ni kufuatilia na ndiyo kazi wanayoifanya viongozi wetu hawa wa nchi yetu. Lakini vile vile bila kumsahau Mheshimiwa Mkuu wetu Mkoa wa Dodoma ndugu yetu Mheshimiwa William Lukuvi, jinsi alivyokuja Mkoa wa Dodoma kwa kweli amekuja kwa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya. Sisi tuna uhakika akiendelea na juhudi hizo ataubadilisha Mkoa wa Dodoma. Sisi viongozi wa Dodoma tumekubaliana naye kwamba tutakwenda naye bega kwa bega ili kuhakikisha matatizo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma kama hayataisha basi basi yamepungua kiasi fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba vile vile nimshukuru Mheshimiwa Rais kutamka na kuthibitisha kwamba Chuo Kikuu kitajengwa Dodoma. Naendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu pengine angechukua uamuzi wa kusema labda chuo hiki kikazungumzwe kwenye vikao kitajengwa wapi na wapi ingewezekana kabisa pengine chuo hiki kisingejengwa Dodoma. Naamini alijua hilo na ndio maana akatamka moja kwa moja kwamba chuo hiki kikuu kitajengwa Dodoma. Namshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nitoe angalizo kwa Serikali kwa sababu ujenzi wa Chuo Kikuu hiki ni kwamba kutakuwa na ongezeko kubwa kwa wananchi au wanachuo watakaokuja Dodoma. Ni vizuri basi Serikali ijiandae kwa kuboresha mambo mbalimbali kwa mfano umeme, hospitali, maji, barabara na mambo mbalimbali ambayo kwa kweli yatakuwa ni muhimu kwa ajili ya matumizi ya wakazi na wanachuo watakao kuwepo Mkoa wa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile ningeomba basi katika hili nililolisema Serikali itueleze, naamini si kwa mwaka huu, lakini hata kwa mwaka ujao ni vipi imejiandaa kukabiliana na ongezeko hili? Ningeomba vile vile nizungumzie suala zima la ukame wa Mkoa wa Dodoma. Haya nitakayozungumza ni kwa nia ya kusaidia, kuondoa au kupunguza umaskini katika Mkoa wa Dodoma. Sisi sote na nchi nzima na mataifa mengi yanajua kwamba Mkoa wa Dodoma, ni Mkoa wenye ukame. Mkoa wa Dodoma kuwa wenye ukame si kosa letu wakazi wa Mkoa wa Dodoma, naamini hivyo ndivyo Mkoa wa Dodoma ulivyo toka enzi na enzi. Nina uhakika kwamba sisi wa Mkoa wa Dodoma hatukupenda hali hiyo, iwe hivyo ni hali ya mazingira yenyewe ilivyo. (*Makofi*)

Sasa ili kuusaidia Mkoa wa Dodoma uweze kuwa Mkoa wa neema na tunaamini wakati mwingine mvua huwa zinanyesha nzuri na wakazi wa Mkoa wa Dodoma ni wakulima wazuri na ni wafugaji wazuri. Nina uhakika kwamba kama ingekuwa mvua zinaendelea kunyesha wala hatuna sababu ya kupata msaada wa chakula mara kwa mara ni kwa sababu mvua havinyeshi za kutosha na sisi sote tunajua. Wakati mwingine huwa tunapata mvua za kutosha tunalima mpaka tunalisha na Mikoa mingine si kana kwamba ni njaa ya moja kwa moja. Sasa ningeomba basi Serikali ibadilishe mawazo kwamba badala ya kusema tu kwamba Mkoa wa Dodoma ni Mkoa wenye ukame basi ijaribu kutafuta mbinu mbalimbali ambazo naamini kwamba zilishatafutwa na

zilishashughulikiwa bahati zilifika mahali tu zikaonekana kwamba haziwezi kuendeshwa tena kama ilivyokuwa huko nyuma.

Kwanza Mkoa wa Dodoma, tukitaka uwe na kilimo cha kuendelea kazi kubwa ni kuhakikisha kwamba Serikali inaboresha na kuchimba mabwawa katika maeneo mbalimbali. Mkoa wa Dodoma ulikuwa na mabwawa kutoka huko nyuma na kila Wilaya ina mabwawa na mabwawa haya ni mengi tu. Kwa kweli bahati mbaya siyajui hesabu yake, lakini nina orodha ya machache kwa mfano Bwawa la Ikoa, Bwawa la Dabalo, Bwawa la Hombolo, Bwawa la Chinendeli, Bwawa la Matumbulu na mengine mengi haya ni mabwawa madogo madogo. (*Makofi*)

Lakini kama sitawashukuru kwa kweli nitakuwa si mwingi wa fadhila ningeomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, kupitia kwa mama Anne Malecela aliweza kufika katika Bwawa la Matumbulu wiki iliyopita na kuona hali halisi ya bwana lile. Mabwawa haya huwa yanatumika sana na wananchi wa Mkoa wa Dodoma kwa kulima mboga mboga, nyanya na mazao mbalimbali ambayo kwa kweli yanastawi katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Serikali itajipanga vizuri ikayaboresha haya mabwawa na tuna uhakika Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuboresha mabwawa, sasa tunaomba basi katika fedha zilizotengwa sehemu kubwa itengwe kwa ajili ya Mkoa wa Dodoma, kwa sababu sisi sote humu ndani muda wetu mwingi tunakaa Mji wa Dodoma. Sasa kama kilimo kitaboreshwa kwa ajili ya kupata mboga mboga, matunda na chakula nadhani tutaishi vizuri na hata ongezeko la wananchi linalokuja hapo baadaye kwa kweli hakutakuwa na tatizo la kupata vitu mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nizungumzie mabwawa mawili makubwa, kuna bwawa moja kubwa ambalo lilishafanyiwa utafiti katika kipindi kilichopita kati ya miaka ya 1959, 1961, 1962 na utafiti wa mwisho na taarifa za mwisho ni za mwaka 1984, Bwawa la Mto Bubu ambalo kwa kweli Serikali katika kipindi kilichopita iliazimia kujenga Bwawa la Mto Bubu kwa ajili ya kuongeza maji katika Mji wa Dodoma. Ni bwawa kubwa na lilitazamiwa vile vile bwawa hili lizalishe hata umeme kwa kiasi fulani. (*Makofi*)

Sasa iliandikwa lifanyiwe utafiti si chini ya mara mbili iliandikwa vizuri ikafanyiwa makisio vizuri, lakini jambo la kushangaza sijui kitabu hiki kilizamishwa wapi. Lakini bahati sisi wa Mkoa wa Dodoma tunacho. Mheshimiwa Waziri, kama akihitaji kwa kweli tutampa, lilitazamiwa kuwa bwawa kubwa na lingesaidia kuzalisha chakula ambacho nina uhakika kwa utafiti uliofanyika kipindi hicho ni kwamba kwa kutumika kwa Mkoa wa Dodoma, pamoja na Mkoa wa Singida. Sasa tunashangaa kwa nini utafiti huu uliwekwa sandukuni na usitoke tena mpaka siku za leo ambazo kwa kweli tumejitahidi kufuatilia na kuupata.

Sasa ningeomba basi Serikali ijikite katika kuboresha Mji huu ni pamoja na kuangalia kuboresha Bwawa la Mto Bubu ambalo nina uhakika wananchi watalima kwa

kipindi chote cha mwaka mzima. Sasa watakapolima nina uhakika watapata chakula cha kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi wakazi wa Dodoma kazi yetu kubwa kwa kweli ni kilimo na nyie ni mashahidi mnapopita barabarani mnaona nyanya, vitunguu, mboga za aina mbalimbali ni kwa sababu ni za kumwagilia. Hatuna mito ambayo kwa inayotiririka maji mwaka mzima. Sisi hatuna mito, mabwawa ndiyo tunayoyategemea na mabwawa haya yanatoa hata samaki za kutosheleza Mji wa Dodoma. Sasa Serikali kama italiweka wazi na kufuatilia juu ya mabwawa haya ya Mkoa wa Dodoma kwa kweli tungeishukuru sana. Mimi niulize tu Serikali na nikumbushe kwamba Mheshimiwa Rais wetu na Mheshimiwa Waziri Mkuu, wanavyofanya kazi kwa kuthamini mambo yaliyofanywa na uongozi uliopita basi mimi nadhani Serikali itathimini utafiti huu uliofanywa na nina uhakika kama watafuatilia na naomba majibu ya Serikali iniambie kwamba ni kwa nini utafiti huu wa mabwawa uliwekwa sandukuni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo ningeomba nizungumzie Hospitali yetu ya Mkoa wa Dodoma. Naamini wengi mmefika na mmetibiwa pale. Hospitali yetu kwanza eneo ilipo pale limeshajaa nyumba, haina tena mahali ambapo labda kusema wanaweza wakaongeza nyumba nyingine. (*Makofi*)

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye hoja zilizoko mbele yetu, hoja ya Wizara ya Mipango na Hoja ya Wizara ya Fedha. Lakini kabla ya hapo ningependa kumpongeza Mheshimiwa Yusuf Makamba, kwa kuteuliwa kwake kujiunga na Bunge lako Tukufu. Mimi nikiwa mwenyeji wenu hapa Dodoma ningependa kumkaribisha hasa kwa niaba ya Matonya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuungana na msemaje aliyemaliza sasa hivi Mheshimiwa Mariam Mfaki, katika kuwakilisha shukrani za wananchi wa Dodoma Mjini na Wananchi wa Mkoa wa Dodoma kwa Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kutokana na uamuzi wake wa kujenga Chuo Kikuu kipya hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Chuo cha ukubwa huo ambao unatarajiwa kwa kweli utachangia kwa kiasi kikubwa sana katika kuongeza kasi ya ujenzi wa Makao Makuu. Nina uhakika Rais wetu aliona mbali na aliona kwamba hii ilikuwa ni njia mojawapo ya kuweza kusaidia katika kuboresha miundombinu ya hapa Dodoma ili kurahisisha au kuharakisha ujenzi wa Makao Makuu. Tunamshukuru sana kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niruhusu nikupongeze wewe na Serikali kutokana na ujenzi wa ukumbi mpya wa Bunge. Kwa miaka mingi watu wa Dodoma, walishafikia hatua ya kusema kwamba lile tamko la kusema Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali, ni danganya toto tu. Lakini hatua kama hii ya kujenga Ukumbi, ambao ni wa kisasa kabisa na ambao hauhamishiki, imewarudishia imani wakazi wa Dodoma kwamba sasa kweli Serikali iko *serious* kwa suala la kuhamia Dodoma. Tunakushukuru sana na tunaishukuru sana Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nije kwenye hoja zilizo mbele yetu. Nitoe pongezi kwa Mawaziri wote wawili Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha, kwa matayarisho mazuri waliyoyafanya kwa Bajeti ya mwaka huu. Mpango wa Maendeleo ambao umewasilishwa kwetu umetayarishwa vizuri na nampongeza Waziri pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya. Mpango huu umechambuliwa vizuri sana na Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na pia na wachangiaji mbalimbali ambao wametangulia katika ukumbi huu. Mimi sina haja ya kurudia mengi mazuri yaliyopangwa katika mpango huo, isipokuwa kuipongeza Serikali kwamba mwelekeo kwa kweli ni mzuri.

Nikija kwenye Bajeti ambayo ameiwasilisha Mheshimiwa Zakia Meghji, Bajeti hii kwa kweli ni nzuri na imepokelewa vizuri na wananchi. Kuna hatua nyingi sana ambazo zimechukuliwa katika Bajeti hii kukabiliana na matatizo mbalimbali.

Tatizo la mazingira kwa kweli limeangaliwa na pamoja na kwamba Serikali ni nadra sana kuachilia mapato yake lakini kwenye suala la mazingira Serikali imekuwa tayari kupunguza ushuru na kodi kwenye mafuta ya taa kama hatua mojawapo ya kuwashawishi wananchi waachane na matumizi ya mkaa ambao kwa kweli unatumalizia miti na unapelekea sehemu nyingi za nchi yetu kuwa jangwa. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa hatua hiyo iliyochukuliwa na pia hatua nyingine mmojawapo iliyochukuliwa ya kufuta kabisa kodi ya gesi ya kupikia. Hatua hizi mbili bila shaka zitasaidia sana harakati zetu za kuboresha mazingira ili tuweze kurudia hali ambayo ilikuwa inaridhisha huku nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wamefurahi hasa wafanyakazi kusikia kwamba Serikali imewatengea kiasi cha fedha kwa ajili ya nyongeza ya mishahara yao. Mishahara ya wafanyakazi hasa wa Serikali imekuwa duni kwa muda mrefu sana na Serikali imeshatamka kwamba ilikuwa ina lengo la kuboresha mishahara hiyo bali ambacho kimekuwa kikikosekana ni ule uwezo. Lakini katika Bajeti hii na najua pamoja na uwezo mdogo Serikali imeonyesha nia kwamba suala la mishahara duni sasa linatafutiwa ufumbuzi. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika bajeti hii kuna hatua mbalimbali zimechukuliwa kuongeza ushuru wa bidhaa fulani fulani zinazotoka nje ili kulinda viwanda vyetu na pia kuna hatua fulani fulani ambazo zinasaidia viwanda vyetu kukua zaidi zimechukuliwa katika Bajeti hii. Pia nimshukuru na nimpongeze sana Waziri kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa jinsi ambavyo imetekeleza kwa ufanisi mzuri sana Mpango wa Maendeleo wa mwaka uliopita 2005 na Bajeti yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita na kutokana na viashiria uchumi *(economic indicators)* ambazo tumepewa kwa kweli Serikali imesimamia vilivyo Maendeleo mazuri ya uchumi wetu na tukiacha wale wachache ambao wanabeza haya maendeleo au mafanikio lakini ukweli uko pale kwamba pamoja na hali ngumu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majanga ambayo yametupata katika mwaka uliopita bado *performance* ya *economy* yetu imekuwa ni nzuri na ya kujivunia na tumezipita nchi zilizo nyingi tukijilinganisha katika nyanja ya dunia, nyanja ya Afrika na hata nyanja ya Afrika ya Mashariki. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri hiyo iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusimamia vizuri uchumi, pamoja na *indicators* kuonyesha uchumi wetu unakua, lakini kwa mwananchi wa kawaida hilo halionekani kabisa.

Sasa hapa nazungumzia mwananchi wa Dodoma, Dodoma Mjini, Dodoma Vijijini, kwa kweli ni sehemu zile ambazo uchumi wetu umeonyesha kukua kwa kiwango fulani yale manufaa ya kukua huko kwa uchumi yatakuwa hayajamfikia sawa sawa mwananchi wa kawaida popote alipo hapa nchini.

Sehemu iliyokua zaidi ni sehemu ya viwanda, sehemu ya madini, sehemu ya mahoteli. Sasa ukiangalia wamiliki na waendeshaji wa shughuli hizi kwa kweli ni ama wawekezaji wa kutoka nje au ni matajiri wakubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hapa Dodoma kwa bahati mbaya sana kwa kweli viwanda ni kama vile hakuna. Mahoteli ya kitalii nayo pia hakuna. Pia kwa Dodoma hakuna matajiri wakubwa wakubwa. Kwa Dodoma ni kwa bahati mbaya sana kwa kweli viwanda ni kama vile hakuna, mahoteli ya kitalii nayo pia hakuna.

Kwa hiyo, kwa mwananchi wa Dodoma kwa kweli ongezeko la pato lake mimi ningeweza kusema kwamba ni *negative* yaani ni hasi. Sasa tufanye nini kwa ajili ya mwananchi huyu wa Dodoma? Ndugu yangu Mheshimiwa Mariam Mfaki aliyenitangulia katika kuchangia kwa kweli amelizungumzia kwa ufasaha suala lote. Mkombozi wa Dodoma ni kilimo cha umwagiliaji na nisingependa kulizungumzia zaidi isipokuwa kilimo cha kawaida yaani kilimo cha mazao ambayo yanaweza kuhimili ukame na katika hili ningependa kumshukuru Mheshimiwa William Lukuvi, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma ambaye ameshatoa mpango kabambe na sisi viongozi wa Dodoma tukubaliane naye kwamba tutahimiza kwa nguvu zetu zote ili mwaka kesho kilimo cha mazao ambayo yanahimili ukame uweze kushamiri ili angalau tuondokane na tatizo la chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba sasa nizungumzie kwa haraka tu suala la miundombinu katika Mkoa huu. Tuna bahati sana kwamba barabara ya Morogoro kuja Dodoma inakarabatiwa na imetengewa pesa za kutosha kwenye Bajeti. Barabara ya Dodoma kwenda Manyoni inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Tumeahidiwa kwamba barabara ya Arusha, Dodoma hadi Iringa inashughulikiwa. Nirudie tu kilio chetu kwamba hizi zisiwe ahadi tu, tusiishie tu kwenye upembuzi yakinifu. Lakini sasa twende kwenye utekelezaji ili hii barabara muhimu na ambayo pia itachangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya Dodoma na kuhamia kwa makao makuu Dodoma kama zikikamilika. Kwa hiyo, tunaomba sana hizi barabara zitengewe pesa za kutosha na kazi ifanyike ili yakamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba kuzungumzia barabara za hapa Dodoma mjini kama mnavyoona kwa kweli barabara za hapa hayaridhishi na kwa mji ambao tunasema ndiyo kitovu cha nchi lazima tujitahidi tufanye lolote lile linalowezekana ili tuweze kuweza kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu la barabara hapa Dodoma amepewa *CDA* lakini kwa miaka mingi sana kama tunavyofahamu *CDA* amekuwa hapewi fedha za kutosha ili aweze kuendeleza barabara. Sasa ombi letu ni kwamba sasa hali ibadilike. Nimejaribu kuangalia kuona kama *CDA* ameongezewa chochote katika Bajeti ya mwaka huu na bado nina wasiwasi. Kwa hiyo, ningeomba tupewe jibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie. Nimetoka Arusha *weekend* hii wananchi wa Arusha wamenituma nilete shukrani zao za dhati kabisa kwako wewe na Bunge lako Tukufu kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge ya hali na mali kwa msiba uliotupata kule Arusha wiki iliyopita. Kwa hiyo, nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Yusuf Makamba, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge katika Bunge hili, *boss* karibu. Tatu, nawapongeza Mawaziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Manaibu wao, Makatibu Wakuu wao na Maofisa wote walio chini ya Wizara hizi mbili kwa hoja zao mbili zilizowasilishwa hapa Bungeni. Waziri wa Fedha nikupongeze kwa kipekee kabisa hotuba yako ya Bajeti ya kwanza, umeanza vizuri. Nakutakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kabisa kwa kuwapongeza *TRA*. Waziri wa Fedha katuambia kwenye ukurasa wa 11 wa hotuba yake kwamba Serikali inaamini safari hii kwamba lengo la mapato la mwaka 2005/2006 itafikiwa bila shaka yoyote. Watu ambao wanafanya kazi na kuhakikisha malengo yanafikiwa, wanahitaji kupongezwa, kuhamasishwa na kulindwa, na naomba tufanye tufanye hivyo kama Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu si wakati wa kufanya majaribio kwenye taasisi hiyo, twende na *record* ambayo inasifika, kama rekodi inasifika basi ni wajibu wetu kuwapa nafasi ya kuendelea kufanya kazi kubwa iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nirejee malengo ya Bajeti ya mwaka 2006/2007 nianze kwa kusema kwamba naridhika Bajeti hii inaanza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. Mimi nitatilia mkazo maeneo matatu yaliyopewa kipaumbele kwenye Bajeti hii. Kwanza bajeti inazingatia umuhimu wa kuongeza rasilimali kwa ajili ya kukuza uchumi wa kama msingi wa mkakati endelevu wa kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, pili, Bajeti hii inachochea yale maeneo ya uhakika ya kuongeza ajira kwa kasi inayotegemewa na kwa njia ambayo ni endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu uwezeshaji wa wananchi kama sehemu muhimu ya mpango wa kuhakikisha maisha bora kwa kila Mtanzania, pia limezingatiwa katika bajeti hii. Lakini ili tuweze kufanikisha haya matatu Mawaziri hawa wawili wanatuambia nini. Nguvu ya bajeti hii kwa mtazamo wangu itatokana na jinsi watakavyofafanua na watakavyotekeleza yale ambayo wameyaonya katika hotuba ya Waziri wa Fedha hasa kwenye ule ukurasa wa 22 mpaka 26 yakifafanuliwa vizuri, yakitekelezwa vizuri, basi tutakuwa na matumaini makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tukiri kwamba toka walipochaguliwa Waheshimiwa Mawaziri muda mfupi sana umepita na hawakuwa na muda wa kufanya kazi yao kikamilifu. Lakini pia lazima tuwapongeze wameanza vizuri kwa kujiwekea dira na mwelekeo unaotia matumaini. Inatia matumaini namna gani. Waziri wa Fedha katika yale maeneo ambayo naona ni muhimu, anasema anaandaa taratibu ambazo zitawezesha uanzishaji wa *SACCOS* ya makundi mbalimbali ya jamii. Sasa mimi ningependa kuhamasisha waende kwa *speed* zaidi kwenye hilo. Yako ambayo yanaweza kufanyika hata kabla hizo tatatibu hazijakamilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, hivi sasa fedha za *TASAF* zinafika kwenye maeneo yetu na ni vizuri tusaidie fedha hizi za *TASAF* zielekezwe kwa njia ambayo itakuwa ni endelevu ili wakati mkopo huu wa *TASAF* utakapopevuka tuwe na vitu vya kuonyesha wananchi kwamba tunalipa deni hili la *TASAF* lakini haya ndiyo yaliyofanyika katika Taifa letu. Sasa moja ya vitu ambavyo nafikiri wangetusaidia sisi huku tunaopokea hizo fedha ni kutusaidia katika kuchangia uanzishwaji wa *SACCOS* na hatimaye uanzishwaji wa benki za wananchi katika maeneo yetu. Hizo zikianzishwa ndiyo njia endelevu za kuendelea kuwasaidia wananchi katika maeneo yetu. Hatutakuwa na vitu vya kuonyesha huko mbele wakati deni hili la *TASAF* litakapokuwa limeongezeka. Vinginevyo, pesa hizo za *TASAF* zitaingia kule, zitazama hatutakuwa na la kuonyesha.

Mheshimiwa Spika, tuna historia ya vitu vingi vya namna hiyo vinapoingia kwenye maeneo yetu na sisi tushughulikia ipasavyo baada ya muda hatuna la kuonyesha, sasa hii isiwe ndiyo hilo, tuibadilishe. Pili, Waziri wa Fedha anasema mifuko iliyopo ya dhamana itaimarishwa ili wananchi wengi zaidi waitumie na taratibu zitakamilishwa ili kuanzisha mfuko wa dhamana kwa mikopo ya maendeleo. Nawapongeza kwa kuja na hilo na kuwa *very clear* nini watakachofanya. Lakini uzoefu tulionao ni kwamba inachukua muda mrefu sana kukamilisha hizi taratibu na inachukua muda mrefu sana kwa walengwa kufanikiwa kufikiwa na mifuko hii. Sasa sisi tungependelea, tunaiomba Wizara zote mbili zihakikishe kwamba kasi na nguvu ya awamu hii inaonekana katika kuhitimisha zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, tusisite kuanzisha Taasisi kwa ajili ya kusimamia mifuko hii ya dhamana. Kwa sababu nchi zote duniani kwa yale maeneo ambayo wanayapa kipaumbele, hawakusita kuanzisha taasisi za kusimamia maeneo hayo. Tuseme Marekani, Marekani wanayo *Export Import Bank.* Kazi yake kubwa ni ku-*promote*

*exports* za Marekani huko nje. Hii ni ya Serikali hawaoni aibu kuwa nayo kwa nini sisi tuone aibu kuwa na chombo ambacho kitasukuma maendeleo katika nchi yetu.

Marekani hiyo hiyo ina *overseas private corporation* kuwasaidia Wamarekani kuwekeza nchi za nje. Wanawasaidia Wamerekani wa kuwekeza nchi za nje. Marekani hiyo hiyo ina *small business administration* kuwasaidia watu wenye biashara ndogo ndogo kuweza kuingia kutoka kwenye umaskini kuingia kwenye mkondo wa uchumi, *main stream.* Sasa sisi pia tusione aibu kuwa na taasisi za namna hiyo kwa ajili ya kusukuma maendeleo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwamba hatimaye Serikali imeona umuhimu wa kutambua *TIB* na kuiongezea mtaji kwa ajili ya mikopo. Lakini nikisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri namwona kama ana wasi wasi. Anasema hata hivyo ili benki hii iweze kuanza shughuli ya benki ya maendeleo mtaji wake hauna budi uongezwe ufikie angalau shilingi bilioni 50 kwa kuanzia. Sasa je, Mheshimiwa Waziri unatuambia kwamba *TIB* itapata shilingi milioni 50 au mnatuambia kwamba unaona ingefurahi ipewe lakini wewe unanyamaza. Sasa naomba utuhakikishie lini *TIB* itapata na utuletee mpango wa miaka mitatu mpaka miaka mitano kwamba kila mwaka *TIB* itakuwa inapata kiasi fulani ya fedha kutoka Serikalini kuongeza mtaji wake ili iweze kufanya kazi iliyopo mbele yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu kuna suala hili la *Mortgage Financing* limekwishazungumziwa sana, mimi naomba tu kwenye *Finance Releasing* tufanye kama walivyofanya watu wengine wa nje. Tumepitisha sheria hii ya Benki Kuu na Sheria ya Taasisi na Asasi za Benki inawapa Waziri wa Fedha na Gavana, mamlaka, makucha ya kushughulikia hizi benki ili pesa zao ziweze kuelekezwa katika *productive areas* za nchi zetu. Tutumie mamlaka tuliyo nayo katika sheria hizi mbili tupitishe Sheria ndogo zitakazozitaka hizi benki angalau asilimia 10 ya *portfolio* yao iwekezwe kwenye mikopo itakayoenda kwenye sekta muhimu kama kilimo na kilimo hiki sio washughulike na *marketing* washughulike na *production* uzalishaji. Sio *marketing* maana yake hivi sasa wanakula hela zetu kwa urahisi kabisa kwa mambo ya *marketing.* Lakini waelekezwe ziende kwenye uzalishaji. Kilimo, *mortgage finance* na kama kwa mwaka hawatakuwa wamewekeza wametoa mikopo kwa kiwango hicho basi wawajibike ku-*deposit* kwenye *resarve* ya Benki Kuu kwa kiwango kile ambacho wameshindwa kukifikia ili Benki Kuu sasa itumie *phase* hizo katika kutunisha dhamana mifuko yake ya dhamana kwa ajili ya kuhamasisha hizo sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanajua kwamba kama watawajibika kupeleka Benki Kuu hizo pesa hawatapata riba. Lakini wao wenyewe wakisukumwa kwa sababu wanatafuta riba, watatafuta miradi ya kuitolea mikopo. Basi hiyo ni njia mojawapo ambayo inaweza ikatumika hapa katika kuzihamasisha hizi benki kulenga katika yale maeneo ambayo tunataka yalengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni lile suala la *leasing* mwaka jana Waziri wa Fedha alisema *releasing policy statement* ni sera ya Serikali sasa mwaka huu imekuja sasa kwenye Bajeti, wanasema itapewa kipaumbele. Lakini sasa tunataka kuona kwa vitendo.

Yapo ambayo yanaweza kufanyika hata kabla huo muafaka haujapatikana na mimi nina wasi wasi sana na Kamati, kuunda Kamati kutafuta muafaka hasa kwa watu ambao *interest* zao zinagongana, hiyo itatucheleweshа. Yako ambayo tunaweza kufanya kwenye *lease* kikubwa ni kuondoa *VAT*. Tukiondoa *VAT* hata katika Bajeti hii tutakuwa tumeonyesha dira nzuri kwamba sisi tuko *sereous* na *finance lease* ukiondoa *VAT* kama tulivyoondoa katika *Air Craft Finance* katika *Air craft finance release* tumeondoa *VAT.*

Sasa hatutakuwa na sababu zozote za msingi za kuja kuwa na kodi hii ya ongezeko la thamani kwa *leasing* ya aina nyingine yoyote kama tumetoa katika *air craft.* Tukiweza kufanikisha hayo, tutakuwa tumeonyesha kwamba sisi tuko *serious* kuamua uchumi wetu. Tutaweza sasa mwalimu yule aliye pale kwenye *SACCOS* pale Arusha atakuwa na matumaini ya kwamba ataweza kupata mkopo wa kujenga nyumba yake na aulipe mkopo huo kwa muda wa miaka 20 mpaka 30 *mortgage financing*. Mkulima wangu wa trekta anaweza kubadilisha ile trekta yake ile ya zamani ambayo imepitwa na wakati akakopa trekta nyingine ya kisasa akaboresha kilimo chake pale Tera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mama yangu, Mama China pale *Unga Limited* pamoja na Juma Mzee pale Majengo wataweza kupata mikopo kwa ajili ya kuboresha biashara zao ndogo ndogo. Hayo yote yanaweza kufanikiwa tu tukikamilisha. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango wangu katika hoja zilizopo mbele yetu. Lakini kabla sijafanya hivyo nakuomba kwa ruhusa yako na mimi nitoe salaam za shukrani kutoka kwa wananchi wetu wa Arumeru kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Tanzania kwa salaam za rambirambi tulizozipata wakati wa maafa ya ajali ambapo wananchi 54 wamepoteza maisha yao na 20 wamelazwa ni majeruhi na wengine wako mahututi. Wananchi hawa wanaishukuru Serikali yao kwa kitendo hicho na hisani kubwa ya kuwakumbuka wakati huu. Ahsante sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Yusuf Makamba, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa mmoja wetu katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nampongeza sana. La pili, naomba nijielekeze kuwashukuru watoa mada Waziri wa dhamana ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa hoja zao walizowasilisha hapa na ambazo zimepitishwa na Kamati ya Fedha na Uchumi na tukaiunga mkono kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia, kuipongeza Serikali kwa mambo makuu matatu, moja, kwa kutekeleza bajeti ya mwaka wa fedha 2005/2006 kwa mafanikio makubwa sana licha ya ukame, uhaba wa chakula, kupanda kwa bei za mafuta na dizeli ambazo zingeweza kuyumbisha uchumi wa nchi yetu. Naishukuru Serikali na kuipongeza kwa jitihada hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya pili, niipongeze Serikali kwa kushughulikia suala zima la njaa. Baa la njaa liliipata nchi nzima lakini Serikali imeweza kujitahidi, hakuna maafa yaliyotokea kutokana na njaa hii. Naipongeza Serikali. La tatu, niipongeze Serikali kwa kuwa na masikio. Kabla hatujaja Bungeni kulikuwepo na malalamiko makubwa ya kutoka kwa watu mbalimbali, wananchi mbalimbali, sekta mbalimbali kuhusu bei ya mafuta. Mafuta ya petroli, dizeli, mafuta ya taa na kadhalika.

Nashukuru na naipongeza Serikali kwamba wamesikia kilio hiki cha wananchi na wameondoa ushuru na kodi ya *VAT* katika mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa na gesi ambayo itapunguza makali ya maisha ambayo yalikuwa yanatokana na kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo kwa walaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye bajeti ya mwaka 2006/2007. Bajeti hii ina mwelekeo, bajeti hii ni nzuri, wananchi wengi wameishangilia na kuisifu, imegusa wafanyakazi, wafanyabiashara, wakulima na hata wanafunzi. Bajeti hii ni nzuri lakini bado ni tegemezi kwa hiyo, inatakiwa Serikali na sisi sote tujielekeze, tujitahidi kukusanya mapato ya Serikali na kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha hizi ambazo tutazikusanya ili tuendeleze maendeleo ya nchi yetu na kupunguza umaskini katika jamii.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa mikakati mizuri ya jinsi ambavyo itajitahidi kusimamia ukusanyaji wa mapato haya na itakavyosimamia matumizi ya fedha hizi tutakazokusanya. Mimi napenda nichangie katika sehemu zifuatazo, ya kwanza ni hili la kupanua wigo wa kodi. Serikali imetueleza kwamba itapanua wigo wa kodi, sina ubishi na hilo na wala sina tatizo nalo. Lakini nina tatizo na jambo moja nalo ni misamaha ya kodi ya ushuru wa forodha na kodi ya *VAT.*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali yetu inatoa misamaha ya kodi kwa watu binafsi na taasisi mbalimbali zikiwepo *NGO's.* Kiasi cha misahamaha ya kodi inayotolewa mwezi hadi mwezi katika nchi yetu kwa wastani ni bilioni 71. Hiki ni kiasi kikubwa sana katika uchumi wetu, ni mzigo mkubwa sana. Serikali imetueleza kwamba tuna kitengo cha walipa kodi wakubwa katika Tanzania nao wako 286, mchango wao kwa mwezi ni shilingi bilioni 51 na ndiyo tunajivunia sana mchango huu kwamba ni mchango wa kutufikisha hatua kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukilinganisha shilingi bilioni 51 tunazokusanya kutoka kwa walipa kodi wakubwa na kiasi hiki cha misamaha ya kodi shilingi bilioni 71 tunaona kwamba kuna tofauti kubwa pale. Ningeomba, ningeshauri Serikali ijitahidi kurejea na kutazama upya taratibu na sheria na ulazima wa kutoa misamaha hii ya kodi. Kodi ya *VAT* na ushuru wa forodha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye sheria ya uwekezaji katika nchi yetu. Serikali imeleta mapendekezo hapa ukurasa ule wa 46 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kifungu kile cha 43(1). Serikali inapendekeza kubadili kifungu hiki katika sheria za uwekezaji katika nchi yetu. Kwa kuwa sasa hivi Serikali inapitia upya mikataba

ya Madini ningeshauri Serikali yetu itazame pia uwezekano wa kuainisha sheria hii ya madini ili kipengele hiki ki-*apply* kwa sheria hiyo ya madini ambayo inatawala mikataba hiyo madini ambayo haiko chini ya *Tanzania Investment Centre (TIC). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee sasa katika matatizo ya jamii. Nizungumzie juu ya kilimo, nafahamu Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia juu ya eneo hili. Ninafahamu uwezo wetu mdogo wa kifedha katika kuipa kilimo kipaumbele. Lakini nasema kilimo ni uti wa mgongo. Kilimo ndio mwajiri mkubwa katika nchi yetu. Inaajiri asilimia 80 ya Watanzania wanaoishi vijijini na asilimia hii lazima tuilinde. Tusipoilinda asilimia hii inayotokana na kilimo kama ikishuka na huku *population* inaongezeka, ajira hii ikishuka vijana wetu wengi watakwenda mijini. Kutakuwepo na misongamano mkubwa wa vijana wetu jeshi ambalo halina kazi katika miji ambayo itaongeza idadi ya machinga katika miji yetu. Ni lazima tujitahidi kuwekeza katika kilimo. Tufanye kilimo cha kisasa, tuweze kuwa-*retain* watu wetu kwenye kilimo, tuweze kuongeza hii asilimia 80 ya ajira ikue mwaka hadi mwaka. Hakuna njia njia nyingine ya kufanya hili isipokuwa kilimo. Kilimo chetu kiwe cha kisasa kiwavutie wakulima, vijana wabakie kwenye vijiji walime.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima pia tuboreshe kilimo chetu ili tuweze kuwa na mazao ya kilimo ambayo tunayasindika tunaya-*add value* ili tuweze kuya-*export* sasa hivi mazao yetu ya kilimo ukiangalia mazao ya chakula hakuna ambayo tunayapeleka nje. Kwa hiyo, sekta hii hata kama tunapata *forex,* tungeweza kupata zaidi kama tungewekeza katika kilimo. Ninatambua kabisa mchango wa Serikali katika hili kuongeza fedha za pembejeo lakini hilo halitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie juu ya *food security.* Nataka niseme mwaka huu tumepata mafunzo, tusipoangalia kilimo chetu hiki tunaweza kuwa na njaa kila mwaka wakati tumevuna katika msimu husika. Tuangalie upya kitengo chetu cha *food security.* Kitengo cha *SGR* cha nchi yetu mnajua kilikuwa na vipengele viwili katika sheria yake nayo ni kwamba ilikuwa iwe *buyer of last resort* yaani mazao yakishauzwa popote pengine kwenye masoko mengine ndiyo *SGR* ndiyo ije inunue chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba sasa hivi *SGR* iwe *buyer of first resort* na iwe *seller of last resort* kwa njia hiyo tutajihakikishia kwamba chakula ambacho kimevunwa, kimenunuliwa kutoka kwa mkulima kabla hajashawishika kuuza mahali pengine na baada ya hiyo ndiyo sasa wakulima wauze hiyo ziada. Tukifanya hivyo tutakuwa na chakula cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie juu ya tatizo la maji, hili sitalizungumzia kwa undani sana kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wenzangu, wameshalizungumzia kwa upana sana na kwa wingi sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshatoa msimamo kwamba kwa kweli hili ni tatizo katika nchi nzima na Serikali inajitahidi kutafuta ufumbuzi wa uhaba wa maji. *(Makofi)*

Pamoja na hilo katika jimbo langu la Arumeru Magharibi, Serikali ilichukua maji ya Mto Nduruma kwa manufaa ya wakazi wa mji wetu wa Arusha na hilo jambo wananchi wa Arumeru hawajalipinga.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali iliwaambia na iliwaahidi kwamba watapewa kiasi fulani cha fedha ili waweze kujenga vyanzo vya maji, yale yaliyobaki ili waweze kusambaza kwenye vijiji na kata mbalimbali. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi na sitaki kumsakama sana katika hili lakini nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi hawa wa Arumeru wanakuomba kwa hisani na kwa heshima na taadhima uwakumbuke katika hilo, kwa sababu wao wametoa maji kwa wenzao nao wakabakia na tatizo la maji. Kata hizo ni Bangata, Sokon, Moshono, Mlangarini, Nduruma na Bwawani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Elisa Mollel, naona Waheshimiwa Wabunge wanapata taabu na hizi dakika 15, lakini ndio zilizokubaliwa, ikilia kengele ya pili itabidi ukae hakuna tena kuzungumza. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, na mimi kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hotuba ya bajeti mbili ambazo zimewasilishwa na Mawaziri wa Fedha na yule wa Mipango. Lakini naomba nichukue nafasi hii pia na mimi niwapongeze Mawaziri kwa kuwasilisha hotuba zao vizuri, hotuba ambazo kwa kiasi kikubwa zinajibu matumaini makubwa ya Watanzania. Kabla sijajielekeza kwenye maeneo ambayo nafikiri ni muhimu niyasemee mimi naomba niseme hili la jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza Mbunge mmoja jana alisema kwamba Wabunge tunakuwa kama tunakuja tu kuunga mkono yale ambayo tayari yameshaamriwa na Serikali. Ninachotaka kuzungumza hapa ni kwamba mchakato wa Bajeti ya Serikali au bajeti *process* kwa kweli mimi nadhani sio nzuri, muda ambao tunakaa Bungeni na kuipitia bajeti kwa kweli haitoshi kwa Wabunge kuweza kuchangia inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naiomba Serikali ijaribu kubuni utaratibu ambao Waheshimiwa Wabunge watahusishwa katika ngazi zote kuanzia mwanzo wa utayarishaji wa bajeti mpaka mwisho na ndio sababu Wabunge tunaonekana kama walalamikaji ndani ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila Mbunge anayesimama aidha, analalamika kuhusu jimboni kwake au analalamika jumla kuhusu yale ya Serikali. Wabunge tunaonekana kama omba omba kwa Serikali, lakini mimi naamini kama tungeshirikishwa vizuri, kama Serikali ingebuni utaratibu mzuri pengine haya ya kupigia kelele sana Serikali hapa ndani yasingekuwepo na mimi nadhani inawezekana hata *budget session* hii isingekuwa ndefu kama ilivyo sasa na ndio sababu pia una kama watu tunarudia yale kwa sababu kila mtu anataka asisitize yale ambayo yanaligusa jimbo lake lakini pale hata yale yanayoigusa Serikali yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo la jumla, naomba na mimi nijielekeze kwa haya yafuatayo, mimi natoka kwenye eneo la kilimo, jimbo langu la Mbozi Mashariki na Wilaya ya Mbozi kwa ujumla ni Wilaya ya kilimo. Tunasema zaidi ya Watanzania asilimia 80 wanajihusisha na kilimo, lakini mimi nadhani Mbozi ningesema ni zaidi ya asilimia 95 wakazi wa kule wanajihusisha na kilimo, kwa hivyo kilimo kinabaki ni sehemu ya watu hawa. *(Makofi)*

Napenda niishukuru Serikali kupitia bajeti hii kwamba imejibu yale ambayo mengi tumeahidi kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nimepitia ukurasa wa 20 wa hotuba ya Waziri wa Fedha ameorodhesha yale ambayo kwa kweli tuliahidi kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi. Hapa yako yale yanayohusu ruzuku ya mbolea, mbegu na pembejeo za kilimo pamoja na mifugo pamoja na miundombinu ya umwagiliaji ambayo kwa hotuba ya Waziri wa Fedha haya maeneo yote yameongezewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi naomba nizungumzie sana ruzuku ya mbolea na mbegu pamoja na pembejeo za kilimo. Kuhusu mbolea bado ni tatizo kubwa na mimi naishukuru Serikali inatambua kwamba hata mbolea ni tatizo kubwa. Nilikupokuwa nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa wakati anazindua Bunge lako Tukufu nilisema mbolea kama Serikali haiwezi kuhakikisha kwamba inasambazwa kwa kiasi cha kutosha tutakuwa kila mwaka tunapiga kelele kwamba tuna njaa tuna njaa.

Mimi naomba Serikali iamue kwa dhati kabisa pamoja na kwamba imeongeza ruzuku ya mbolea kwa maana ya kutoka shilingi bilioni 12 mpaka 21 kama tulivyoelezwa, lakini bado kiasi hiki hakitoshi. Tunaipongeza Serikali kwamba imeliona imeongeza pesa, lakini bado hakitoshi na mimi nilisema wakati nachangia hotuba ile kwamba Wilaya ya Mbozi tulihitaji tani 38,000 za mbolea kwa msimu wa mbolea uliopita. Lakini tulipewa tani zisizozidi 6,500.

Mheshimiwa Spika, sasa umeomba kiasi hicho unapewa tani zisizozidi 6,500 tunategemea tuzalishe kwa miujiza ipi. Mimi nadhani Serikali lazima ichukue hatua, nchi hii haina sababu ya kwenda kuomba chakula kutoka kwa wahisani au kutoka nchi nyingine duniani na mimi naomba niungane na Mheshimiwa Diwani, Mheshimiwa George Simbachawene, alisema hapa kwamba tunachopaswa kufanya ni kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kilimo, kulikuwa na jina hapa *the big four* kwa maana ya mikoa ya Mbeya, Iringa, Ruvuma na Rukwa. Mikoa hii kama Serikali ingeamua kwa dhati kuwapelekea kiasi cha mbolea ambacho wanahitaji, mimi ninahakika nchi hii tungeondokana kabisa kabisa na tatizo la kuwa ombaomba au kuomba msaada wa chakula kutoka nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunajua Marekani si zaidi ya asilimia 10 ya Wamarekani wanaojiusisha kwenye shughuli za kilimo, lakini hawa ndio wanaolisha Marekani na kuuza ziada nje ya nchi. Lakini pia tunajua nchi kama Mauritius ilikuwa nyuma sana kwenye shughuli za kilimo na viwanda, wote tunamjua Waziri Mkuu Mstaafu Mhatili Mohamed, alipoingia madarakani kwa kweli aliibadilisha Mauritius kuwa nchi ambayo inalima sana, lakini pia ikaongeza viwanda na kwa maana hiyo kuifanya nchi ambayo si

tu kwamba inajitosheleza kwa chakula lakini pia inaweza kuuza hata ziada kwenye Mataifa makubwa makubwa duniani na yale maskini kama sisi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba hapa tujipange sawa sawa, hatuna sababu ya kuwa ombaomba wa chakula. Serikali iamue kwa dhati kabisa, lakini pia hii mbolea inayokuja tunaomba iwe na *label* hasa ya ruzuku kwa sababu mimi nilishuhudia kule jimboni kwangu mbolea imeletwa ya ruzuku haina *label,* wajanja wachache wameinunua wakizunguka wakaanza kuwauzia wananchi kwa shilingi 30,000 kwa mfuko mmoja.

Mheshimiwa Spika, lakini hii ndio mbolea ya ruzuku, tunafikiri kama Serikali ikibandika *label* na sio lazima hiyo *label* hii itoke viwandani kama mbolea ikija huku mimi nadhani tunaweza Serikali ikawa na utaratibu ya kuiweka *label,* hawa watakaonunua hawawezi kwa maana hiyo hata kwa hila wakaiuza kwa sababu itajulikana kwamba hii ni mbolea ya ruzuku na yeyote anayeweza kubainika anauza mbolea ya ruzuku anaweza akachukuliwa hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia mbolea zote zinazohusu wakulima katika nchi hii zote ziwe na ruzuku, mbolea zote ziwe na ruzuku. Mimi Jumamosi iliyopita nilienda Jimboni kwangu nilizungumza na wananchi wakasema kwa kweli kama Serikali ikitatua tatizo la mbolea tunaweza tukafanya maajabu makubwa sana kwenye kilimo na hivi nazungumza nina hakika wengi wananisikiliza na wengi wananitazama pengine tunaomba Serikali ijibu kilio cha Watanzania hawa. *(Makofi)*

Naomba nizungumze eneo la kiwanda, nilipokuwa pia nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais niliwahi kusema kwamba kama tunataka kufanya kilimo kweli kweli ni lazima tuwe na mbolea na hatuwezi kuwa na mbolea ya kutosha kwa kutegemea tu kuagiza nje ya nchi haiwezekani, Serikali ichukue hatua na mwenzangu Mheshimiwa Richard Nyaulawa, jana amezungumzia Mheshimiwa Richard Nyaulawa nni Mbunge wa Mbeya Vijijini, kwamba lazima Serikali sasa ichukue hatua, lazima tufikirie Serikali lazima ifikirie na mimi nimeshangaa kwenye hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, nilitegemea kwamba liwepo kwamba pengine Serikali ina mipango ya kujenga kiwanda cha mbolea.*(Makofi)*

Mimi nilipozungumza hili nilipokuwa nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Joseph Mungai, alisema kwamba si jukumu la Serikali kujenga kiwanda, mimi nilisikitika kidogo. Lakini inawezekani kweli sio jukumu la Serikali, lakini Serikali hii ndio inayopanga mipango, Serikali hii ndio inayoweza kuwashawishi wawekezaji na wakawekeza kwenye maeneo kama hayo. Sasa Waziri anapojibu kwamba si jukumu la Serikali na kwa kweli kwamba ninyi wa Mbeya mnaweza mkaji-*organize* wenyewe muiandikie Serikali, mimi nilishangaa sana. Kwa hiyo, naomba Serikali kwa kweli katika maeneo haya iwe *serious* kidogo kama tunataka kujikomboa katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la umeme kwa haraka haraka tumeshazungumza huko nyuma kwamba kuna miradi ya umeme ambayo imebaki ya

muda mrefu. Kule Mbozi kuna miradi mitatu ya umeme, nguzo zimechimbiwa zaidi ya miaka mitatu hamna kinachoendelea, ukiwauliza Mawaziri wanaohusika wanasema tutaweka kwenye mipango hivi tangu miaka mitatu hakukuwa na mipango yoyote inayopangwa. Mimi naomba Serikali iwe *serious* katika masuala mengine naijibu kwa kweli hoja hizi za Watanzania.

Lakini pia nataka niseme kwamba katika suala la nishati kuna suala la kule Mbozi, Mbozi ni Wilaya kubwa sana, kutoka Makao Mkuu ya Wilaya kwenda kwa mfano kwenye jimbo la Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu ni karibu kilometa zaidi ya 140. Kule tukizungumza kufikia umeme sasa wa *TANESCO* pengine inawezekana isiwe rahisi sana, tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba umeme wa s*olar*, tunajua ni ghali sana sasa hivi, lakini Serikali ipunguze gharama kwenye umeme wa *solar* ili wananchi wengi waweze kufaidika na hasa wale wa mbali na miundombinu hasa ya umeme ambapo inawezekana umeme usifike leo au kesho kutwa, na kwa kweli kule chini jimbo la Magharibi, uharibifu wa mazingira ni mkubwa sana. Tunaomba Serikali ichukue hatua za kupunguza bei ya vifaa vya *solar* ili pengine wananchi wa kule waweze kufaidika zaidi na hatua hizo.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la mawasiliano, mahali fulani nikifikiri pengine inawezekana tukawa tunaji-*contradict* wenyewe, kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukifungua ukurasa ule wa 58 tunasema kwamba tunataka kuendeleza kupanua huduma za simu za mezani na mkononi hadi ngazi ya vijiji. Lakini kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha kwenye ukurasa wa 40 tunaongeza ushuru wa kodi ya simu za mkononi na hivi karibuni Serikali inataka kuleta Muswada wa Mawasiliano, ni sawa na mtu au mwanaume unatafuta mwanamke wa kuoa halafu unamwambia mimi unajua huwa nachapa sana viboko, hivi tunategemea huyu mwanamke akukubali hata kama angekukubali, mimi sidhani kama anaweza kukubali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaongeza gharama za simu, wakati tunataka tuwaambie Watanzania ambao hawajazipata bado tunaongeza ushuru wa simu hizi, afadhali na wengine ambao tunazo tayari, lakini wale ambao hawanazo na wa kule vijijini watafikiri kwamba hakuna sababu ya kuwa na simu hizo. Kwa hiyo, hata Muswada tunaotegemea kuuleta hapa mbele, unaweza usiwe na faida sana hapo mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la mwisho kwa sababu ya muda naomba nizungumze suala la madini kidogo, nilizungumze umeme lakini nilitaka nataka nizungumze suala la madini. Kule Mbozi kuna kampuni ambazo zimeingia zinachimba madini, kampuni hizi zilipoenda hata uongozi wa Wilaya haukuwa na taarifa kwamba umeenda kule, sasa hii ilisikitisha kidogo. Kuna maeneo ya Nyimbili ambayo kuna inasemekana kuna dhahabu na watu walienda kule uongozi wa Wilaya haujui.

Kuna maeneo ya Mlima Ng'amba, jirani sana Vwawa Makao Mkuu ya Wilaya, kuna maeneo ya Bara, kuna maeneo ya Chindi kwenye jimbo la Magharibi, lakini watu wameenda au makampuni yameenda huko wanapoulizwa wanasema sisi tumeangizwa na Wizara tuje. Lakini baadaye tulipozungumza nao ni kweli walipewa *prospective licences* kwa ajili ya kuchimba madini. Wamekuwa wanachukua tani na tani za mawe wanasema

wanapeleka Italy kwa ajili kama *sampling,* hivi kitu ambacho ni *sample* unahitaji kuchukua tani na tani za mawe unapeleka huku, Serikali ya Wilaya haiambiwi chochote, makampuni yale yameharibu miundombinu pamoja na barabara katika Wilaya yetu. Sasa mimi nadhani Serikali itambue Serikali zake ambazo ziko Wilaya kwamba Serikali Kuu yenyewe imeziweka, lakini pia iziheshimu watu wanapopelekwa huko makampuni, ni lazima Serikali hizi zijue sawa sawa ili kuepuka migongano ambayo kwa kweli inaweze ikajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kengele bado nisingependa inigongee, basi naomba pia Serikali ijielekeze kwenye barabara, mimi natambua juhudi kubwa za Serikali katika kujenga barabara. Lakini barabara nyingi zinajengwa chini ya viwango, kule Mbozi tuna barabara karibu nne za Mkoa, tuna barabara ya Ruanda, Iyula, Idiwiri, Nyimbili, *Mbozi Seco,* Mlowo, Igamba, Kamsamba, Igamba, Msangano, Zelezeta, Isansa, Ipoloto hadi Itaka. Lakini barabara hizi zinajengwa chini ya viwango, sitegemei kwa Wilaya inayolima kama mbozi barabara zake zinajengwa kila mwaka, hivi kwa nini Serikali isichukue uamuzi wa kuzijenga hata kwa kiwango cha changarawe nzuri. Kule Mbeya tuna kokoto zinazozalishwa na Kongorokware ambayo inamilikiwa na *TAZARA* pale Mbeya. Kwa nini tusizungumze na Mbozi pia kule kuna kokoto, kwa nini Serikali isiamue kutumia kokoto hizo ikazijenga hizo barabara walau ikapumzika kwa muda fulani ili kuzitengeneza hizi kila mwaka ambako mimi nafikiri kwa kweli tunatumia pesa nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Kamsamba mpakani na jimbo la Kwela, kuna daraja moja na hii barabara ya Mlowo, Igamba, Kamsamba ni ya muhimu sana katika uchumi wa Wilaya ya Mbozi. Lakini tunashindwa kuvuka kwenda jimbo la Kwela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWICHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza natoa salaam za pole kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kigamboni baada ya kupata ajali ya gari na kwa bahati mbaya watu watano walifariki pale pale na watatu wamefariki baadae. Kwa hiyo, naomba wazipokee salaam zangu za pole hizo na ujumbe rasmi nimetuma. *(Makofi)*

La pili, naomba kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Waziri wa Fedha kwa hotuba nzuri ambayo inamatumaini mazuri kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, naomba kuzungumzia barabara ya Kilwa, tunashukuru Serikali imejitahidi, suala hili limekuwa la muda mrefu lakini hatimaye juzi tulipata mfadhili na kwa nguvu za Serikali barabara hiyo inatarajiwa kujengwa ifikapo mwezi wa Desemba. Kwa hiyo, nawashukuru kwa dhati Serikali na kwa juhudi hizo. Lakini tuna tatizo katika barabara hizo.

Moja, suala la fidia la wananchi ambao wamevunjiwa nyumba zao kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo. Wananchi wa Temeke, wananchi Kigamboni wametutuma tuje

kulizungumze suala hili ili Serikali ianze kulifikiria tena kwa kuwa tayari imeshapata msaada sasa Serikali iongeze nguvu kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi ambao nyumba zao zimebomolewa, maskini, nyumba mtu alikuwa anaitegemea ni hiyo hiyo moja baada ya kuvunjwa sasa hivi wanahangaika na maisha. Kwa heshima na taadhima naomba Serikali, hili ilipokee, ilione kuwa ni suala muhimu na ilipe kipaumbele. Lakini pia kuna suala linasikitisha kidogo, kuna jumla ya wananchi 29 wao wanakaa Kongowe, Kata ya Kongowe kwa bahati mbaya nao wamekumbwa na kuvunjiwa kwa ajili ya kujengwa barabara hii ya Kilwa na watu hawa walihamia barabarani kwa ajili ya kufuata kijiji, wametolewa huko maporini kwenda barabarani kwa ajili ya mpango wa Serikali uliokuwepo kwa wakati huo. Lakini nao cha kusikitisha wameenda ofisi zote kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, wameenda Ofisi ya Waziri Mkuu, barua tele wameenda kwa Mheshimiwa John Malecela, Mheshimiwa Vita Kawawa, lakini mpaka leo nenda rudi hawajafanikiwa lolote.

La mwisho tuliambiwa kwamba tutafanyiwa mipango ili salaam hizo ziweze kufika kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuwafikiria chochote watu hawa 29. Kwa vile Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa, basi naomba kwa misingi kwamba watu hawa 29 waliohamishwa kutoka kwenye maeneo yao kuja barabarani kwa ajili ya kijiji na mpaka hati wanayo ya kijiji na nyaraka nyingine, naomba wafikiriwe. Mbaya zaidi barabara haifiki Kongowe na tayari wameshabomolewa, barabara imeishia Zakhem, Kata ya Charambe, kwa hiyo, machungu juu ya machungu, wamebomolewa barabara haifiki, sijui Serikali inasema nini kuhusu hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la MKUKUTA, suala hili ni zuri naziomba Wizara hizi mbili Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Wizara ya Fedha, waandae utaratibu maalum ambao utawezesha benki zote zilizopo Tanzania kutambua mpango huu. Ili wananchi watakapopata hati zao za kurasimishwa rasmi ardhi na nyumba wanapokwenda kuomba mikopo wasisumbuliwe, tunaomba utaratibu huo uwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ujenzi wa daraja la Kigamboni, ambalo limo kwenye Ilani ya Chama tawala lakini kwa bahati mbaya au sijui niseme bahati nzuri kwenye mpango wa Serikali Kuu haumo na huu ni mradi ambao utahitaji fedha nyingi za kutosha. Nilitegemea kwamba labda kwa mwaka huu wa mwanzo zitatengwa fedha kwa kuanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili.

Kwa hiyo, nimeingiwa na mashaka kidogo, naomba tupate maelezo ya kina, mkakati wa ujenzi wa daraja hilo la Kigamboni litakuwaje wananchi wa Kigamboni wamekipa Chama cha Mapinduzi kura nyingi wakitegemea ujenzi wa daraja hili, ilikuwa ni kishikio kikubwa sana. Hali kadhalika kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imezungumzia suala la kuvuna maliasili za bahari, kwa bahati mbaya kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango wala Fedha haukuelezwa mkakati wowote wa kuweza kuanza kuchuma, kuvuna rasilimali hizi za bahari na kuanzisha viwanda vya usindikaji wa samaki kwa ajili ya biashara za ndani na nje ya nchi kujiongezea mapato. *(Makofi)*

Naomba hili pia Serikali walione, kuna suala la *TASAF*, tunawapongeza sana *TASAF* kwa awamu yao ya kwanza wamefanya kazi vizuri lakini katika jimbo la Kigamboni, kuna mradi mmoja wa barabara ambao unatoka katika Kata ya Somangila kwenda Kata ya Kisarawe II, wamejenga barabara nzuri madaraja wameyaacha, sasa barabara hii pamoja na uzuri wake haiwezi kupitika, kwa sababu madaraja yameachwa. Sasa hili *TASAF* naomba walipokee na tupate majibu muafaka ili wananchi wa Kata ya Kisarawe II na Kata ya Somangila wajue mwelekeo ukoje, badala ya kwenda awamu ya pili. Kwenye *budget speech,* ya Mipango na Fedha halikuguswa kabisa suala la utamaduni na michezo, utamaduni na michezo hasa suala la michezo Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amelizungumza kutaka kuonyesha Tanzania sasa tunaelekea wapi kwenye suala la michezo. *(Makofi)*

Lakini bahati mbaya kwa sababu ni mkakati, humu haukutajwa, sasa mwelekeo huo tutakwenda vipi bila kuwemo kwenye mpango wa nchi. Naomba katika marekebisho makubwa yatakayofanywa, suala la michezo liangaliwe tulizungumza kwenye ilani yetu kuinua vipaji vya wanamichezo, tutainua vipi kama kwenye mipango haimo, ninaomba hili liangaliwe. *(Makofi)*

Kuna suala la mfuko wa utamaduni, ili kukuza utamaduni wetu lazima tuwe na mipango mizuri ya nchi, utamaduni kwenye mipango hii haikuangaliwa kabisa, tunasema sasa tunauwacha utamaduni wetu au tutauendeleza.

Naomba hilo pia liwekwe ndio maana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akaunda Wizara maalum kwa ajili ya kusimamia utamaduni, michezo na habari, kwa sababu ya uzito wake. Lakini kwenye mipango yote miwili *budget speech* zote mbili hazimo, nimefurahi kusikia kwamba kuna masuala ya uendelezaji ujenzi wa viwanja. Lakini haikutamka bayana wapi patajengwa, nilikuwa ninaomba kwamba kipaumbele kitolewe kwa ujenzi kwa uwanja wa kisasa wa ndege makao makuu yetu ya Serikali Dodoma. Dodoma inakuwa na nina hakika itakuwa ni kivutio kikubwa kwa Mataifa mbalimbali kujivuta kuhamia Dodoma, wakati wote wanajua tutafika wakati wote ninajua nitaondoka. Lakini mpaka sasa hivi hawana uhakika wa kufika hawana uhakika wa kuondoka ili ni tatizo lao. *(Makofi)*

Kwenye suala la uwezeshaji, kuna baadhi ya mikoa ina benki za wananchi wa mikoa hiyo, au wa Wilaya hizo, lakini Serikali haijaonyesha nguvu zozote za kuweza kusaidia benki hizo za wananchi kwa mfano sisi pale Dar es Salaam tunabenki ya wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam. Tunaomba Serikali nayo katika mipango itoe kipaumbele kusaidia benki hizi ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kuna suala la kuisaidia Zanzibar kiuchumi, katika hotuba yake Mheshimiwa Rais pale ya kufungua Bunge alizungumzia suala la kuisaidia Zanzibar kiuchumi. Lakini kama wenzangu wa awali walivyosema kwenye mpango huu wa Serikali, Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango, haijaonyesha nia yoyote ya kuisaidia Serikali ya Mapinduzi kiuchumi, sasa sijui wanangojea Mheshimiwa Rais atamke tena au vipi. Mheshimiwa Rais ametamka ilikuwa bado utekelezaji, tunaomba kwa heshima na

taadhima tuione Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwamba wenzetu wapo nyuma na tuwasaidie.

Kwa hiyo, nategemea kwamba mipango itafanywa ya kubainisha lipi na lipi litaweza kuwasaidia wenzetu wa Zanzibar ili waweze kuinuka katika hali duni yao ya uchumi. Uvuvi nilishauzungumzia huku nyuma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii ya bajeti iliyoko mbele yetu. Napenda kuwapongeza sana Mawaziri kwanza Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mbunge Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Bajeti tu imetoa majibu makubwa katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi na imeleta imani kubwa kwa wananchi wote Tanzania, lakini pia imeleta imani kubwa kwa wanawake, sijui kwa vile imesomwa na Waziri ambaye ni mwanamke au kwanini lakini wanawake wengi wamepata imani na bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu MKUKUTA, pamoja na pato la nchi yetu kufikia asilimia 6.8 lakini bado liko tatizo kubwa la wananchi wengi kutouelewa MKUKUTA na vile vile kutofahamu ni namna gani wanaweza wakashiriki katika utekelezaji wa malengo makubwa ya MKUKUTA.

Naiomba Serikali itengeneze programu maalum ya kuweza kuwahamasisha wananchi na kuwaeleza ni nini hasa malengo ya MKUKUTA na vile vile kwa namna gani wananchi wanaweza wakashiriki wao wenyewe moja kwa moja katika kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke hotuba ya Mheshimiwa Rais alipokuwa analihutubia Bunge lako Tukufu alituasa kwamba kwanza tuhakikishe kwamba tunaitoa Tanzania kwenye lindi la umaskini, lakini vile vile tuhakikishe ushiriki wa wananchi katika uchumi wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusiana na uwezeshaji wa wananchi, naishukuru Serikali kwa nia ya kupenda kuwawezesha wananchi wa Tanzania hasa hasa kupitia vyama vya *SACCOS* na *SACCAS* lakini vile vile kujaribu kuwawezesha katika vikundi vyao vya uzalishaji mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo katika vyama hivi moja nawapongeza sana Wabunge ambao wamevianzisha vyama hivi kwa jitihada zao wao wenyewe kama Wabunge, vyama hivi vinatakiwa vihamasishwe na vianzishwe na Maafisa wetu Ushirika

na Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo katika Halmashauri zetu lakini kwa masikitiko makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Idara hizi mbili hazina *OC* katika Halmashauri na hivi inapelekea Maafisa Maendeleo na Maafisa Ushirika kushindwa kufanya kazi zao za msingi na kushindwa kufika vijijini kuwahamasisha wananchi waweze kujiunga na vikundi vya *SACCOS* na *SACCAS* ili waweze kushiriki katika kujenga uchumi, naiomba Serikali iangalie idara hizi mbili ili ziweze kufanya kazi zao ka mujibu wa kanuni.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie katika suala hilo hilo la uwezeshaji wa wananchi katika upande wa *Micro Finance*. Bado nchi yetu haijajikita vizuri kwenye suala la *Micro Finance* na vile vile tunaona ya kwamba katika sekta ya fedha, mabenki mengi ni ya wageni kutoka nje, benki za wananchi zinafikia pengine idadi ya benki sita tu pengine katika mikoa ya Iringa, Ruvuma, Kilimanjaro na Dar es Salaam lakini katika Wilaya nyingi hakuna Benki za Wananchi. Mimi naamini katika Benki za Wananchi na ninawaomba wananchi wengi tujiunge katika vikundi vidogo vidogo na hatimaye tufungue sasa Benki zetu ili tuweze kuumiliki uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu uwezeshwaji wa wanawake, lakini pia katika nafasi hii napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwanza kwa kutambua uwezo mkubwa walionao wanawake na hivi kuwapa nafasi. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais wanawake hawa hawatamwangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo katika vyombo vya maamuzi tunashukuru Serikali imeangalia sana uwezeshwaji wa wanawake tuna tatizo kubwa katika uwezeshwaji wa wanawake kiuchumi. Bado wanawake wengi wanapenda kufanya biashara na wanapenda kuwa wajasiriamali bado hawajaweza kupata nafasi na kuhudhuria maonyesho mbalimbali ndani ya nchi na nje ya nchi ili waweze kuhimili ushindani wa soko ambao ni mkubwa sana sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia katika uwezeshaji wa wanawake lakini pia katika masuala mazima ya kijamii. Lipo tatizo kubwa la vifo vya wanawake katika uzazi, tatizo hili ni kubwa na naiomba Serikali iangalie tatizo hilo kwa sababu kama tusipokuwa makini basi wanawake wengi watakuwa wanaendelea kufa kutokana na uzazi, takwimu zinaonyesha kwamba inakadiriwa wanawake sita katika kila wanawake 1,000 wanaojifungua hufa kwa ajili ya uzazi. Tatizo hili ni kubwa, kwa hiyo, naiomba Wizara ya Afya ikishirikiana na Serikali kwa ujumla iangalie na itupe mkakati maalum wa kupunguza vifo vya wanawake katika uzazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kama Serikali yetu itakuwa na nia thabiti ya kuwawezesha wanawake katika siasa, uchumi na jamii maana yake itakuwa imeliwezesha Taifa, ninaamini ya kwamba wote tunakubali kwamba ukimwezesha mwanamke mmoja basi utakuwa umeliwezesha Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kupongeza sana asasi zisizo za Kiserikali ambazo zinajitahidi sana katika kushughulikia masuala mazima ya kuangalia kwamba nchi yetu

inaendeshwa katika usawa wa kijinsia na hapa nitamke wazi kwamba tunawashukuru sana viongozi na wanachama wa *TWPG* hasa *AID Foundation, SUNNY Tanzania, TGNP* na mashirika mengine kwa kushirikiana na Serikali katika kuwawezesha wanawake.

Mheshimiwa Spika, lakini naiomba Serikali yetu katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nina wasiwasi na bajeti yao na kwa vile hawajaisoma lakini uzoefu unaonyesha kwamba bajeti ya Wizara hii mara zote inakuwa ni ngumu na inakuwa ni ndogo sana. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali iangalie kwa kweli mfumo wa bajeti hii, mimi sijui ni nani anayeanza kuiandaa bajeti hii lakini kama ni watu kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa nini wanaibana mno hii bajeti ya Wizara hii? Bila kuandaa raslimali watu nchi yetu itashindwa kuendelea kwa sababu kimsingi ni lazima watu waandaliwe na watu wa idara ya maendeleo ya jamii ndiyo wenye kazi kubwa ya kwenda kuhamasisha wananchi, wakulima, vikundi vya uzalishaji mali, kwa hiyo, naomba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto bajeti yake iongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Madiwani. Kwanza nawapongeza sana Madiwani wote Tanzania kwa kazi nzuri ya kusimamia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, wote tutakubaliana kwamba Madiwani wanafanya kazi nzuri na vile vile wanasaidia sana katika kusimamia miradi mbalimbali.Wote tumeona jinsi Madiwani walivyosimamia ujenzi wa madarasa, barabara na kazi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali Kuu ishirikiane na Serikali za Mitaa katika kuboresha maslahi ya Madiwani ili waweze kufanya kazi zao kwa *speed* na viwango vinavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niishukuru sana kwa Serikali kupeleka madaraka makubwa katika Halmashauri zetu na vile vile kupeleka pesa nyingi katika Halmashauri, pesa hizi kama zitakuwa hazijapewa usimamizi maalum zitaleta tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kilimo. Siasa ya Mkoa wa Ruvuma ni kilimo na kilimo kwa Mkoa wa Ruvuma ni pembejeo kwa hiyo ninakuomba utaratibu wa ruzuku ya pembejeo sasa hivi haumnufaishi mkulima wa Ruvuma. Ninaomba wananchi wa Ruvuma na wananchi wote kwa ujumla waangalie namna gani tunaweza tukashirikiana na Serikali ili kuangalia utaratibu wa ruzuku uweze kwenda vizuri na vilevile kitengo chetu cha *TFC* kitumike vizuri *SGR* itumike vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi huko Songea kuna matatizo makubwa ya ununuzi wa mazao, wanunuzi huria wananunua mazao kwa vipimo wanavyovitaka wao, wananunua mazao kwa vipimo kama jumla, sijui kuna lumbesa, kangomba na hivi vipimo vyote vinawanyonya wananchi.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kutamka wazi na bayana kwamba kuna mikoa sita Tanzania haijaendelezwa kimiundombinu ukiwemo Mkoa wa Ruvuma. Nina amini ya kwamba kauli hii iliyotamkwa na

Mheshimiwa Rais na imerudiwa na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, kwenye hotuba yake ukurasa wa 41 itatekelezwa katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida nami napenda kushukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na wale wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii ambayo ni bajeti nzuri yenye matumaini mazuri kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni nzuri endapo itatumika jinsi ilivyopangwa, kwa uaminifu mkubwa sana. Hivyo napenda kuzungumzia masuala muhimu yafuatayo kwa kusisitiza Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nikianza na kilimo. Bajeti imezungumzia suala la kilimo lakini bado sijaona itie mkazo hasa kwa upande wa vyuo vya kilimo, vyuo vyote vimefungwa. Tukienda kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ina vyuo, inapofundisha walimu inawasambaza nchi nzima, ukienda upande wa Afya pia na wenyewe wana vyuo vyao wanafundisha wataalam na kuwasambaza lakini tunapokuja kwenye upande wa kilimo vyuo vyote vimefungwa sasa najiuliza kilimo hiki ni kweli kitaendelea? Wataalam endapo itakuwa hakuna tunapozungumzia suala la umwagiliaji, uvunaji wa maji ya mvua hakuna wataalam sana sana ni wale wanaotoka vyuo vikuu sasa sijui hawa kama kweli wanaweza wakakidhi haja ya wakulima wote, kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali iangalie sana suala la vyuo vya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inapozungumziwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji hayo mazingira mazuri sina hakika kama yamebainishwa kwa sababu labda niseme kwa upande wa mkoa wa Singida. Mkoa wa Singida ni mkoa ambao una wafugaji wengi sana, ufugaji wa kuku, kilimo cha alizeti, ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kadhalika. Mazingira hayo mazuri sina hakika kama yamebainishwa kwa sababu tunapotaka kuwavutia wawekezaji ni lazima miundombinu iboreshwe. Ni mwekezaji gani anayeweza kusafiri saa 12 kufika Mkoa wa Singida ili aje aangalie ni suala gani ambalo litamvutia kwa ajili ya kuwekeza kama ni kiwanda au ni vinginevyo, ni lazima barabara iboreshwe ili kuvutia wawekezaji.

Kuna wawekezaji wengine anaona haweza kusafiri saa 12 anahitaji atumie usafiri wa ndege lakini Mkoa wa Singida hauna uwanja wa ndege ulio bora, sasa tunaposema uwekezaji sifahamu kuwa Singida umewekwa upande gani na Mkoa wa Singida unahitaji uwekezaji kwa hali ya juu kwa sababu wananchi kule sisi ni wafugani wa kuku huwezi kutoa kuku kutoka Singida kwenda Dar es Salaam kwa barabara kama ile kwa hiyo, wananchi wanakuwa wanapata shida kwa suala la soko la kuku. Lakini endapo mazingira ni mazuri nadhani tunaweza tukapata kiwanda kwa ajili ya *sausage* au usindikaji wa nyama za kuku na wananchi wa Mkoa wa Singida wakafaidika, kwa hiyo, naomba suala

hili litiliwe mkazo hasa la miundombinu na kuweka mazingira mazuri kuwavutia wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nizungumzie suala la miundombinu, japokuwa wazungumzaji waliopita wameshaongea nami sitachoka kuzungumzia. Tanzania hii sasa hivi tunayosema sasa hivi tunakwenda kwa kasi, sielewi kasi hii inaanzia wapi na inashia wapi, kwa karne hii mikoa bado haijaunganishwa barabara kwa miundombinu ya barabara ukichukulia Mkoa wa Singida ukitaka kwenda Dodoma unapita kwa barabara ya vumbi kwa kusuasua, ukitaka kwenda Babati, Manyara barabara ni mbovu, ukitaka kwenda Mkoa wa Tabora barabara ni mbovu yaani kwa karne hii bado mikoa yetu haijaunganishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa usemi wa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, Serikali iangalie vizuri suala la miundombinu kuunganisha mikoa hii kwa barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ukienda kwenye mikoa mingine unakuta wao wana barabara hata za kuunganisha wilaya yaani barabara za lami ninazungumzia barabara za lami, mikoa mingine inaunganishwa kwa barabara za lami lakini ukifika Singida ni vumbi. Naomba uwiano ufanyike barabara isiwe ni baadhi ya mikoa tu kuwe na uwiano wa kutosha kati ya mikoa yote kama ni barabara za kuunganisha mikoa basi tuunganishe mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia barabara inayotoka Mkoa wa Singida kwenda Wilaya ya Manyoni. Barabara hii Serikali iliingia mkataba na Wachina lakini mkataba huu umekuwa wa kusuasua, haueleweki, mkandarasi aliyepo sasa anazungumzia kwamba barabara hii ataijenga kwa kilometa 63 lakini awali ilikuwa ni kilometa 118, kilometa 63 inaishia Isuna na anasema kwamba ataimaliza itakapofika mwezi Machi tarehe 22, mara aseme mwezi wa nne au wa tano mwaka 2007.

Naomba Serikali ituhakikishie wananchi wa mkoa wa Singida kwamba kwanza barabara hii ya kilometa 63 je, ni kweli itafikia muda huo na itakuwa imekwisha na kilometa nyingine zinazobaki kuna utaratibu gani? Naomba suala hili mkoa wa Singida usiendelee kuchezewa, barabara ya Mkoa wa Singida ni sawa na mshipa wa damu unaopeleka damu kwenye moyo. Magari yanayotoka Dar es Salaam yanabeba mizigo kupeleka nchi za jirani yanapita barabara ya Mkoa wa Singida lakini barabara ile imekuwa ikichezewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kuzungumzia suala la afya. Suala la afya pamoja na kwamba mzungumzaji aliyesema muda uliopita amezungumzia suala la akina mama, labda mimi nianze na zahanati. Wananchi wamejitahidi kwa kushirikiana na *TASAF*, wamejenga zahanati lakini zahanati hizi hazina waganga sasa je, majengo haya yabakie kuwa viota vya ndege?

Kwa hiyo, naomba Serikali ipeleke waganga kwenye zahanati hizi kutokuwakatisha tamaa wananchi maana hizo ni nguvu zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote Mkoa wa Singida hauna Daktari Bingwa kwa muda mrefu sana, Serikali imekuwa ikiangalia na kujibu majibu ya kwenye maandishi na kujibu majibu ya mdomo lakini haitekelezi kwa hiyo, naomba Mkoa wa Singida upatiwe Daktari Bingwa angalau mmoja wa kukidhi mahitaji ya magonjwa ya akinamama.

Mheshimiwa Spika, bado kuna matatizo kwa madaktari, madaktari wetu wanasomeshwa na Serikali yetu lakini wanakimbia wanakwenda nchi za nje kufuata maslahi. Naomba Serikali iweke mkazo katika kuwa *retain* kwa kuwapa maslahi mazuri. Madaktari wanaotoka nchi za nje wanapewa mishahara mizuri huenda hata utaalam hauwazidi wale wa kwetu kwa hiyo ninaomba Serikali iache mtindo wa kuwathamini waganga na madaktari wanaotoka nchi za nje na kuwapuuza madaktari wetu ili waendelee kubaki hapa nchini waweze kuhudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu Elimu ya Juu yaani Sayansi na Teknolojia sielewi Wizara hii imepewa fungu kiasi gani lakini nchi yoyote iliyoendelea imeendelea kutokana na kusomesha watu wake kwa wingi hivyo ninaiomba Serikali iitazame kwa jicho la pekee Wizara hii, iipangie fungu ambalo linawezesha kuwasomesha vijana wetu kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya.

Sasa hivi tukizungumizia Bodi ya Mikopo bado kuna malalamiko mengi na Wizara hii imesema kwamba wale vijana wanaotaka kupata mikopo watalipiwa kwa asilimia 60 na 40 ajilipie mwenyewe. Je tutafika tunapokwenda? Kama Wizara hii haitatengewa fungu la kutosha tutakuwa tunacheza makida makida, hatutaendelea. Hivyo naomba Wizara hii itengewe fungu la kutosha na wale vijana ambao wameshapata mkopo kwa mwaka wa kwanza leo unamwambia utampa asilimia 60 ile 40 aitoe wapi? Aache? Atakapoacha ile uliyomlipia mwaka wa kwanza ailipaje na wakati hakuendelea na elimu hiyo?

Bado tunazungumzia Chuo Kikuu kipya ambacho kinatarajiwa kujengwa hapa Dodoma ni lazima Wizara hii iangaliwe Vyuo Vikuu vya hapa nchini ni vichache wataalam pia ni wachache na Chuo Kikuu kinaongezeka ni lazima wasomeshwe wataalam wa kuja kufundisha hao wanafunzi 40,000 hatuwezi kusema kwamba tutategemea kuazima kutoka nje pesa ni nyingi sana za kuwalipa wataalam kutoka nje. Kwa hiyo, Wizara hii iangaliwe kwa makini sana na kwa undani ili nchi yetu iweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, naongea haraka haraka kwa sababu naona muda unanitupa mkono. Mahakamani zetu sasa hivi kuna uozo kesi hazitoki mle sielewi kuna matatizo gani, kesi miaka 10 ushahidi haujapatikana ni ushahidi gani? Eti majaji wachache, kama ni wachache wale waliopo wamefanya kwa kiwango gani? Hakimu anafika mahakamani anaandika tu naahirisha tarehe, naahirisha tarehe halafu anatoka anaendelea na shughuli zake. Ninaomba Serikali itupie macho mahakama zetu ili kuleta maisha mazuri kwa Watanzania wenye hatia wahukumiwe na wasio na hati wakae huru, ninawaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu janga la UKIMWI limekuwa likizungumziwa mijini lakini vijijini eti kuna kamati sijui ndogo ndogo na kadhalika, zile kamati hata hawaelewi lolote, pesa zilizotengwa ziende vijijini waache kukaa maofisini watoke waende vijijini wakawaelimishe watu ili waondokane na imani za kwamba fulani kalogwa kwa sababu hawaelewi. Kwa hiyo, naomba zile pesa zilizotengwa waende vijijini wakawaelimishe watu kuhusu janga la UKIMWI na dawa zipelekwe vijijini viwekwe vituo huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la njaa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hizi mada mbili za hotuba ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Awali naomba nianze kutoa pongezi kwa Mawaziri wote wawili kwa hotuba nzuri walizowasilisha hapa, vile vile niipongeze Serikali kwa ujumla wake kwa mikakati ambayo imeainishwa hasa kwenye bajeti kwa sababu inalenga hasa kutatua matatizo ya msingi ya wananchi na hasa walio maskini.

Mheshimiwa Spika, ningependa tu kuzungumzia kwenye maeneo machache ambayo nafikiri yanafaa kuboreshwa zaidi hasa kwenye bajeti au kwenye hotuba ya Mheshimiwa Zakia Meghji. Kwanza nizungumzie upande wa matumizi. Kama wengi waliotangulia kusema wamesema kwamba nchi yetu ni kubwa na matatizo yake ni mengi na pia vipaumbele vimeainishwa kwenye hotuba ya Waziri wa Mipango kisekta, sasa hapa nilifikiri ni vizuri tukaweka pia vipaumbele kwenye maeneo ambayo yanahitaji kutizamwa kwa mtizamo wa kipekee na hapa ninazungumzia hasa sura ya Mkoa wa Shinyanga kwenye maeneo yaliyo mengi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitaanza na elimu. Mkoa wa Shinyanga una matatizo makubwa ya elimu Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi na pia Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, naye amefika. Kwa ujumla mkoa wetu una matatizo makubwa ya elimu na matatizo haya mimi naamini hayatokani na wananchi wenyewe, lakini yanatokana pengine na msukumo kidogo ambao wananchi wanakuwa wanapata kutoka kwenye Serikali.

Mheshimiwa Spika, kinachojitokeza ni madhara yanayotokana na kutokuwepo kwa elimu katika maeneo haya, nitakuja kuelezea mambo mengi baadaye lakini nizungumzie tu kwamba sasa hivi Mkoa wa Shinyanga *off course* na mkoa wa Mwanza una matatizo ya mauaji ya vikongwe ambao msingi wake mkubwa ni ujinga maana yake ni kwamba kutokuwa na elimu kwa mkoa wetu kunasababisha maafa pia.

Sasa ili kukabiliana na tatizo hili pamoja na elimu ambayo tutakuwa tunaitoa katika mazungumzo ya kawaida kwenye mikutano ya hadhara lakini bado ninafikiria kuboresha elimu hasa ya Sekondari ni jambo la msingi sana. Sasa kwa kuwa jambo hili linajulikana nilifikiri ni vizuri likaonekana waziwazi kwenye bajeti, uwepo mkakati

maalumu wa kusaidia kuboresha elimu mkoa wa Shinyanga, ni kweli tumehimiza wananchi wetu wajenge shule za sekondari kila kata na kama ilivyokuwa kwenye sura ya wilaya ya Geita kwenye swali lililoulizwa hapa juzi Wilaya ya Kahama pia imejitahidi sana karibia kila kata ina majengo ya madaraka ya sekondari, Mheshimiwa Waziri alifika ameona kila kata shule zimeanzishwa kinachokosekana ni *input* ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri kwamba majengo yajengwe imara, sawa. Yanatakiwa yawe imara lakini yaishe ili watoto wasome sasa ningeomba Serikali iweke mkakati wananchi wamechangia maboma yamekamilika sehemu zilizo nyingi Serikali ilete pesa na yenyewe itoe mchango wake wananchi wamechangia sisi wenyewe tumechangia na mimi mwenyewe nimechangia kwenye baadhi ya shule nyingi tu kama mtu binafsi sasa ningependa kuomba Serikali iweke nguvu kwenye hilo eneo.

Ninazungumzia Serikali hasa kwa sababu sehemu kubwa ya mapato ambayo tumekuwa tukiyapata yalikuwa hasa yakitegemea kwenye kodi au makato ya mazao, tulikuwa na ushuru wa Pamba, Tumbaku, ambao kama mlivyosikia kwenye jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, alipojibu swali la Mbunge wa Sumve kwamba makato kwenye mazao yamefuta maana yake ni kwamba hata mfuko wetu wa elimu wa mkoa wa Shinyanga kwa sasa hivi hautaweza kukusanya makato kutoka kwa wakulima maana yake ni kwamba itabidi tutafute namna ya kukusanya moja kwa moja kutoka kwa mtu mmoja mmoja ambayo kwanza utekelezaji wake ni mgumu lakini nashukuru jibu lililotolewa na Mheshimiwa Chibulunje hapa alisema kwamba sasa hivi itabidi tutegemee zaidi MMEM na MMES na MMEM na MMES maana yake ni Serikali Kuu. Kwa hiyo, naomba tu kwa hilo Serikali itusaidie kuliangalia kwa makini.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limezungumziwa kwa ujumla ni mawasiliano na hasa ni mawasiliano ya barabara. Mkoa wa Shinyanga uko katika Kanda ambayo ina matatizo makubwa ya mawasiliano, ni mkoa ambao unategemea sana Reli ya Kati, ni mkoa ambao unakuwa *affected* sana na kutokuwepo barabara ambayo msemaji aliyetangulia kusema amezungumzia barabara inayopita Mkoa wa Singida, sasa hapa nilikuwa ninaomba jamani tuweke vipaumbele.

Kwanza yale majibu ya ujumla kila swali linaloulizwa kuhusu barabara kwamba upembuzi yakinifu unaendelea na kadhalika mimi nafikiri ni vizuri tukafika mahali tukawa tunasema kwamba barabara yako Mheshimiwa Mbunge haitatengenezwa mpaka barabara ya kwenda kwenye Mikoa imekamilika ili tukamilishe *Trunk Roads* mikoa yote iungane kwa barabara za lami halafu upembuzi yakinifu wa hizi barabara nyingine ambazo zinajitokeza uendelee. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tuweke kipaumbele Mkoa wa Mwanza ufikike kwa lami kutoka Dodoma mapema iwezekanavyo lakini pia mkombozi wetu Reli ya Kati wamelizungumzia wasemaji waliotangulia naomba tu kusisitiza tafadhali sana hii ni roho ya wakazi wa Kanda ya Magharibi na kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia nizungumzie matatizo ya upande wa wafugaji. Wafugaji wetu wamekuwa kwa kweli katika sura ya sasa wamekuwa ni watu ambao hawana raha katikanchi yao, wakisikiliza kauli za Serikali, wakisikiliza hoja za

Wabunge wanavyochangia hapa wamekuwa ni wakimbizi labda kwa kuwa hawapo kwenye *Geneva Convention* wanafanywa kwamba wao hawana haki, mimi nafikiri siyo sahihi nasema hivyo kwa maana moja kuna wafugaji wametoka Mkoa wa Shinyanga na wengine wametoka mikoa mingine ya wafugaji na mimi nazungumzia hasa wa mkoa wa Shinyanga wako huko Ihefu na ni ndugu zetu tunawajua wanatupigia simu kwamba Mheshimiwa haya tumeambiwa tutoke huku lakini hata ile *route* tu ya kutoka huku kurudi Shinyanga haipo, ukiambiwa utoke hapo Ihefu hujaambiwa uende wapi lakini pia hujaambiwa upitie wapi. Kwa hiyo, hawana pa kwenda wala hawana pa kupita wilaya zote zinazozunguka eneo lile wanazuia sasa ni vizuri sana tukawasaidia na kwa bahati nzuri kaka yangu Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, yupo na nilikuwa naomba sana asitoke kabla sijazungumza. *(Makofi)*

Naomba Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Wizara hii ndugu yangu na Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, naomba Wizara ya Maendeleo ya Mifugo isiwe Wizara ya maangamizi ya Mifugo tafadhalini. Kwenye *cabinet* Waziri wa Mazingira anazungumzia Ihefu na wewe simama kidete zungumzia wafugaji hawa tutengeneze mkakati. Ni lazima tuwasaidie hawa watu hatuwezi tu kuishia kuwalaumu, kuna wakati niliuliza swali la nyongeza kwamba wafugaji wetu mifugo yao imekufa. Kuna wafugaji wa namna mbili kuna wengine ambao ni wafugaji kimila kwamba mifugo ndiyo utajiri wake lakini wafugaji wengine wanafuga kidogo na wanalima kidogo. Lakini hawa wafugaji wadogo wanaolima na kufuga ndiyo hasa wamekuwa *affected* na baa la ukame yaani mifugo imekufa ambao ndiyo walikuwa wanatumia kwa ajili ya kulimia, sasa nikauliza kwamba wafugaji hawa watasaidiwaje? Jibu lililotoka kwa kweli lilikuwa siyo jibu muafaka kwamba tuliwaambia wapunguze mifugo kwa hiyo kwa sasa hivi tunawaomba wapunguze mifugo, mifugo yenyewe iliyokuwepo ni watano kwa ajili ya kulimia nao wamekufa sasa wapunguze wangapi?

Kwa hiyo, nilifikiri ni vizuri tusiwe tunatoa majibu ya jumla, suala la wafugaji lina sura tofauti lakini tunahitaji kuweka mkakati wa kiserikali wa kuwasaidia hawa watu.

Kuna wale ambao ni wafugaji wakubwa, wanafuga kama sehemu ya mila, kuna wengine akiwa na ng’ombe wengi ni utajiri, ukimwambia auze wale ng’ombe aanzishe biashara ya *guest house* hata kiswahili hajui ataweza kweli kuandika *receipts* na *invoice?* Biashara yake ni ng’ombe m-*transform* pole pole huwezi tu ukamwambia punguza mifugo, atakujibu nipunguze nifanye nini? Tuchukue muda wa kuwaelimisha hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia upande wa tatizo la njaa na mikakati ya kuboresha kilimo, nitazungumzia hili tatizo ambalo limejitokeza hivi karibuni. Ningeomba tu kusema kwa kifupi kwa sababu jambo hili limeshatokea, nini tumejifunza. Kwanza tunatakiwa kuweka mikakati ya kuboresha kilimo sisi wenyewe tumejifunza kwamba kuweka *crash programme* wakati tatizo limetokea haisaidii. Kwa mfano dhahiri, tunajua kwa kiasi kikubwa sana misamaha tuliyoitoa kwa wanunuaji wa mahindi na mchele haujajionyesha kwenye bei halisi ya mazao haya kwenye soko na hata mimi ninapata wasiwasi aidha, kuna kutokujua au hatukuwa tumeweka mkakati maalum

kwamba *okey* wewe utaagiza tani fulani za mahindi utayasafirishaje kuyafikia kwa mnunuzi wa mwisho na bei iwe kiasi gani. Kwa sababu tumempa msamaha wa kodi ni lazima auze kwenye *agree price.* Wao wanaleta wanauza kwenye bei ya soko ndiyo maana tumewapa msahama bei wakati ule ilikuwa kilo shilingi 300/= sasa hivi kwenye shilingi 500/=, unga ulikuwa shilingi 500/= sasa hivi ni shilingi 800/= sasa haya mahindi tuliyosema wanaleta export trading watashusha bei ya muda wapi?

Kwa hiyo, *these are business men* wanataka faida na kukitokea *loophole* wana *utilize and that is what happen.* Kwa hiyo, nilikuwa naomba tusiwe na *crash programme,* tuweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba tunajitosheleza kwa chakula na katika kufanya hivyo ni lazima kila eneo liboreshewe kilimo chake. Watu wa mkoa wa Shinyanga pamoja na kwamba tunapata matatizo ya ukame mara kwa mara lakini tunaweza tukalima mtama. Sasa nilifikiri ni vizuri tuhimize kilimo cha mazao yanayohimili ukame kwenye maeneo hayo na tunaweza tukajitosheleza kwa chakula. Kwa hiyo, pamoja na kuhimiza hayo nilikuwa naomba Serikali pia ijaribu kujiwekea mikakati ya muda mrefu tusijikute tupo kwenye kona kila wakati kwamba hatuna option zaidi ya kuchukua *the very difficult option* kwa wakati huo na kwa sababu tumeshajifunza ninaamini kwamba tatizo hili halitajitokeza siku za hapo usoni.

Mheshimiwa Spika, pengine ningependa kuzungumzia kwa haraka haraka kuhusu Mapato ya Serikali. Kwa ujumla mimi ningependa kuwabeza *TRA* kufikia malengo haimaanishi kwamba umefanya vizuri, kufikia malengo kwa miaka mitatu mfululizo maana yake malengo yenyewe ndiyo yana kasoro, huwezi uka *over perform three years consecutively* kunatokea matatizo ya kawaida ya kiutendaji ambayo yangefanya kuonekane kwamba tumeshindwa kufikia malengo kwa sababu kumetokea njaa na hali mbaya ya hewa lakini tumevuka malengo, kuna matatizo katika malengo.

Mheshimiwa Spika, Waziri ningeomba nikushauri, kwanza kuna maeneo mengi ambayo tungeweza kuboresha kwanza ni wigo wa kodi unaweza ukapanuliwa zaidi, sekta isiyo rasmi haijaingizwa katika wigo wa kodi vizuri kuna watu wengi tu wanafanya shughuli zao hawalipi kodi, tumeanzisha utaratibu wa *TIN,* lakini *TIN are useless numbers* mtu mwenye *TIN* ni watu wangapi wanafuatilia kuhakikisha kwamba wanalipa kodi?*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaolipa kodi ambao sasa hivi imebaki ni *soft target* ni wale waajiriwa wanalipa kwa mtindo wa *Pay As You Earn (PAYE)* ambao wako kwenye *pay roll*. Lakini wapo wengi ambao hawapo kwenye *pay roll* na pia kuna *secondary employment* ambapo pato lake halitozwi kodi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu wa mawazo kwa Wizara zote mbili ambazo zimetolewa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba wananchi wangu wa Jimbo la Siha kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana ambayo imekuwa inafanyika toka utawala wa Awamu ya Nne uanze. *(Makofi)*

Mimi nilipokuwa naangalia hotuba hizi sikuanzia hapo tu. Tulipata majanga hapa ya chakula tukaiona Serikali iko *on top of business* nilimwona Mheshimiwa Rais wa Nchi hii anakimbia, nilimwona Mheshimiwa Waziri Mkuu anakimbia na Watanzania wakapata *assurance* kwamba hakuna tatizo la chakula na kama tunavyoona tumekwenda vizuri sana. Napenda kuipongeza Serikali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nimetoka kidogo kwenda kuzika mtoto wa Mwenyekiti wetu Mungu amweke mahali pema peponi. Lakini nikakimbia nije nikawahi hotuba zote mbili na bahati nzuri nikabahatika.

Mheshimiwa Spika, nilimuaga Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kazi hii iliyofanyika hapa kwa watu ambao tunaanza ni kazi nzuri. Hizi *data* wanazozisemwa kwamba hazimo humu ndani zimo, kuna vitabu vingine vimetolewa hapa na vingine tumevikuta kwenye pigeon hall. Hizi *data* zote zipo Serikali imeandaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa watu ambao tunatoka kwenye *background* hii tuliyotokana nayo kwa kweli Serikali imejitahidi na *it is my judgement as Members of Parliament* na hii nazungumza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha. Hotuba zote mbili ni nzuri, Bajeti ya Wizara ya Fedha ni nzuri na Mipango ni mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapa nirudi nyuma nizungumze mimi nilipokuwa naangalia humu ndani nilikuwa naangalia kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inatekelezwa. Maoni yangu naona inatekelezwa kwa sababu yote yaliyoahidiwa yamo humu ndani. Hawezi mtu akaniambia kwamba hapa hakuna kitu. Tunaambiwa kwamba ruzuku ya mbolea itaongezeka, wananchi wangu wanalima migomba, kahawa, mahindi, maharage na mimi nasema *this is good*. Unaniambia hapa kwamba umeondoa kodi ya mafuta ya taa, najua wananchi wangu wanaotumia koroboi kule nyumbani watapata nafuu, unasema hapa mishahara imeongezeka kutoka bilioni 640 inakwenda mpaka kwenye trilioni sijui na milioni 4. Halafu mimi niseme kwamba hii hotuba hakuna kitu. Nasema hii kazi ni nzuri. Wananchi wangu wale ambao nimepata nafasi ya kuzungumza nao wameniambia ni kazi nzuri na pale penye matatizo tutaonyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mipango ni *component* ya kijamaa siyo *component* ya kibepari. Nchi za kibepari hazipangi, wanaopanga ni wajamaa na ujamaa umezungumzwa ndani ya Katiba ya nchi hii. Nchi hii Tanzania Waheshimiwa Wabunge tuliomo humu ndani tusipozungumza habari ya ujamaa watu watakufa.

Mimi nimeona ujamaa unazungumzwa hapa. Nchi za kijamaa, njia kuu za uchumi zinakuwa mikononi mwa umma. Katika nchi za kibepari hawapangi, wanapanga katika *Enterprise level*, Shirika moja moja hivi ndiyo linapanga. Inaongozwa kwa sheria ya utashi na urari, kwa sheria ya mashindano na sheria ya thamani ndizo zinazotawala

pale na nguvu za soko ndizo zinazofanya kazi. Ile ya kwanza ya ujamaa, heshima yake kubwa ni kwamba watu wanatatua matatizo kwa njia ya haki na usawa, ndiyo heshima yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ya pili, watu wote wanahusishwa katika uzalishaji kama ni Billgets naye anashiriki katika *capitalism*. Tatizo lake mkija kwenye kugawana ndiyo unaambiwa kakaa pembeni mtu mmoja anachukua. Lakini heshima yake kubwa ya *capitalism* na hapa naomba nim-*quote* Marx, kwa sababu Marx alisema: "*One good things about capitalism it develops the level of the productive process,*" mwisho wa kunukuu. Ndiyo moja kubwa anayosema Marx. Heshima yake kubwa ni hiyo. Kwa sababu humu ndani watu wanasema ooh, tunajenga ujamaa, ooh, tunajenga ubepari, ooh, tunajenga nini. Hii yote iliyopo ni mielekeo. Hakuna ujamaa hapa wala hakuna ubepari hapa. Kuna watu wanazungumza habari ya *Blind Markets Economy* hii nayo ina *debate* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inayofanyika katika *developing countries* ni *basic contradiction,* iliyopo hapa ni kati *labour* na *the level of productive process* ndiyo maana watu wanalima na jembe la mkono, ndiyo maana umaskini upo, ndiyo maana mnaleta MKUKUTA mnaona hatwendi. Unakaa hapa, nitatoa mfano, unasema unataka kumleta *strategic investor*, unataka akuletee mtaji, akuletee teknolojia ya kisasa, akuletee ajira, akuletee *government revenue* mambo manne. Unaamka unamleta hapa unamwambia umeme utatolewa kwa mgao kuanzia saa 12.00 asubuhi mpaka saa 12.00 jioni. Katika *developing countries* nisizungumzie nchi yangu ya Tanzania. Kilicho hapa siyo ujamaa wala siyo ubepari. Hiki kinachoendelea huku kinaitwa shughuli ni shughuli, zinaitwa harakati. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuwa *very clear* kuhusu suala la *theory,* kama hatuna *theory* ambayo iko *clear* katika mambo tunayofanya maana yake tunajifanyia hivi hivi halafu tutakuwa hatuendi. Ule mfumo wa ubepari tunaotaka kazi yake ni kutafuta kitu kinachoitwa faida kibao. Nataka kusema nini hapa *issue* ya umeme katika nchi hii ni *issue* ya Serikali. Ukimwambia hapa *private sector* isimamie suala la umeme wanakaa pembeni wanaogopa kwa sababu wana *allegie* na kitu kinachoitwa hasara. Ni lazima useme na umuulize David Ricado, mchukue Rodkez, tuchukue akina Adam Smith, nende kasome *developed nations* mahali popote ambapo panahitaji *huge investment* ni lazima Serikali iingilie kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, baba, hapa hatuna jinsi, *issue* ya umeme katika nchi ukiiachia *private sector* hapa nakwambia hatufiki. *Issue* ya reli ambayo mpaka sasa tunazungumza. Waingereza wale hawafikii mahali wakasema ondoa reli hii. Reli inakuwa ni mali ya Serikali, unakodishwa biashara mle ndani, ndizo unakabidhi wale *private sector* wanafanya pale. Kwa hiyo, hapa hatuwezi kuwaachia kufanya hivyo na ndiyo maana namuunga mkono Mheshimiwa Waziri wa Fedha anapozungumza habari ya bilioni 200 kwa ajili ya *issue* ya umeme. Nawaomba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono, Ubungo waweke umeme na Kinyerezi waweke umeme haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusipokuwa na umeme haya mabadiliko yote yanayozungumzwa humu ndani ni kazi bure, hatutafika mahali popote. Kwa hiyo, hili lazima tuhakikishe ndani ya mpango huu ulileta na bajeti ni sehemu ya mpango, lazima humo humo ndani hiyo bajeti ujiwezeshe kwa siku zinazokuja. Tumeambiwa tegemezi yetu hapa imefikia asilimia 39. Matumaini yangu ni kwamba *gradually* tunapokwenda mbele tutaambiwa kwamba sasa utegemezi wetu umepungua labda imekuja kwenye asilimia 35 au 30. Kwa sababu *eventually* unataka uondokane na hii *issue* ya kutegemea watu wa kutoka nje wakusaidie. Ndani ya bajeti ni lazima utengeneze kitu kinachoitwa mtekenyo wa ndani.

Mheshimiwa Spika, mtekenyo wa ndani unazalisha kitu kinachoitwa ziada, huwezi ukasomesha watoto, ukanunua petroli, ukanunua kila kitu, halafu ukasema mimi nimeishasomesha watoto wote na mimi nimeishakula. Elimu matokeo yake utayapata baada ya miaka 40. Ukimaliza kila kitu, umesomesha watoto, petroli imenunuliwa, majeshi yamelipwa, mishahara imelipwa, umekwisha, *there is no development*. *Development* ni *surplus* na *development* ni ziada.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima tumefika mahali tuweze kuzungumza barabara zitatengenezwaje, shule zitajengwaje, lakini mle mle tujitengenezee uwezo humo humo ndani ya bajeti ndiyo hii kelele inayopigwa hapa ndani ya watu twende tukafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka nisogee mbele kidogo. Hapa imezungumzwa habari ya kuongeza ushuru wa simu. *This is an account production* na hii namwomba Mheshimiwa Waziri anisikilize. Wewe umesema unataka kufikisha umeme kule vijijini halafu unasema unataka kuongeza ushuru kwenye simu kwa asilimia nafikiri 7, hiyo ita-*frustrate* hiyo *mood.* Maana yake ukiongeza asilimia 7 maana yake ni kwamba unaongeza *cost production*. Ukiongeza hiyo maana yake kwamba tutazungumza kwa muda mfupi. Kwa hiyo, ku-*beep* kutaongezeka, nikitaka kuongea na Waziri Mkuu nam-*beep*, nikitaka kuongea na Spika, nam-*beep*, nikitaka kuzungumza na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, nam-*bee*p ndicho kitakachotokea hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, chonde chonde naiomba Serikali kule kwangu ninavyozungumza sasa hivi, nikitaka kuzungumza na kijiji changu cha Kandashu kule Siha siwapati, Leklimu siwapati, Namwai siwapati, Londorosi siwapati, Ngaranairobi siwapati, Oromwoi siwapati na nina hakika ninazungumza kwa niaba ya Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Monduli kule juu kote hatuwezi kuwapata. Mpaka umwambie sogea, panda kwenye miti ndiyo umpate umwambie tulia hapo hapo unaongea naye kidogo simu imekatika. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ulimwengu wa leo tunavyosema kijiji kimekua cha kwanza unachokiangalia ni suala la mawasiliano. Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya ulikuja *West Kilimanjaro,* Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari ulikuja *West Kilimanjaro,* chonde chonde naiomba Serikali iondoe huu mpango wa ushuru kwenye simu. Gharama ya kutoa taarifa inabaki pale pale. Aliyeko Londorosi akifiwa atatoa taarifa, atateremka

atakwenda Sanyajuu au atakwenda Bomang'ombe. Kwa hiyo, sisi tunachotakiwa ni kumpunguzia wananchi gharama hii. *TTCL* tuliambiwa kwamba vijiji vyote vya nchi hii vitapata simu. Leo ushuru unataka kuongezeka na kupata simu *is modern way of living* ni utaratibu wa kisasa wa kuishi siyo *luxury* ile. *(Makofi)*

Sisi tulio Waheshimiwa Wabunge wote tuliomo humu ndani tunapiga kelele hapa kila mmoja anawasiliana na Jimbo lake. Mimi wananchi wangu wa Siha kila siku wanazungumza na mimi simu wananipa *update* ya mambo yaliyoko kule. Naiomba Serikali chonde chonde tusaidieni, tuondoleeni huu ushuru wa simu ambao umezungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, barabara yangu ya Bomang'ombe, Sanyajuu, Ngaranairobi, mpaka Kamwango nitapata nafasi nzuri ya kuzungumza hapa. Tumezungumza, tumeongea, tumeambiwa upembuzi yakinifu sijui na nini. Mimi naomba niikumbushe Serikali kwamba Mlima Kilimanjaro ungekuwa Afrika ya Kusini hivi tunavyozungumza hapa *fifty percent* ya bajeti ingetoka katika Mlima Kilimanjaro. Mlima wa Kilimanjaro haukai Kilimanjaro unakaa Tanzania, mapato yanayotokana na Mlima wa Kilimanjaro yatakuja mpaka hapa, yatasaidia hizi barabara za Kigoma zinazopigiwa kelele hapa, barabara za Mtwara alizozungumza Mheshimiwa Raynald Mrope, huwezi kuzungumza utajenga barabara bila kujua utapata wapi fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtalii anakwenda Kilimanjaro anakaa siku tatu anangoja papambazuke auone Mlima Kilimanjaro. Leo tumekalia utajiri mkubwa pale, ooh, Kilimanjaro wameendelea sana wale bado unawaongezea na nini. Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, mzee wangu wakati mwingine nakuona unapita kule na vumbi lote lile. Tusaidie ile barabara ya kutoka Bomayang'ombe mpaka Sanyajuu mpaka Ngaranairobi na mpaka Moshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, habari ya kwamba uchumi umekua kwa asilimia 6.7 tunataka kupata kitu kinachoitwa *economy development* siyo *economy growth, they must be one to one function* kati ya *development* ya watu na ukuaji wa uchumi. *Otherwise* mimi nikienda kule Siha naambiwa uchumi umekua, si tunakwenda, wanasema huyu mwisho wake wa kumchagua hatumchagui tena kuwa Mbunge. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Rais Bill Clinton alichofanya alikwenda akatoza matajiri fedha za kodi akazichukua akawapelekea hao watu wadogo wadogo. Watu wadogo wadogo ndiyo wametuketisha humu ndani wazee wangu, ndiyo maana mnamwona Mheshimiwa Rais wetu wa nchi anapeta. Sisi ni matunda ya watu wadogo wadogo. Kwa hiyo, tunapozungumza habari ya uchumi kwamba umekua tunataka tuione *one to one function* kati ya kukua kwa uchumi na *development* ya watu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja iliyoletwa hapa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuzungumza. Lakini naomba pia nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri waliyoifanya pamoja na Watendaji wao. *(Makofi)*

Lakini vile vile nimpongeze Mheshimiwa Yusuf Makamba, hasa kwa kuteuliwa, lakini vile vile kukubali kukaa karibu na ndugu yangu Mheshimiwa Aggrey Mwanri hapa na ndugu yangu Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, pale katika benchi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeanza kwa kuzungumzia bajeti hii moja baada ya nyingine na nitaanza na ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Kwa kifupi bajeti ni nzuri, lakini ni vyema mambo yafuatayo yakawa yamekuwa *reflected* katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kwa mfano, kilimo ndiyo sekta ambayo inachangia kwa zaidi ya asilimia 45 ya Pato la Taifa, yaliyozungumzwa ndani ya mpango mzima ni machache, ningeomba yafuatayo yaongezwe. Uzungumzwe mpango wa *National Irrigation Master Plan*, uelezwe mle. Kwa sababu katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu, miwili iliyopita kumekuwa na upungufu wa hekta zilizolimwa kwa mpango wa *irrigation. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa lazima tuangalie tunakusudia nini kufanya katika kilimo na hivyo tuseme kama mpango wa *Irrigation Master Plan* umekamilika watwambie *Irrigation Master Plan* ina-*cover* hekta ngapi? Kama bado haujakamilika basi tuambiwe. Mimi nafahamu ndani ya Jimbo langu ipo miradi minne ambayo imepelekwa na kukubaliwa katika Mpango wa *National Irrigation Master Plan*. Mmoja fedha zimekwishapelekwa na taratibu za maandalizi zinafanyika ni mpango *wa Irrigation* uliyoko Mashewa Kata ya Kisiwani. Lakini fedha pia zimepelekwa Kata ya Misoswe na mpango wa *Irrigation* pale unaendelea kujengwa. Sasa ni vizuri tukaonyeshwa kilimo tumekiangalia kwa kiasi gani.

La pili, katika mpango mzima kama tumezungumza na tunazungumzia Ilani ya Uchaguzi yapo mambo ambayo yamekwishaainishwa mle unapoyaona hayapo katika Mpango wa Bajeti unaanza kuwa na wasiwasi hasa katika maeneo ya utangulizi. Kwa mfano, uendelezaji wa Bandari ya Tanga kuijenga upya huu haukuguswa. Lakini ni mpango ambao tunadhani ni muhimu utekelezwe katika miaka mitano au kumi inayokuja. Kwa nini tusiutaje? Ujenzi wa reli kutoka Tanga kwenda Musoma imo ndani ya Ilani ni vizuri tukautaja. Sisi Tanzania tutafaidika zaidi na reli hiyo, asilimia zaidi ya 95 ya reli itakuwa ndani ya ardhi ya Tanzania, wenzetu wa Uganda ni kiasi kidogo sana. Lakini Uganda wanashabikia zaidi reli hii kujengwa kuliko sisi ambao reli hii itapita katika eneo kubwa la nchi. Ni vizuri tukaliangalia hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile, miradi ya Liganga na Mchuchuma lazima iwe imetajwa. *Survival* ya nchi hii ni katika miradi mikubwa na bila shaka katika miradi hiyo ya chuma na mkaa wa mawe. Yameanza kuzuka malumbano katika maeneo mbalimbali na hasa katika maeneo yalipo hifadhi hizo za Liganga na Mchuchuma. Sasa tusiachie malumbano hayo yakaharibu faida tunayotarajia kuipata kutokana na uwekezaji katika

miradi mikubwa kama hiyo. Ni vyema tukaitaja na tukasema matarajio yetu ni nini kwa mradi wa Mchuchuma na ni matarajio yetu ni nini kwa mradi wa Liganga.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu, ningetarajia kuona kwamba angalau yale ambayo Mheshimiwa Rais ameyazungumza kuhusu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili kuonyesha thamani ya ahadi ya Mheshimiwa Rais tungetaja mpango ule wa ujenzi wa Chuo Kikuu hapa Dodoma katika mipango yetu kwamba tunakubali ipo tutaitekeleza kama Mheshimiwa Rais alivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Fedha, mimi nafurahi sana kuna mpango mzito mkubwa wa MKUKUTA. Fedha zimetengwa lakini lazima tuiulize Wizara ya Fedha katika mpango huo wa MKUKUTA, je, tumekumbuka kutenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia za mafao ya wafanyakazi katika sekta mbalimbali? Katika Jimbo la Muheza bado wananchi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwenyewe anajua alipokuwa Wizara ya Maliasili na Utalii anafahamu kwamba *World Bank* walituahidi fedha kwa ajili ya fidia, hazikuja. Sasa tumetenga fedha kwa ajili kuwalipa wananchi wa Amani, Wanderema fedha zao zilizobaki. Nashukuru kwamba Serikali imeanza kulipa bila kusubiri fedha hizo za wahisani, lakini zilizobaki je, tumezitenga?

Lakini vile vile tuliahidi katika Bunge kwamba tutawalipa fidia wananchi wa shamba la mpira la Kihu. Je, tumetenga fedha hizo? Lakini je, tumekamilisha mafao ya wafanyakazi wa mashamba ya Mkonge? Hayo ni mambo muhimu sana. Kwa hiyo, kwangu mimi na kwa ushauri wangu mimi MKUKUTA ugawanywe katika maeneo yafuatayo:-

Moja, kuwe na MKUKUTA fidia kwa maana ya kwamba tutawalipa fidia. Hivi unadhani utawashawishi wananchi 15 wajiunge pamoja waanzishe mradi ambapo kwa utaratibu huu tutawawezesha kwa kuwapa shilingi 300,000. Lakini wananchi hao hao 15 au 20 wanakudai wewe Serikali milioni 30. Sasa kwa nini kama unatengeneza MKUKUTA usitengeneze MKUKUTA huu wa fidia kwanza. Kwa sababu ukiwapa hawa fedha milioni 30 watafanya kazi nzuri zaidi hata kuliko 300,000 utakazowapa kwa mpango mwingine wa MKUKUTA tunaotarajia. Kwa hiyo, uwepo MKUKUTA fidia ambao kwa kweli utasaidia kuwaondolewa umaskini kundi kubwa la wananchi wanaodai fidia Serikalini.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA wa pili, uwe na MKUKUTA ambao mimi napendekeza uitwe MKUKUTA ajira. Huu MKUKUTA ajira ndiyo ulenge sasa katika kuwawezesha wananchi waweze kupata vifaa vya kufanyia kazi ili waweze kujitegemea. Kwa mfano, kuna *SIDO*, kuna *VETA*, kuna Chuo kule katika Jimbo langu cha Ustawi wa Jamii watu wanachukua stadi za kazi. MKUKUTA ulenge kwa wanafunzi wale katika Vyuo hivyo kwamba wakimaliza masomo yao wale waliochukua stadi za ufundi wa kushona wanapewa vyerehani, wale waliochukua ufundi wa umeme wanapewa vifaa vya kutendea kazi. Huu ndiyo MKUKUTA utakaowasaidia hawa wanyonge ambao ninaamini kabisa wana matatizo na wanahitaji msaada huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, MKUKUTA fidia na MKUKUTA ajira, lakini huu MKUKUTA ajira nao uendane na MKUKUTA miradi. Wapo ambao hawadai fidia,

wapo ambao hawajaingia katika Vyuo, lakini nao wanahitaji vilevile kuwasaidiwa. Hawa ndiyo watakaojiunga katika vikundi mbalimbali wakafanya kazi wakabuni miradi na Serikali ikawasaidia. Kwa hiyo, MKUKUTA fidia , MKUKUTA ajira na MKUKUTA miradi.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie habari ya mafuta. Kwa bahati nzuri mimi nimefanya kazi katika Shirika la Maendeleo ya Petroli kwa zaidi ya miaka 18. Sekta hii ya mafuta naifahamu vizuri. Tumefanya jitihada kubwa kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alizofanya ya kukutana na viongozi wa makampuni ya mafuta. Naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake kwa jitihada walizofanya kukutana na kuzungumza na viongozi wa makampuni ya mafuta. Mafanikio yameanza kuonekana kwamba yale waliyokuwa wameyakusudia baadhi yamekubalika na yameingizwa katika mpango huu wa bajeti ukiwemo mpango wa kuondoa *VAT* na vile vile na kurekebisha ushuru katika bidhaa za mafuta hasa petroli, mafuta ya taa na dizeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe tahadhari, matarajio ya wananchi ni makubwa sana katika suala hili la punguzo la petroli. Sasa tuwambie mimi nimefanya mahesabu hapa, mahesabu yangu kitaalum kwa kiwango changu yanaonyesha kwamba tofauti haitakuwa kubwa sana, haitazidi zaidi ya shilingi 80 kwa lita punguzo. Je, wananchi wanatarajia nini? Matarajio ya wananchi ni makubwa. Kwa hiyo, tu-*address* hii *issue* ya matarajio ya wananchi kwa kuwambia ukweli baada ya maamuzi haya matarajio yetu ni petroli, dizeli itapungua kwa kiasi gani? Lakini tuendelea kuwashawishi na makampuni ya mafuta kwa sababu itafika mahali tutawalaumu makampuni ya mafuta. Kwa sababu taarifa zangu ambazo nimezikusanya kwenye *internet* zinaonyesha katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, ukichukua petroli peke yake kumekuwa na ongezeko la bei ya petroli kama ifuatavyo:-

Kwa kipindi cha mwaka 2004 hadi Desemba, bei mafuta ya petroli kwenye soko la mafuta na soko linalozungumzia kitaalum ni *mean FOB Mediterranean Italian bases plus oil gram* bei ilikuwa shilingi 335. Ilipofika Desemba, 2005 bei hiyo ya mafuta ilikuwa dola za Kimarekani 506 maana yake kuna ongezeko la zaidi dola 175 kwa kipindi cha mwaka mmoja. Ilipofika Mei, 2006 kwa petroli dola za Kimarekani 704 kuna ongezeko la dola 198 kwa kipindi ambacho ni kifupi zaidi ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, sasa la kutazama hapa na hili ndilo Mheshimiwa Rais alilisema pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba yapo mambo ambayo yatakuwa nje ya uwezo wetu hili ni moja, ongezeko hili la petroli. Tuna uhakika gani sasa baada ya kufanya marekebisho hayo ambapo sasa pengine petroli itapungua kwa karibu shilingi 80, hizi bei za mafuta zitatufikisha wapi, zinashuka au zinaendelea kupanda. Kama zitaendelea kupanda ninachotaka kusema ni kwamba hii tofauti tuliyoiona ya shilingi 80 itamegeka na itakwisha katika kipindi kisichozidi zaidi ya mwaka mmoja na nusu unaokuja itakuwa imekwisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefanya *calculations* ambazo zinaonyesha hilo kwamba ukichukua *average* ya mabadiliko yote, ukaigawanya kwa tani iwe shilingi sasa hivi ni

kwamba kwa *exchange rate* ya shilingi 1,150 niliyochukua kwa lita, kwa tani moja ya mafuta hayo ya petroli ni shilingi 3,350. Maana yake ni kwamba ukiibadilisha kwa *convention factor* ya kutoa kwenye tani kupeleka kwenye lita ambayo ni shilingi 1,359 unapata a*dvantage* tu ya shilingi 25, maana yake itakwisha katika muda mfupi na tutarudi pale tulipokuwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wa kusitisha shughuli za Bunge kwa asubuhi hii umewadia. Lakini naomba niseme mawili tu.

Moja, ni kuwashukuruni nyote kwa jinsi mlivyo makini na mnavyoshiriki katika shughuli za Bunge hili. Nataka kutoa tahadhari tu kuna mmoja au wawili jana jioni kwenye kipindi cha habari cha *ITV* walionekana wakiwa katika tafakari nzito sana. Kwa kuwa nawapenda wote hali hiyo si nzuri kwa kuchaguliwa tena kwa hiyo, ni vizuri sana tujitahidi. Asilimia 98 tuko sawa tu, lakini tafadhalini sana humu ndani ziko kamera sita na zinanasa karibu kila kitu. Kwa hiyo, ni vizuri ukijisikia umechoka kidogo nenda kantini kanywe kahawa halafu unarudi unaendelea. *(Makofi/Kicheko)*

Pili, kesho, 5.30 asubuhi nitasitisha shughuli za Bunge kwa sababu saa sita kasoro robo tutapata mgeni, Rais wa Jamhuri ya Ireland. Mgeni huyo atakuwa na mwenyeji wake Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na mgeni huyo atalihutubia Bunge.

Sasa utaratibu ambao nitaukumbusha tena jioni ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wote tutabaki tumeketi, wakati tunampokea mgeni nikishasitisha shughuli za Bunge. Ila tu Wenyeviti wote wa Kamati na Makamishna wa Tume kwa niaba ya Bunge zima ukiacha upande wa Serikali ambao ni dhahiri wanahusika tutakuwa pale nje kumpokea Rais huyo mgeni wetu ambapo na nyimbo za Taifa zitapigwa kule nje.

Wengine wote tunaomba mbaki kwa sababu baada tu ya mapokezi hayo tutaingia humu ndani kwa utaratibu tuliouzoea wa kuwapokea wageni hasa baada ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kutoa raia ya maombi ya kutengua Kanuni ili kuwaruhusu watu walio wageni kuingia humu ndani ya ukumbi. Shughuli yenyewe itachukua takriban saa moja hadi kutoka nje na kuweza kupiga picha na mgeni kwa vikundi maalum kama itavyoelekezwa.

Kwa hiyo, naomba kesho baada ya mgeni kuondoka Kamati ya Uongozi tukutane kikao kifupi cha dharura ili kuelezana jinsi gani tutafidia muda wa saa 1.30 ambao ungetumika katika mjadala wa hoja za Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha na ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji tutaufidia vipi ili tuweze kupokea majibu ya hoja siku ya Ijumaa jioni. Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia.)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuweza kunipa nafasi hii kwa kuweza kuchangia hotuba iliyopo mbele yetu ambayo iliwasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hotuba hii tumeipokea na ni hotuba nzuri ambayo inatupa mwelekeo wa kuweza kuleta maisha bora kwa Watanzania. Naomba nishukuru pia wadau wote walioshiriki katika kuandaa kwa namna moja au nyingine bila kuwasahau wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ambao walifanya kazi kubwa ya kupitia na kuchambua Bajeti hii na hatimaye hivi sasa ipo mikononi mwetu tunaendelea kuijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utalenga katika ushauri au kusisitiza katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwanza katika suala la miundombinu. Katika Bajeti hii imeelekeza kwamba shughuli za miundombinu katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Rukwa pamoja na Kigoma na Tabora itatiliwa mkazo katika kuimarisha shughuli nzima hizi za miundombinu. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara napenda kwanza nianze kwa kutoa shukrani kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya tatu kwa kazi nzuri ambayo alikuwa ameifanya ya kuweza kujenga daraja la Mkapa katika Mto Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuelekeza shukrani hizi kwa msingi mzuri aliouacha kwa kuweza jiwe la msingi katika barabara ya Kibiti-Lindi. Mheshimiwa tunashukuru sana na ninaiomba Serikali ya awamu ya nne iendeleza shughuli hizi kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Kama tunavyojua kwamba barabara hii kwa kweli ni kero ya wananchi wa Mikoa ya Kusini kwa kipindi kirefu hata mimi kabla sijapata akili niko shule ya msingi nilikuwa nawasikia Wabunge wakilalamikia barabara hii. Sasa naomba kabisa katika awamu hii Serikali ifuatalie kwa karibu usimamizi wa karibu barabara hii iweze kukamilika ili ajenda hii ya barabara ya kusini tuweze kufutiwa hapa Bungeni. Inakuwa ni aibu kila awamu Wabunge wanaoingia wanazungumzia suala moja la barabara hii ya Kibiti Lindi. Tunaomba sana awamu hii barabara hii iweze kuisha.

Mheshimiwa Spika, ukitaka kujua tatizo lililopo Kusini kwa ajili ya adha ya barabara hii ningependa ufike pale angalau Ubungo kwenye kituo cha mabasi ndipo utakapohakikisha kwamba wenzenu bado tuko nyuma. Kwa sababu ukiangalia mabasi yanayoenda Mikoa ya Kusini pengine hata viwanda walitengeneza mabasi hayo ukiwapelekea wanaweza wakawa wameyasahau. Ni mabasi mabovu wanzenu bado tuko kwenye mabasi ya *carrier* juu, ambayo Mikoa mingine wameshayasahau toka kipindi kilichopita. Sasa tunaomba sana kwa kweli awamu hii ajenda hii ya barabara ya kusini tufutiwe kabisa kwa kukamilisha hiyo barabara.

Vile vile napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa msingi aliouweka Mheshimiwa Benjamin Mkapa kwenye daraja la Mto Ruvuma ambalo litakuwa linaunganisha Msumbiji na Tanzania. Msingi umeshawekwa tunachokitarajia sasa hivi ni kwamba awamu hii maandalizi ya ujenzi wa daraja hili yatakuwa yamekamilika na sisi tuweze kufunguliwa milango ya Tanzania kwenda Msumbiji ili tuweze na sisi kufanya biashara na wenzetu wa nje kama mipaka mingine ilivyo wenzetu wanavyoweza kunufaika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Samahani itabidi ujaribu *microphone* ya jirani hapo tafadhali, zote zenu. Katibu mafundi warekebishe hiyo. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee, suala la pili ambalo nataka nichangie ni suala la kilimo. Tutakumbuka kwamba katika mwaka huu tumekuwa na tatizo kubwa sana la njaa karibu Mikoa yote ya Tanzania ukiwemo na Mkoa wa Mtwara. Tunashukuru Serikali kwa kweli ilifanya jitihada za kuweza kutupatia chakula cha msaada ili kunusuru maisha ya wananchi wetu. Lakini kilichobakia sasa hivi ilikuwa ni karibu Mikoa yote kuweka mikakati ambayo itaweza kuwasaidia wananchi wetu katika kipindi kijacho. Sisi Mkoa wa Mtwara tumejitahidi kufanya mikakati ambayo tunaamini kabisa kama Serikali itatuunga mkono, naamini kabisa pengine wananchi kwa kipindi kijacho wanaweza wakajikwamua wenyewe katika suala la njaa, mpango huu si mwingine ni kwa ajili ya palizi ya korosho kwa sababu Mkoa wa Mtwara zao kubwa sana ni korosho.

Mheshimiwa Spika, jitihada zimefanyika, katika Wilaya za Masasi, Nanyumbu, palizi ya mikorosho imefanyika, mwaka huu hakuna mkorosho uliobakia bila kupaliliwa lakini kuna tatizo kubwa sana la kuweza kupata pembejeo. Halmashauri wamejitahidi kwa kadri ya uwezo wao kununua pembejeo na kuweza kusambaza vijijini lakini pembejeo hazitoshi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iweze kutusaidia au ifanye jitihada za haraka sana kwa sababu muda wa kupulizia mikorosho unapita ili wananchi waweze kupulizia mikorosho na hatimaye pengine korosho kama zitaweza kuzaa wakapata pesa wananchi wakaweza wakajinunulia chakula na kuweka akiba.

Mheshimiwa Spika, suala la lingine ambalo nataka kuchangia ni suala la maji. Suala la maji kwa Mkoa wa Mtwara karibu Wilaya zote zina tatizo la maji, hususan Tandahimba, Newala, Masasi pamoja na Wilaya ya Nanyumbu. Lakini napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa kauli ambayo ameitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu leo hii asubuhi ya kwamba Wilaya ya Masasi itafanyiwa kila mkakati wa kuweza kupatikana pesa kuweza kuondoa kabisa tatizo hili maji, ninashukuru sana. Lakini pamoja na jitihada hizo napenda nikumbushe kwamba Kusini tuna matatizo. Huwa miradi inaandaliwa inaweza ikafikiwa kwenye hatua ya utekelezaji, utekelezaji unasimama sababu hatuzijui. Ninalizungumza hili kwa sababu mwaka wa fedha 2001/2002 kulikuwa na mpango wajapani walikuwa tayari kusaidia kuchimba bwawa kwenye Mto Lukuledi ambalo lingeweza kusaidia kwa wanaoishi Magharibi kwenye Wilaya ya Masasi pamoja na wananchi wanakaa kwenye mpaka wa Mto Lukuledi kwa Wilaya ya Nachingwea. Mpango huu ulikamilika pesa zilishatengwa lakini sielewi wahandisi tulionao kwenye Mikoa yetu ni wahandisi wa namna gani.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu inawezekana hata taaluma yao hawaitumii vizuri. Waziri wetu Mkuu wa hivi sasa wakati akiwa Waziri wa Maji alikuja kwa ajili ya kutaka kuangalia eneo la kuchimba bwawa, kwa sababu pesa zilikuwa tayari. Lakini alipofika ilishangaza wahandisi wanasema kwamba Mheshimiwa mradi huu ni afadhali tuache kwa sababu tukichimba bwawa hili litakuwa na maji ya chumvi ambayo hayafai kwa matumizi ya binadamu hata wala, kulishia wanyama, wala kumwagilia. Lakini sasa kwa kuwa walishagundua kwamba maeneo yale ya Lukuledi na vijiji vinavyozunguka na vijiji vya Nachingwea kuna tatizo kubwa la maji tulishangazwa kuona kwamba mradi huu uliisha na hakuna mbadala wowote uliofanyika.

Kwa hiyo, napenda kuzungumza kwamba tatizo la wakazi wa Kata ya Lukuledi na Kata za Ndomoni kwa Wilaya ya Nachingwea tatizo la maji hadi hivi sasa lipo tunaomba Serikali iangalie mbadala wa hilo ambalo walishakuwa wametuandalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala linalogusa watumishi wa Halmashauri. Tatizo la watumishi wa Halmashauri hatuwezi kulizungumzia kwa undani zaidi bila kuwazungumzia Madiwani. Kwa sababu hawa watumishi wako chini ya Madiwani, lakini inasikitisha kuonekana kwamba Waheshimiwa Wabunge wanajaribu kutoa hoja zao za kuwatetea Madiwani lakini Serikali hadi hivi sasa haijachukua jukumu lolote la kuweza kuzisaidia Halmashauri ili kuweza kuboresha maslahi ya Madiwani.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa sisi Waheshimiwa Wabunge, hawa Madiwani ndiyo fimbo yetu ya mkono wa kulia wa kuweza kutusaidia katika shughuli zetu za maendeleo katika Majimbo na Mikoa yetu. Sisi kwa kipindi kirefu tutakuwa tunashiriki huku katika vikao vya Bunge, kwa hiyo, wenzetu Madiwani wanabaki katika maeneo yetu, wao ndiyo watakuwa wahamasishaji wakuu katika shughuli za maendeleo katika majimbo yetu. Lakini kazi hizi wanazifanya katika mazingira magumu, hawana usafiri, posho wanazozipata ni ndogo lakini wanafanya kazi hizi kwa juhudi zao zote na sisi Wabunge tunaporudi kwenye maeneo yetu tunakuta ndugu zetu hawa wamefanya kazi nzuri lakini katika hali ya mazingira magumu. Ningeshauri au ningeiomba Serikali sasa hivi ikae iangalie ni jinsi gani tunaweza kuzisaidia Halmashauri zetu katika kuboresha maslahi ya Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niendelee kuchangia katika suala la maslahi ya watumishi wa Serikali. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati katika hotuba hii imegusa kwamba watumishi watakuwa wameongezewa mishahara endapo kama Bajeti yetu itapita. Mimi nimeshukuru sana katika hili lakini pamoja na kuboresha maslahi ya hawa watumishi, ningeomba tuangalie angalau maeneo wanayoishi majeshi yetu kwa mfano, Jeshi la Ulinzi, Polisi na Magereza. Watu hawa wanaishi katika mazingira magumu, nyumba ambazo kwa kweli sasa hivi zimeshachakaa lakini wanaishi humo, vile vile wenzetu wa magereza kazi yao ni ngumu tunaweza tukasema kwamba karibu nusu ya maisha yao na wao wanaishi maisha ya kijela jela lakini Serikali bado tumewaacha hawa watu wakiwa wanaishi katika mazingira magumu. Ningeomba Serikali hata kama ni kwa kipindi kijacho tuangalie ni jinsi gani tunaweza tukaboresha maeneo wanaoishi hawa askari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kengele imeshalia ya kwanza, nisingependa nigongewe tena kwa mara ya pili naomba nitamke tu rasmi kwamba ninashukuru kwa kupata nafasi hii na ninaunga hoja mkono kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nikumbushe tena kwamba anapoongea mmoja amewasha *microphone,* yeyote Mheshimiwa Mbunge huko mliko akijaribu kugusa *microphone* anaharibu mawasiliano yote. Kwa sasa hivi mafundi wamegundua kwamba katika mstari ule anaokaa Mheshimiwa Kidawa Salehe Hamid, kuna Mbunge mmoja aliwasha *microphone* ndiyo iliyofanya zizimike, kwa sababu haitakiwi ziingiliane hivyo.

Kwa hiyo, sasa inarekebishwa lakini nawasihi sana tuwe waangalifu tusiguse *microphone* wakati mwenzetu amekwishawasha *microphone* na anaongea. Hiyo inaharibu kabisa mtambo wa kompyuta unaosimamia hizi *microphones*. Napenda nimwambie Mheshimiwa Mariam Kasembe kwamba dakika zake mbili ambazo zilipotea wakati najaribu kurekebisha *microphone* zilifidiwa asidhani amepunjwa. Namwita Mheshimiwa Lucy Mayenga wakati Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia ajiandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza kabisa napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kupongeza Bajeti hii, Bajeti ambayo imekuwa ya kwanza kuwasilishwa na Waziri wa Fedha mwanamke, ambaye kwa kweli na yeye ameonyesha kwamba wanawake tunajali maana amewasilisha maswala ambayo kwa kweli Watanzania wengi tumekuwa tukiyategemea na kuyatarajia ingawa tunajua kwamba matatizo mengi hayawezi kutatuliwa kwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka kuzungumzia suala zima la ajira kwa vijana. Tunapozungumzia kuongezeka kwa kukua kwa uchumi, kuongezeka kwa pato la Taifa na ambalo mpaka sasa hivi limefikia asilimia 6.8, mimi nadhani hatutaweza kuzungumza haya ikiwa kama hatutazungumzia matatizo ya ajira kwa vijana wetu hapa Tanzania. Hivi sasa nchi yetu inajitahidi kadri inavyoweza kuweza kuhakikisha kwamba inapenya katika mfumo wa soko huria duniani ambao uko sasa hivi. Lakini kuna vikwazo vingi sana ambavyo vijana wetu pamoja na Watanzania kwa ujumla wanavipata kutokana na wao kuwa na uwezo lakini mazingira yamekuwa yakiwakwaza. Hivi sasa kulinga na mfumo wa soko huria kumekuwepo na watu kutoka nje wengi sana ambao wanaingia hapa Tanzania.

Lakini mimi nilikuwa naiomba Serikali katika hili, Idara ya Kazi katika Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana waweze sasa kuamka, waweze kuwa ni watu ambao wanashughulikia matatizo haya ya vijana hasa kwa kuhakikisha kwamba wanajitahidi kufanya ukaguzi wa maeneo ya kazi mara kwa mara. Vipo vitu ambavyo vimekuwa vikilalamikiwa na watu wengi, ni masuala ambayo yamekuwa yakiulizwa na vijana wengi, ni masuala ambayo yamekuwa yakiulizwa na vijana wengi popote pale. Lakini inaonekana kwamba imekuwa ikisemwa tu kwamba kuna wageni wengi lakini jinsi gani walivyo hapa Tanzania, kuna wengine ambao wapo kihalali hatukatai, lakini kuna wengine ambao hawako kihalali, hali ambayo inasababisha vijana wetu ambao

wameenda shule vizuri wanakosa nafasi kutokana na nafasi zao kufanywa na watu waliotoka nje. *(Makofi)*

Mimi pia katika hili nilikuwa naomba kuulizia, Tanzania katika mfumo wake mzima wa kuwaajiri askari polisi pamoja na Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kuna utaratibu kwamba unapokuwa umeajiriwa na majeshi haya unapoamaua kuacha kazi kwa sababu yoyote ile, unapoamua kuacha kazi umekwenda nje labda kusoma unaporudi huwa mara nyingi hawakubaliwi. Mimi nilikuwa naomba kuweka msisitizo kwa Wizara ya Usalama wa Raia, katika nchi mbalimbali ambazo hasa zinafungua Mahakama za Kimataifa, kwa mfano hata *The Hague* au *ICTR*, zimekuwa zikichukua watu wengi wa *profession* mbalimbali na kati ya hawa polisi wetu wamekuwa wakichukuliwa wengi sana. Kuna idadi ya polisi, kuna idadi ya wafanyakazi hapa Tanzania wanachukuliwa wanakwenda kufanya kazi. Kinachowapeleka kule inawezekana ni maslahi. *(Makofi)*

Mimi nilikuwa nadhani hivi sasa Serikali yetu pamoja na Wizara hii hebu ijaribu kuangalia upya kuhusu huu utaratibu ambao unafanywa kwamba ikiwa wewe ni polisi, ukiacha kazi ukiondoka basi utakaporudi hauruhusiwi tena. Kwa sababu inawezekana labda walikuwa wameweka hii sheria kwa utaratibu mzima wa kuwa-*discourage* watu kuacha nchi yao na kuondoka. Labda sasa hivi hebu wajaribu tena kuangalia huu utaratibu upya kwa sababu watu hawa wanakuwa wamekwenda huko, wamefanyakazi kwa miaka kadhaa 10, 15, lakini wemerudi wana ujuzi basi hii Serikali sasa hivi kwa sababu wameingia katika Serikali nyingine mpya awamu ya nne hebu tujaribu kuangalia upya kuhusu hili wazo ili ikiwezekana tuwarudishe hawa vijana wetu wa Kitanzania ambao pia wataweza kutusaidia kupambana na masuala mbalimbali katika majeshi yetu katika mbinu za kisayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Baada ya kuzungumza suala hilo la ajira, nilikuwa napenda kuzungumzia pia suala la *EPZ*. Katika ukurasa wa 37 wa hotuba ya Waziri wa Fedha amezungumzia kwamba Serikali itaongeza juhudi zaidi za kuhamasisha uanzishaji wa maeneo maalum ya uwekezaji na uzalishaji kwa ajili ua uuzaji nje yaani *EPZ.* Mimi nilikuwa kwanza napenda kupongeza utaratibu mzima na mfumo mzima na kazi yote ambayo Serikali imekuwa ikifanya katika kuhakikisha kwamba suala la *EPZ* linafanikiwa. Lakini mimi nikikuwa naomba kushauri. Hivi sasa kumekuwepo na wawekezaji kutoka nje ambao wamekuwa wakilalamikiwa kwamba wanatumia malighafi ambazo si za hapa nchini. Mimi nilikuwa naomba basi viwanda hivi vitakavyojengwa hapa Tanzania viweze kutumia malighafi za hapa hapa Tanzania. *(Makofi)*

Lakini hata hivyo waendelee kutumia malighafi, vile vile kuwepo na nguvu kazi yenye ujuzi. Hizi *EPZ* zitaanzishwa lakini basi na sisi katika *level* yetu Wizarani na sehemu mbalimbali tuweze kuwasomesha vijana wengi zaidi ili kwa kweli kuwe na nguvu kazi yenye ujuzi katika kukabiliana na suala hili jipya ambalo linaingia. Kwa sababu wenzetu wageni wamekuwa wakiona mambo kama haya ya maendeleo na hizi hatua ambazo zimeanza kupigwa hapa Tanzania na wao pia wanaanza kujitayarisha. Kwa hiyo, na sisi pia ni vizuri tukajitayarisha kuweza kujua kwamba suala hili tunaweza kukabilina nalo vipi na jinsi gani litaweza kuwafaidisha Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kidogo kuzungumzia suala la ukwepaji wa ushuru wa mafuta katika bandari yetu ya Dar es Salaam. Biashara ya mafuta ni biashara ambayo kwa kweli kwa wale wafanyabiashara ni kitu ambacho mtu anaota na anaona kwamba isingetokea hata siku mmoja akaja ikatokea sababu yoyote akaacha kufanya hii biashara. Hivi sasa katika bandari yetu kama tunavyojua uingizaji wa meli pale ni dola 1,000 wanachajiwa wale ambao wanaingiza zile meli. Lakini sasa hivi kuna utaratibu umeanzishwa kwamba hawa watu kwa sababu wanajua wakiweka gati pale kushusha bidhaa zao kama ni mafuta, kama kitu kingine chochote wanachajiwa dola 1,000. Hivi sasa wamekuwa na utaratibu wa kuweka kule baharini katikati ambako hawaingizi kabisa bandarini na wamekuwa wanashusha mafuta. Wafanyabiashara wengi wemekuwa wakienda kule na kuchukua mafuta na hatimaye kuendelea katika matumizi yao.Wizara ya Fedha, Wizara ya Usalama wa Raia ni vizuri sasa iongeze doria katika maeneo haya, eneo hili la bahari limekuwa sasa kutokana na hali hiyo ya ukwepaji kodi imeonekana sasa ni sehemu nzuri ambayo mtu anaweza akakwepa kodi lakini akajinufaisha kwa njia nyingine, akatumia kama vile ni sababu.

Mheshimiwa Spika, niongee haraka haraka kuhusu suala la wanyamapori. Katika suala zima la ukuaji wa uchumi hapa Tanzania, utalii umekuwa ukisaidia kwa kiasi kikubwa sana kuweza kuinua pato letu na kuinua uchumi wetu kwa ujumla. Lakini mimi nilikuwa nashauri, Wilaya zote ambazo ziko karibu na mbuga za wanyama ziwe na viongozi ambao kwa njia moja au nyingine wanauchungu na hawa wanyama. Kamati ya Maliasili na Utalii hivi karibuni ilifanya ziara katika eneo la mbuga ya Serengeti. Tulikwenda kule na moja kati ya mambo tuliyashuhudia ni kwamba wale wahusika ambao wako katika Wilaya hizi kama ni Mahakimu, kama ni Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na kadhalika wamekuwa ni watu ambao kwa kweli suala la uchungu wa wanyama hawana. Sasa mimi nilikua ninawaza kwamba Serikali ihakikishe basi kama ni Mahakimu, wanawekwa Mahakimu ambao kwa kweli watakuwa na uchungu endapo kama kutakuwa na mtu anafanya ujangili katika maeneo haya ya mbuga za wanyama achukuliwe hatua kali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kati ya vitu ambavyo tulielezewa na yule Mhifadhi Mkuu wa pale alisema kwamba katika kesi 45 ambazo zilikuwa zimefikishwa Mahakamani ni kesi mbili ndiyo zimetolewa hukumu. Kesi nyingine Hakimu anasema kwamba wahusika wamekimbia hawajulikani waliko.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hasara ambayo imetokana na uharibifu wa hawa wanyama, wanyama wameuwawa, wanyama wamechunwa ngozi na Tembo wamechukuliwa zile pembe.

Mheshimiwa Spika, lakini unakuta huyu Mkurugenzi au hawa Mahakimu inaonekana kwamba ni watu ambao wana-*collide* na hawa watu ambao wanafanya uhalifu na matokeo yake nchi yetu inakosa pesa na tutaendelea kulalamika hivyo hivyo. Lakini kwa kweli mimi naomba kwamba Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi na Mahakimu katika Wilaya zote ambazo zina Mbuga za wanyama wawe ni watu ambao wanachujwa mara mbili mbili.

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia, ninaomba kuzungumzia suala la mwisho ambalo ni suala la mgawanyo wa rasilimali katika Mikoa yetu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi nina ombi tu kwa Wabunge wenzangu kwamba tusiendelee tu kuilalamikia hii Mikoa ambayo tunaona kwamba ina neema zaidi. Sisi wenyewe katika Mikoa yetu, katika hotuba zetu huko kwa wananchi, tuendelee kuwahimiza kufanya kazi na pia tuwe wakweli kwa wananchi wetu. Kwa sababu utakuta mambo mengi Waheshimiwa Wabunge tunakuwa tukiongea au kufanya chochote cha kusisitiza kuhusu maendeleo, wananchi wetu imekuwa baadhi ya vitu hatuwaambii ukweli kwa sababu ya ile tu kuona kwamba kwa sababu naweza hapa nikasema ukweli, ninaweza nikawaambia hapa msinywe pombe, wanaweza kuwanyima kura.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani tunapozungumzia suala hili la kuinua uchumi, tuangalie na tubadilishe utaratibu mzima, tuanze na sisi wenyewe kwa wananchi wetu kabla na kumalizia huko.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine na Serikali nayo katika huu mgawanyo wa rasilimali katika Mikoa mbalimbali, basi huko ambako kunalalamikiwa wasione kunalalamikiwa bure na wao kidogo hebu waanze kuwaangalia kwamba hivi kwa nini hawa watu wanalalamikia huku tu? Pengine kuna ukweli!

Mheshimiwa Spika, Ahsante sana!

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa!

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa hivi nina *message* kutoka kwa mafundi kwamba kuna kitu kinaitwa *Error Memory Message* kwenye Mfumo. Wameomba sekunde chache. Kwa hiyo, mkiniona kimya siyo kwamba ni chochote, ila ni kwamba tunaomba warekebishe. Mafundi, endeleeni!

*(Hapa Bunge lilikaa kimya kwa sekunde 30)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Losurutia, pale kwako ilikuwa ndiyo inaonyesha kabisa kwamba kuna tatizo.

**MBUNGE FULANI:** Kote.

**SPIKA:** Kote! Basi, mafundi mjitahidi tumalize hilo tatizo.

*(Hapa Bunge lilisimamisha Shughuli zake kwa dakika 10)*

**SPIKA:** Ahsante sana! Natumaini sasa labda kuna nafuu! Bado! Basi labda tuendelee kwa sababu mtachukua muda mrefu bure kama baadhi ya *mic* zitasema, basi itatosha. Namwita Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, kama nilivyosema atafuatiwa na Mheshimiwa John Lwanji, wakati huo huo Mheshimiwa Charles Kajege ajiandae.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hoja ya Wizara hizi mbili. Hakika baada ya kukushukuru wewe, naomba kuishukuru Serikali kwa dhati kwa kutuponya njaa. Ile njaa haikuwa mzaha, watu wengi walikuwa wanakula na kulala katika Miji mikubwa, lakini huko Vijijini ilikuwa hatari sana. Nashukuru katika Wilaya yangu tulipata chakula na hakufa mtu kama ilivyotolewa katika ahadi ya Serikali kwamba hatakufa mtu, Serikali itatupa chakula na imetupa. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe hongera zangu za dhati hususan kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama wanavyosema ni mama aliyefanya kazi kwa umahiri mkubwa. Nadhani watakaofuata baadaye watafuata nyayo zake. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshiniwa Waziri wa Mipango amefanya kazi vizuri, naye hongera nyingi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie juu ya kilimo kwa uchache. Kilimo kimeonyeshwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango kwamba kinachangia asilimia 45.6 ya pato la Taifa na mwaka huu imeshuka. Mwaka 2004 ilikuwa asilimia 46.5.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa kilimo umeshuka tena, ni 5.2. *Area* ya mashamba hekta za umwagiliaji zimeshuka. Fedha zilizowekewa kwa kilimo nazo zimeshuka vile vile. Sasa, hofu inaniingia kweli kweli! Tumesaini Mkataba wa *SADC* kwamba uwekezaji katika kilimo lazima ufikie asilimia 10 ya Bajeti ya nchi. Lakini, tumechangia Bajeti ya Kilimo ni 3.2.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imetabiri kwamba hatuwezi kwenda mbele kwanza, lazima tunyanyue kilimo kiende kwa kasi ifikapo mwaka 2010 kifikie asilimia 20. Sasa, utakuta mwaka jana 2005 kimekuwa asilimia 5.2. Hii *point* inayotakiwa na Ilani ya CCM kwamba tufikie asilimia 20 katika miaka minne ijayo, nayo inanitia hofu. Hii iliwekwa hivyo kwa sababu Ilani inasema vile vile tukifikisha ukuaji wa kilimo asilimia 20, tunaweza kufanya uchumi ukakua kwa asilimia 10.

Sasa, hapa mimi tatizo langu ni kwamba *speech* hii au Bajeti hii haionyeshi hatua kwa hatua. Mwaka huu tuko 5.2 mwakani na mpaka kufikia 2010 hizi hatua zimewekwa wapi katika hotuba hii? Tutakwendaje? Mwakani tutasema kilimo kitakua kwa asilimia ngapi? Sasa, hapa ningeomba sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango atueleze tunakwendaje kufikia asilimia 20 ya ukuaji kwa kilimo chetu itakapofika mwaka 2010 kwa kufuata Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Hawa wenzetu wa *SADC* tunawaambia nini kwa kutoa asilimia tatu katika kilimo wakati tumetia Mkataba tuweke asilimia kumi katika *investment* ya kilimo? Sasa hii inaonyesha njaa hapa kwa kufuata Bajeti hii. Tukitaka na tusitake, tuamue na watu wa kuamua ni hawa wawili, wafanye mapinduzi, Waasisi mapinduzi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango kwamba sasa tutafanya mapinduzi ya

dhati ya kilimo. Mheshimiwa Mungai yeye anapokea tu, lakini hawa wawili wakifanya maamuzi, kutia fedha kule katika Wizara ya Kilimo, tutafanya mapinduzi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, sisi, kule Rufiji, miaka ya 1950 na 1960 kulikuwa na Shirika linaitwa *Tanganyika Agricultural Cooperation*. Lilifanya utafiti wa mazao gani yanayoota Rufiji, ikamaliza. Nadhani Wizara ya Kilimo wanayo hii na *in fact* wakati ule alitumwa Afisa Mkubwa wa Serikali hii, naye si mwingine ila Mheshimiwa Idd Simba kwenda *Tennessee Valley Authority* ya Marekani ili mfumo ule wa kilimo uletwe katika Bonde la Rufiji. Lakini, alivyorudi mpaka leo hatukupata kitu, badala yake tumepata kitu kinaitwa Lubada. Kule Rufiji hawajafika watu wa Lubada, sijui wanafanya kazi wapi! Makao Makuu yako Ubungo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Lubada ifutwe, badala yake tufanye mapinduzi! Kwa nini? Kwenye miaka ya 1950 na 1960 tulijaliwa kupata matrekta mengi Rufiji.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka tulivuna mpunga mwingi na pamba nyingi, mwisho wakaitwa *TANU Youth League* kuja kuvuna na kupewa taarifa, unachovuna ni chako ondoka nenda nacho, sisi tumechoka! Hiyo ndiyo kazi ya matrekta ukipeleka Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba matrekta yapelekwe Rufiji. Kwa uchache, kila Kata moja ipate Trekta moja na kwa ajili hii, haya ni mapinduzi. Tungeomba trekta zinazokwenda katika sehemu kunakolimwa chakula au mazao ya chakula, bei ya trekta ishuke iende mpaka nusu, tukopeshwe kwa muda mrefu wa mika mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa naomba nimpe hongera Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Nilikwenda katika Wizara yake, kuna *Area* inaitwa *Mechanised Agriculture Department*, wanayo matrekta pale. Lakini bei yake bado iko juu na kwamba wote tuliambiwa tukakope. Lakini mimi ninaloomba, kwa kuwa haya ni mapinduzi, lazima ikubalike tu, tutatoa hela, tutakopa hela, tutapeleka pale. Kama bei ya trekta moja ni Shilingi milioni 25, unaweza kabisa kutumia Shilingi bilioni 25 ukawapa trekta moja kila Kata, kila Wilaya. Ah! Trekta moja halitoshi. Kule kwetu Rufiji tungepewa sisi trekta 19 kila Kata na kila Kata wangepata 19, tungeshukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hvi kwa sababu ninajua wale wenzetu walioko katika mbuga za wafugaji, wale hawalimi. Kwa hiyo, pamoja na Wilaya kubwa, lakini hawalimi wale. Wale wasukuma, wao wanatumia ng'ombe tu. Lakini kule Rufiji plau la ng'ombe haliwezi kuzindua yale magugu makubwa. Haliwezi! Lazima upeleke trekta.

Mheshimiwa Spika, lingine, hizi siyo hadithi. Ukisoma historia utakumbuka *Chairman* Mao Tse Tung China *with his greatest leadership,* aliwatoa Wachina katika omba omba ya chakula mpaka leo wako huru. Lakini haikuwa mzaha, waliamua kufanya mapinduzi kabisa na wamefanikiwa

Mheshimiwa Spika, ukienda India ukasoma historia ya India, *The Indian Green Revolution* ya Indira Gandh, mpaka leo Wahindi hawaombi Chakula. Lakini haikuwa

mzaha, haikuwa kibajeti hiki, hapana. Yalikuwa ni maamuzi ya kitaifa, tunakwenda katika kilimo na wakaenda katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninaloomba ni kwamba, kurudia tu kwamba Tanzania ina ardhi tele na maji tele na watu wapo, tufanye mapinduzi haya mara moja, tuweze kubadilisha hili suala la omba omba. Tuna Mabonde mengi sana. Bonde la Rufiji kuna *estimate,* likililimwa lote tutalisha Tanzania nzima na vile vile kufanya *export* ya chakula. Pelekeni pesa pale. Siyo pesa moja moja, hapana. Peleka matrekta, peleka pale huduma za ugani, Inshallah Mwenyezi Mungu tukiwa na nia nzuri, tutafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tena nizungumze juu ya barabara hususan barabara ya kutoka kwanza Mkuranga mpaka Kibiti, halafu Ndundu mpaka Somanga. Hii ni barabara ya Kusini. Barabara hii inaendeshwa na inatengenezwa kwa mwendo wa kinyonga. Miaka mitatu, kilomita 150, yaani haieleweki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninadhani njia nzuri, Mheshinmiwa Waziri wa Miundombinu aitizame barabara hii, inatia aibu.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ya kufika Utete ambapo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji, haifikiki. Mimi nimewahi kukwama pale na shahidi ni Mheshimiwa Mwantumu Mahiza - Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Alikuja kunikwamua katika tope lile. Nilipata tatizo kubwa na ukiuliza vile vile Mheshimiwa Celina Kombani - Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), alipita na akapiga simu kule kule kumwambia Mheshimiwa Milton Makongoro Mahanga - Naibu Waziri wa Miundombinu, hivi mmewasahau watu wa Rufiji! Sasa, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inasema kila Makao Makuu ya Wilaya yatafikika wakati wote. Sisi tunaomba mfanye hili tu, tufike Utete wakati wote.

Mheshimiwa Spika, katika barabara, kuna suala la barabara fupi inayotoka Kibiti kupitia Mkongo mpaka Utete, ina Pantoni. Barabara hii ina ahadi ya Rais na ni fupi, kilomita 44, lakini kwa sasa hivi kwa kupitia Daraja la Mkapa, lazima utumie kilomita 84 kufika Kibiti na kufika Utete. Sasa, tunadhani hili nalo linataka majibu ya haraka haraka.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *The Selous*. Asilimia kubwa ya *Selous* iko Rufiji. Haifikiki! Barabara yake mbaya kabisa! Kwa kuwa barabara hii iko katika Wilaya Rufiji lakini inaleta tija kwa Watalii, tunaomba barabara hii ijengwe ili iweze kufikika wakati wote, nayo ni barabara inayotoka Mkongo kwenda katika Vijiji vyote, inaishia Mloka kule Rufiji.

Mheshimiwa Spika, kama ninao muda, nataka nizungumze juu ya Afya. Wizara ya Afya, tunamshukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, kwamba kila Kijiji kitapata *Dispensary* na kila Kata itapata Kituo cha Afya. Hii habari inaleta faraja na ninadhani Rufiji isiachwe nyuma katika hili kwa sababu sasa hivi kwa kweli kuna matatizo ya afya kule Rufiji.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la elimu. Wote mnajua. Yuko mmoja yeye kaniuliza, wewe umekuwaje Profesa? Iko chini kule! Tunaloomba, pamoja na kwamba kila Wilaya itafanya nguvu zake, lakini sisi tutahitaji nguvu za ziada kama mlivyofanya kwa wale wafugaji. Wakati mwingine watu wanapewa *Boarding School*, *Primary school* kwa sababu ya hali halisi. Sisi hali halisi ya Rufiji inahitaji msaada wa Serikali. Ninaunga mkono hoja. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa juhudi zao za kusukuma maendeleo. Kwa kweli hawa Waheshimiwa wametuonyesha njia kwamba hatuhitaji umangimeza. Wamekuwa mstari wa mbele siku zote kujaribu kupita huku na huko kwa ajili ya kuweza kuhimiza na kuhamasisha maendeleo. Kwa kweli, niwaponggeze kwa hilo na nadhani ni mfano. Hatuna muda wa kukaa maofisini sasa hivi wakati tunaweza tukafanya maamuzi hata kwenye *field*. Tunazo *Laptop* na vitu vingine vya kuweza kutusaidia kuweza kutoa maamuzi mahali popote tunapokwenda.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia katika hoja hii hasa baadhi ya sehemu mojawapo ikiwa ni ile sehemu inayohusu ada za ndege. Sasa, ada za ndege kutotozwa kodi, hapa mimi ninachanganyikiwa kwa sababu sijui hizi ni ndege ni *locally owned* au ni *foreign owned*. Ningelipenda kupata ufafanuzi juu ya suala hili kwa sababu isije ikawa ndege hizi kumbe sio zetu, hakuna anayemiliki ndege hizi, isipokuwa ndege hizi zinamilikiwa na watu wa nje. Kwa hiyo, ningependa niweze kupata ufafanuzi juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kitu cha pili, mimi sioni uhusianao kati ya vitambulisho vya uraia na Watanzania kudhibiti maliasili yao. Hicho kifungu na mimi ningependa kiweze kufafanuliwa, kwa sababu sielewi hivi vitambulisho vina uhusiano gani na kudhibiti maliasili.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, suala la *tax invention*, kwa kweli hili suala limekuwa sugu kwa sababu kila kukicha tunasoma. Sasa, hii ya kupeana *option, fine,* au kifungo basi iende kwa watu wale wa kwanza, kama ni kosa la kwanza, la pili. Mimi nafikiri kwa wale ambao ni sugu na wale ambao wamekiuka viwango vikubwa, kusiwe na *option*, ni kifungo. Wapewe adhabu ya kifungo ili waweze kuhakikisha kwamba hawakwepi kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, *issue* ya mafuta imekuwa faraja kwa wengi na kila mtu anazungumza hilo ya kwamba huenda kutakuwa na matumaini. Nadhani kutakuwa na matumaini, isipokuwa sasa tutafanya nini kuhusu watu hawa *distributors* ambao wao kila siku ni kufikiria *super profit*? Sasa sijui Serikali itachukua hatua gani katika kuhakikisha kwamba wana-*affect controls* zinazohusika ili *at the end of the day* ziweze kushuka!

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho ningependa kuchangia ni suala la kuimarisha suala la usalama. Kwa kweli nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Usalama wa Raia kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kwa kweli juhudi zinaonekana na inaonyesha wazi kuwa palipo na nia, pana njia. Kweli kabisa hakuna Wizara ambayo imekuwa ngumu kama hii. Ameshika nafasi katika wakati mgumu kabisa na bahati nzuri matunda yanaanza kuonekena, kwa sababu sasa hivi tunaanza kwenda kuchimba mizizi kabisa yenyewe na hao watu *they are on the retreat*, mimi ninavyoona.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nadhani nia ya Serikali basi imeonekana hapo na sehemu zingine, Wizara zingine na Sekta zingine tuweze kuhakikisha kwamba tunaiga huo mfano, tuweze kukabiliana namatatizo haya.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho ningependa kuchangia ni suala la ufufuaji wa Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa. Jeshi la Kujenga Taifa kama jina linavyosema, ni Jeshi la Kujenga Taifa. Sasa, haya ni maoni yangu mwenyewe, mwingine anaweza kutofautiana na mimi lakini ninachosema, kwa nini Jeshi la Kujenga Taifa katika wakati wa amani tuliweke chini ya Wizara ya Ulinzi? Kwa sababu nilifikiri hili Jeshi hili lingewekwa chini ya Wizara ya Kazi na Ajira, halafu ikawa *job creation*, Wizara ya Kazi na Ajira. Sasa yakawepo Makambi ya hawa kuwafunza mafundi mbali mbali; mafundi mchundo ku-*supplement effort* za *Vocational Training.* Sasa hii Wizara ya Ulinzi, basi zenyewe zingeweka *inputs* za kupeleka watu pale kwenda kuwafundisha masuala ta *discipline*, masuala ya uzalendo, halafu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenyewe iweke *inputs* za Walimu.

Mheshimiwa Spika, nadhani ingekuwa hivyo kwa sababu sioni umuhimu wa Jeshi hili kuendelea kuwepo chini ya Wizara ya Ulinzi. Kwa sababu sisi tuko kwenye amani, Ndio, wenzetu wana matatizo, lakini panapohitajika tuna matatizo, basi italazimu kwa vyovyote sisi wote ni Jeshi la Mgambo, *we are the Reserve Army*, hakuna mtu ambaye hajapitia Jeshini hapa. Lakini, nilifikiri hawa watu wangepewa mafunzo ili waweze kujiajiri. Tatizo ni kwamba, tunapoliweka kule, kinachokuwa *insisted in discipline* na uzalendo. Sasa, wanapokuja kukosa ajira, maana inabidi waondoke, *after a while*, inabidi waondoke. Wanapokosa ajira ni hatari kushawishika kuingia kwenye masuala ya ujambazi na wana *knowledge* ya ku-*operate* hizo silaha na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba labda Serikali ingejaribu kuangalia kwamba hii ingewekwa. Kwa kweli Wizara ya Kazi na Ajira ni Wizara nyeti sana sasa hivi, ni kama Wizara ya TAMISEMI kama nilivyosema, ni Wizara nyeti kwa sababu tunataka kuleta *speed* ya maendeleo. Nilikuwa nafikiri hilo lingekuwa wazo langu tuweze kusaidiana kupeana ushauri kwenye suala hilo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia katika suala lingine la utalii. Sekta ya Utalii bado haijawanufaisha wananchi. Hii mirahaba ya asilimia 25, bado ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, ninakotoka mimi, wakina mama wanalala visimani, katika *Game Reserves* hizo. Wanasikia ndege tu zinakuja zinatua, zikishatua wale wanashuka

wanakwenda kwenye *hunting plots* zao, wanawinda. Wakiishamaliza kuwinda wanaondoka. *These people are in abject poverty.*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi nafikiri labda tungehitaji wataalam wetu waainishe ni kiasi gani cha misaada tunataka jamani. Kwa sababu tunaweza kuwa tunaomba pesa, sasa pesa zenyewe zinakwenda kutibu labda nilinganishe na mtu anayeumwa Malaria, anakuwa *diagnose* pale anakutana na Malaria badala ya kupewa *full doze* vidonge vya Fansida vitatu ameze wakati huo huo yeye anayaambiwa meza moja, kingine leo, kingine kesho kutwa. Kwa hiyo, utakuta ni kila mwaka tunakufa. Mimi nadhani labda sijui watushauri lakini mimi nadhani Serikali ingekaa kwa kina tujue kiasi hasa tunachohitaji kwa sababu ni miaka nenda rudi tatizo la maji liko pale pale. Miaka nenda rudi barabara zetu ziko pale.

Mheshimiwa Spika, wito wangu ni kwamba, tungejua hasa na hawa wanaotusaidia waelewe hasa masuala ya msingi, kama suala la maji, barabara, kwenye masuala ya shule, *of course* tunakwenda vizuri sasa hivi. Lakini ninadhani tungejaribu kuwasaidia wananchi. Akina mama wanalala visimani. Sasa mama wa namna hiyo atafanya maendeleo saa ngapi?

Mheshimiwa Spika, nichangie pia kwenye suala lililojitokeza juzi hapa katika Bajeti, suala la vinywaji baridi. Sasa suala la vinywaji baridi ni kweli kwamba vimepandishwa mbadala ya vinywaji baridi nayo ni chai ambayo nayo sukari imepandishwa bei. Sasa sijui tunywe nini sasa? Maana huku kwenye bia ndiyo kukali zaidi! Mimi nilifikiri labda tungeweza kushawishi watu waondoke huko wajaribu kuona kama wanaweza kuja huko maana bei ikiwa kali watu wanaweza ku- *opt out,* sasa wanakwenda mbadala wanakuta nako kule ni kukali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, soda tunanunua Shilingi mia nne mpaka mia tano, hii itakapokuja sasa itakuwa elfu moja. Sasa hiki ni kinywaji cha watoto, cha watu wazima, sasa sielewi tufanye nini. Lakini mimi ningeliomba hili suala liangaliwe ili tuweze kuona tutafanya vipi ili kuweza kurekebisha bei ya hizi soda.

Halafu suala la pili, ni suala la simu za mikononi. Inawezekana wenzangu wamezungumza, lakini mawasiliano ni muhimu. Kwa hiyo, nadhani hakukuwa na haja wakati huu. Wakati wenzetu kule Vijiji sehemu ambazo hakuna mitandao lakini wananunua wanatoka wanakwenda kutumia sehemu nyingine na wanatumaini kabisa kwamba tuweze kusambaza mitandao. Sasa kama hii inashindikana kumudu, sasa hivi tutakapoongeza ndiyo watashindwa kabisa. Mimi naomba hili suala nalo liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho napenda kuchangia ni suala la ubinafshaji. Mimi naomba kitu kimoja, kwamba tumekuwa tukizingatia zaidi raslimali fedha, rasilimali majengo. Lakini rasilimali watu tumekuwa tukiweka pembeni. Kwa kweli imekuwa ni habari ya kusikitisha sana katika baadhi ya Mashirika. Nikitoa mfano, tuna jengo la *Tanzania Motors Services,* liko jirani hapa, wafanyakazi wao walijitahidi kwa jasho lao wamejenga *infrastructure.* Walikuwa na majengo ya biashara 19

wakaambiwa na Serikali kwamba bwana mjenge mengine na wakajenga. Walikuwa na Mikataba yao *Tanzania Motor Services* ilizaliwa kutokana na *Redtop Motor* pamoja na *motor* ya maji wakawa na Mikataba yao. Lakini wakati wa kubinafsisha hii, hawa watu Mikataba yao iliwekwa pembeni na ikabidi iwalipe kama *terms* ambazo zinahusu Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ningeomba Waziri anayehusika ajaribu kuliangalia hili. Wako barabarani, wana kesi sasa hivi ilikuwa Mahakama Kuu, imerudishwa hiyo kesi sasa iko *labour*, ni miaka karibu karibu sita sasa na kuna *law of limitation act* ambayo ikifika muda kesi inafungwa. Mimi naomba suala hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, barabara zetu kama nilivyosema hapo awali mimi natoka Wilaya ya Manyoni Magharibi. Barabara muhimu miaka yote ambayo imekuwepo ni barabara ya Itigi Mbeya, wazee wote waliopo hapa ambao wamesoma Shule kutoka Nyanda za Juu Kusini walikuwa wanakwenda Tabora, wanakwenda Mwanza, wanakwenda Bukoba kusoma. Umuhimu wa barabara hii huwezi ukaelezea. Lakini mara baada ya kujengwa barabara ya lami ya Morogoro, ile barabara ilisahauliwa kabisa na ikaja kuwekwa msumari wa mwisho baada ya kufa *East African Road Services.* Lakini barabara ile ina umuhimu kwa sababu pale rasilimali nyingi zipo, kuna mbao hakuna asiyejua, kuna asali na n'ta, kila mtu hapa anaelewa umuhimu, kuna *game reserve. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasikitika kusema kabisa kwamba katika miaka yote ya *game reserve* hakuna Waziri wa Maliasili ambaye amefika pale. Kweli kabisa! Sasa sehemu yenye rasilimali kama hiyo imesahauliwa. Mimi ningeliomba kabisa kwamba pamoja na majibu, *actually* nilimuomba Waziri wa Miundombinu, alinijibu barua, ni nzuri, lakini kuna kipengele kilichoandikwa kwamba ikitegemea kulingana na hali ya fedha. Unajua hili neno huwa ni kukwepa au unakuwa *deferred indefinitely* maana utajibiwa vizuri lakini mwishoni unakuja kuambiwa lakini kulingana na hali ya fedha. Sasa hii kulingana na hali ya fedha...

Mheshimiwa Spika, naunga mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Vile vile, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mwibara kwa kuniheshimu na kunichagua niwawakilishe katika Bunge hili. Vile vile, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Zakia Meghji na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa kwa kutayarisha Bajeti nzuri inayolenga kuimarisha uchumi wetu na kuwaondolea wananchi wetu umaskini. *(Makofi)*

Vile vile, naomba kuwapongeza Watendaji wao Wakuu walioshiriki kuiandaa Bajeti hii. Pamoja na uzuri wa Bajeti hii, naomba nami nichangie haya yafuatayo:-

Kwanza, ugawaji wa rasilimali *(allocation of funds).* Nilipokuwa nikipitia katika Bajeti hii nimeona kwamba kuna matatizo kidogo katika ugawaji wa rasilimali. Kwa

mfano nikiangalia sekta isiyo rasmi *(informal sector)*, Sekta hii inachangia karibu asilimia 30 ya pato la Taifa kwa mwaka. Sekta hii imeajiri vijana wengi sana ambao ndiyo wanaiendesha na wanaitegemea. Lakini vile vile sekta hii ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu kwa sababu sekta iliyo rasmi inategemea sana sekta ambayo siyo rasmi. Kwa bahati Mheshimiwa Waziri wa Fedha hakusema katika Bajeti yake kimetengwa kiasi gain ili kuendeleza sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta nyingine ni Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo ni muhimu. Sekta hii imeajiri karibu asilimia 84 ya wananchi wetu. Vile vile, sekta hii inachangia kwa mwaka karibu asilimia 45.6 ya pato la Taifa. Kwa kweli kama tuko *serious* katika kuondoa umaskini au kufanikisha MKUKUTA, ni vyema rasilimali nyingi na kubwa tuelekeze katika kufanikisha sekta hii. Sekta ya Kilimo ikishafanikiwa, maana yake ni kwamba, tutakuwa tumeondolea umaskini wananchi wapatao asilimia 84. Kwa hiyo, nafikiria kwamba ni muda muafaka sasa hivi Serikali kuchukua hatua za makusudi za kuiboresha sekta hii kwa kuwezesha wakulima kupata nyenzo za kulimia za kisasa na bora. *(Makofi)*

Mikakati iliyopo sasa hivi, naona kwamba siyo sahihi, ni sawa na kumuua nyuki mmoja mmoja badala ya kwenda kumuua Malkia ambaye anazaa hawa nyuki. Kwa hiyo, tukitaka kuondoa umaskini, ni vyema tupeleke rasilimali zetu katika kilimo kule Vijijini ili tuweze kuondokana na umaskini. (*Makofi*)

Ugawaji mwingine wa rasilimali nauona katika miradi ya maendeleo. Ugawaji huu haujali tofauti zilizopo za maendeleo na uchumi katika sehemu mbalimbali. Kwa mfano katika tafiti za hivi karibuni zimeonyesha kwamba Wilaya ya Bunda ndio Wilaya masikini katika Wilaya zote za Tanzania. Lakini ukiangalia ugawaji wa fedha kwa Wilaya ya Bunda, imepata fedha sawa sawa na Wilaya ya Mbeya ambayo imeonekana kwamba ni Wilaya tajiri kuliko zote Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nafikiria tunapokuwa tunagawa rasilimali, basi tuangalie hizi *independent researches* ambazo zimefanya utafiti ili tuweze kutoa rasilimali zetu kwa uhakika na kule ambako tunaona kwamba kweli ni muhimu kupeleka hizo rasilimali zetu.

Ugawaji mwingine uko katika Wizara na Halmashauri. Ukiangalia katika Bajeti yetu ya mwaka huu asilimia karibu 74 ya fedha zote zimekwenda kwa Mawaziri, asilimia 18 peke yake ndiyo imepelekwa katika Halmashauri zetu za Wilaya. Sasa ukiangalia mwenendo wa sasa hivi ni kwamba, Halmashauri zetu ndiyo zimepewa dhamana ya kusimamia na kuendeleza miradi katika Vijiji vyetu. Kwa hiyo, nilikuwa naona kwamba ni vyema sasa badala ya kuacha fedha nyingi katika Mawizara, kununulia *furniture* na kuweka vitu vingine vya anasa, ni vyema sasa fedha ziende Vijijini zikafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano mmoja. Wizara ya Kilimo, ambayo ndiyo inasimamia kilimo nchini, katika Bajeti ya mwaka huu imetengewa kiasi cha Shilingi bilioni 45 kwa ajili ya shughuli za maendeleo, lakini imetengewa zaidi ya bilioni 77 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kwa kweli hii haiendani na kule ambako tunataka kwenda.

Ni vyema fedha kwa ajili ya maendeleo zingekuwa nyingi kuliko fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Katika ile Wizara utakuta kwamba imetenga kutumia Shilingi bilioni 3.4 katika mpango wa *SELF*. Huu ni mpango ambao unatoa mikopo midogo midogo. Vile vile, imetenga kutumia Shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya *TASAF*. Lakini Wizara hiyo hiyo imepanga kutumia Shilingi bilioni 11 katika mfumo wa ufuatiliaji wa umaskini Tanzania.

Vile vile nikumbushe hadithi ya ndugu zangu Wapare ya kuuza ng'ombe kumpata mbuzi. Mimi nilitegemea bilioni 11 ziende kwenye kupambana na umaskini na labda fedha kidogo ndiyo ziende katika kufuatilia kuona *impact* ya hizo fedha zimefanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mipango amezungumzia mipango mizuri ikiwa ni pamoja na umwagiliaji maji. Amesema kutakuwa na umwagiliaji maji katika sehemu nyingi, lakini sijaona hata sehemu moja mradi mmojawapo wa umwagiliaji kandokando ya Ziwa na sehemu zote zenye maji. Sasa nashangaa ni vipi hii miradi itafanikiwa kupeleka umwagiliaji maji ambako hakuna maji wakati kwenye maji ndiyo tungeanzia, Serikali inakuwa inapata kigugumizi. Sasa nilikuwa nashauri kwamba ni vyema umwagiliaji maji kwanza tuanzie katika maeneo ambayo yako karibu na maji, kando kando ya Ziwa Victoria kwa mfano, Mwibara, Bunda, Mwanza, Bukoba na sehemu nyingine kama Kigoma ambako kuna maji mengi ili tuangalie ufanisi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nimeona kwamba ni muhimu lakini hatukulipatia umuhimu unaostahili, ni elimu ya juu. Nchi nyingine nyingi zimeendelea kutokana na elimu kuwa nzuri. Sisemi kwamba hapa hatuna Vyuo vizuri, tuna Vyuo vizuri sana, lakini *we must look for the best education wherever it is*, tutafute elimu nzuri kokote inakopatikana. Wenzetu katika nchi zilizoendelea kama za Mashariki ya Mbali kama *Indonesia, Taiwan* na *Singapore* kila mwaka zinapeleka maelfu ya wanafunzi kusoma katika Vyuo vingine vya nje. Hawa wanafunzi wanapohitimu wanarudi na elimu nzuri, wanarudi na teknolojia ambayo inawasaidia kujenga uchumi na nchi ambazo zinahusika. Nchi nyingine ambayo inapeleka wanafunzi wake kwa wingi nje ni nchi ya Botswana. Nchi ya Botswana ina mpango ambao kila mwaka inapeleka vile vile maelfu ya wanafunzi katika nchi nyingine ili kuweza kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona ni vyema Serikali yetu ikachukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata elimu na ufundi unaostahili kuweza kupambana na hali halisi ya karne ya 21. Tukitegemea kujenga Vyuo hapa Tanzania ndio vijana wetu wasome, tutakuwa tumechelewa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iweze kuliangalia hili kwa mapana.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine naliona ni kwenye upande wa Miundombinu hasa upande wa barabara. Hakuna nchi ambayo itaendelea kama miundombinu yake hasa barabara ikiwa ni mibovu. Barabara ni kama zinakuwa ni *incentives* za kuleta maendeleo katika sehemu ambazo zinapitia. Nikichukulia mfano katika barabara ya kutoka Bunda

kwenda Ukerewe, katika barabara ya kutoka Bunda kwenda Nansio Ukerewe, barabara hii ni kiungo kikubwa sana. Kwanza ndiyo njia pekee ya kuaminika ya kusafiria kuwapeleka hata Visiwani kwao Ukerewe.

Kama alivyozungumza Mbunge mwenzangu hapa, alisema kwamba usafiri wa kwenda Ukerewe kwa kutumia *fast boat* haupo na kweli usafiri wa kwenda Ukerewe ni *unreliable*. Kwa hiyo, barabara hii peke yake ndiyo ambayo inatumiwa na watu wa Mwabira, na watu Visiwa vya Ukerewe. Sasa sio hilo tu, isipokuwa eneo la Mwibara na Ukerewe kwanza linazalisha mazao mengi ya chakula na vile vile mazao ya biashara kama Pamba. Sasa hivi ukiangalia samaki wengi sana aina ya sato wanazalishwa katika hayo maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sekta nyingine muhimu ni Sekta ya Afya. Sekta ya Afya nimesikia Serikali sasa itapeleka Kituo cha Afya katika kila Kata. Lakini katika Jimbo langu la Mwibara tuna hospitali kubwa ya Kibara, hii hospitali ni ya Wamisionari wa Katoliki. Wao wamesema wako tayari kuingia ushirika na Serikali. Sasa mimi naomba, badala ya kungojea tujenge majengo yetu, kuna majengo yako tayari katika Hospitali ya Kibara. Hivyo Serikali yetu iweze kwenda kuungana na hawa Wamisionari tuweze kupata huduma nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine muhimu ni usalama. Kwanza naipongeza Serikali kwa kuwaenzi Jeshi letu la Polisi na kuahidi kuwajengea mazingira mazuri sana ya kufanyia kazi. Lakini vile vile ningeomba sana Kituo cha Polisi cha Kibara ambacho sasa hivi kinafanya kazi katika kufanyia nyumba za wenyeji kiweze kupatiwa Ofisi rasmi, kipewe vitendea kazi kama vile nyumba, magari na mawasiliano ili kiweze kufanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine kila siku tunalalamika kwamba Mahakimu na Majaji hawatoshi, lakini na sisi tujiulize, tunawatendea haki? Je, hawa Majaji maslahi yao yakoje? Mimi nafikiri kwamba muda umefika, Serikali iwaangalie Majaji na Mahakama kwa ujumla kwa namna ya dharura waweze kuangaliwa maslahi yao kwa undani zaidi, tujaribu kutofautisha *professionals*, tusiangalie kwamba mbona wengine wanapata kiasi fulani, tuangalie kwamba hawa kazi yao ni ipi. Hawa Majaji wanahukumu majambazi, wanafanya kazi za hatari, lakini tunapokuja kwenye maslahi tunapata kigugumizi. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie upande huo wa Majaji na Mahakama kwa ujumla waweze kupata maslahi mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu cha mwisho ni ongezeko la *airtime* yaani *excise duty* ya *airtime*. Sasa hivi simu za mkononi siyo *luxury* ni *necessity*. Katika Jimbo langu la Mwibara hakuna *landline* hata moja, lakini nikihesabu wananchi wenye *mobile phone* ni maelfu. Vile vile tukiangalia miundombinu iliyoko kule, kwanza barabara hazipo, barabara siyo nzuri, vyombo vya usafiri siyo vizuri. Tukiongezea hii *excise duty* katika *airtime* maana yake tunaongezea gharama. Sasa gharama hii haitakuwa tu ni gharama ambayo tunakuja tena kuwaondolea fedha, kuwanyima mapato wananchi ambao tayari ni maskini na hawana njia nyingine ya kuwasiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia ya sasa hivi ni dunia ya mawasiliano na mawasiliano ya kisasa. Kwa hiyo, ningeomba Wizara ya Fedha, wapunguze kodi zaidi badala ya kuongeza. Kisingizio wanachotumia kwamba waweze kuainisha *excise duty* zetu pamoja na Kenya na Uganda, kwanza sio sahihi kwa sababu hatujafikia ile *level* ya *common market.* Tuko kwenye *custom union*. *Excise duty* ni *internal duties* ambazo haziko kwenye *level* hii. Sasa hivi ziko katika *level* ya baadaye. Vile vile mbona *VAT* ya kwetu hawakusema ipungue ilingane na za Kenya na Uganda? Kwa hiyo, naona hili ongezeko tutaongezea wananchi wetu gharama na hivyo ningeomba tutafute njia nyingine za kuongeza mapato yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni suala la kusimamia mapato vizuri. Kwa mfano ripoti ya *Auditor General* ya mwaka 2004/2005 imeonyesha kwamba karibu Shilingi bilioni 35 zimepotea katika mazingira ya kutatanisha. Sasa mimi nilifikiria kwamba, kwanza Waziri wa Fedha angekuja akatueleza hizi fedha atazipata vipi kabla ya kusema tuongeze tena kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo machache, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, nimearifiwa kwamba kwamba Mheshimiwa Dr. Chegeni hayupo na kwa bahati njema Mheshimiwa Nyalandu alikuwa Jimboni na ambaye alikuwa ni msemaji wa kwanza leo asubuhi, alipangwa hivyo, sasa namwona amerejea. Kwa hiyo, nampa nafasi hiyo sasa Mheshimiwa Nyalandu, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla wakati huo ajiandae Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge, wengine kuchangia katika Hotuba za Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili ambazo ni hotuba muhimu sana katika Bajeti yetu ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Chama cha Mapinduzi kuwaletea wananchi wa Tanzania, mmoja mmoja maendeleo ya dhati. Katika azma hii, ni azma ambayo siyo tu kwamba hawa Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi lazima waisaidie Serikali waiunge mkono na kuhakikisha kwamba inafikia malengo lakini ndugu zangu wa Kambi ya pili ya Upinzani wasisite katika kuhakikisha kwamba azma hii ya maendeleo ya kasi wanaiunga mkono kwa hali na mali ili twende kwa haraka. *(Makofi)*

Kuna mwimbaji mmoja ameimba wimbo anasema alikuwa anamwambia shetani nipishe nipite, nadhani huyu alikuwa ana safari na kuna mtu akawa anamchelewesha njiani. Kasi ambayo Mheshimiwa Rais ameizungumzia ambayo wote hapa tunakubaliana nayo ni kasi ambayo haitahitaji shetani yoyote atuzuie njiani, wala aizuie Serikali, wala amzuie mtu yeyote kupita ili wananchi wa Tanzania wanaotusubiri, wanaotuangalia matarajio yaweze kufikiwa. *GDP* ya Tanzania hadi kufikia sasa hivi ni wastani wa Dola za Kimarekani Shilingi bilioni tisa. *GDP* ya Kenya na ni Afrika Mashariki ni wastani wa Dola za Kimarekani bilioni 12. *GDP* ya Uganda na hao ni wenzetu ambayo tunajilinganisha kwa sababu ni Jumuiya ya Afrika Mashariki, *eventually* tunaungana siyo

tu kiuchumi lakini na kisiasa. Wao wako kwenye bilioni saba. Hadi kufikia mwaka jana 2005 *Kenya Revenue Authority* kama hii *TRA* yetu walikuwa wanakusanya mara mbili ya *TRA* ya Tanzania kila mwezi. Tanzania inategemea wageni *donors*, iwe misaada au mikopo kwa wastani wa asilimia 39. Waganda wao bado wako zaidi ya asilimia 50, lakini Wakenya wanategemea hawa jamaa wageni kwa chini ya asilimia tano. Hiyo, inaitwa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, pasipokuongeza tija katika kuzalisha mali, watu wafanye kazi, kila mtu afanye kazi kwa muda mwingi, masaa mengi na kwa kasi zaidi, nchi hii haiwezi kufikia malengo na matumaini ambayo tunataka tuyafikie. *(Makofi)*

Siku moja ina masaa 24 na naomba niulize swali. Mtanzania kwa wastani anafanya kazi masaa mangapi? Yale masaa nane ya kazi ni masaa mangapi watu wanaweza wakawa wamekaa wanapiga zogo, wanapiga *story*, wanapiga hadithi na masaa mengi yanatumika kwa Semina, Warsha na Kongamano? Muda ambao nchi hii inapoteza kwa kazi ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Factor* ya uchumi ili uweze kwenda kwa kazi ni lazima tuhakikishe masaa yote 24 watu wanafanya kazi. Ukienda *Nairobi Industrial Area, the most productive part of East African* watu wanafanya kazi masaa 24. Wakimaliza *shift* ya kwanza wanaingia *shift* ya usiku. Watu wanafanya kazi na ukirudi hapa Tanzania, lori limeandoka Dar es Salaam linakwenda Mwanza, jambo la kwanza Polisi watalisimamisha mara 1,000 kabla halijafika Mwanza. Rushwa ni adui wa haki. Rushwa haitaweza kuisaidia hii nchi maana imesemekana haki huinua Taifa lolote lile. Mtu anachukua matunda Morogoro anapeleka Dar es Salaam watamsimamisha mara 20! Kasi ya maendeleo inapungua kwa kiasi ambacho huwezi ukakitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi ikifika saa 12.00 watu wote wanapaki malori yao, wakati gari linakwenda Nairobi, linalokwenda Kampala, Kigali limechukua mizigo yake Mombasa linakwenda masaa 24. Ni nani amewaambia Watanzania itakapofika saa 12.00 watu wapaki magari yao? Kama ni hali ya usalama, ninaomba niwaulize *planners* wa nchi hii mmepanga Shilingi ngapi zilinde nchi ya Tanzania ili wananchi wa Tanzania wasafiri mchana na usiku? Nani alikwambia Wachina uchumi wao unakua asilimia tisa na kuendelea ikishafika saa 12.00 wamelala? Nani alikwambia Wajapani inapofika saa 9.00 jioni, nani alikuambia? Ni nchi gani ambayo watu wake ikishafika saa 12.00 wote wamelala na unategemea uchumi huu ukue zaidi ya asilimia sita na inapofika masaa 12 wote, *the whole country comes to an ostensive*, ni lazima *planners* wa nchi hii wafikirie ni fedha kiasi gani zinahitajika kuilinda nchi hii, kulinda barabara zetu zipitike. *(Makofi)*

Kazi ya Serikali ni kulinda raia na kuhakikisha mali zao zote ziko salama, *productivity* hii, zote ziko salama! *Productivity EPZ* tunaianzisha, naunga mkono lakini kama *infrastructure* haijatengenezwa, wenzetu wa Kenya wataendelea kuwavutia wawezekeji tu. Sisi tumekuwa marafiki na Wachina miaka mingi sana. Tanzania imewaunga mkono Wachina miaka yote katika Umoja wa Mataifa kuhusu *One China Policy*. Tumewatetea Wachina na wamekuwa ndugu zetu, wamejenga barabara.

Lakini *for the first time the Chinese* wanakwenda kuifanya Mombasa *port* kuwa *regional hub* kwa ajili ya nchi zote za hapa kuchukua siyo tu madini, dhahabu, mafuta, yatakayochimbwa na kupatikana yanapelekwa China. Maana yake ni nini? Ni *infrustracture* ya Mombasa ita-*double.* Maana yake nini? Barabara inayounganishwa Mombasa na nchi nyingine zote kwa *competition* ita-*double*. Maana yake ni nini? Nchi kama Rwanda, *DRC, Uganda,* wata-*prefer* Mombasa zaidi kwa sababu ya *infrastructure* ambayo Wachina wata-*invest*.

Mimi napenda niulize *capability* ya Bandari ya Tanga kama ingewekewa fedha ina uwezo wa kuimeza Bandari ya Mombasa na Wakenya wataisikia redioni. Mimi naomba niulize wakati Wakenya wana-*rob* na mtu mmoja aliniuliza, Watanzania wangapi wanaongea Kichina? *Economic espionage* zinafanyika kwa sababu nchi nyingi zimepeleka vijana wao wakajifunza Kichina. China ni Taifa ambalo linakwenda kuitawala. Dunia muda siyo mrefu na wote wanajua, Wamarekani wanajua. Wamarekani wamepeleka vijana wao wajifunze Kichina, sisi tumepeleka wangapi? *Planners* wa nchi hii mko wapi? Mnafikiria nini juu ya hii nchi? Mnafikiria karibu au mbali kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kasi ya kukua kwa uchumi kama tukiweza kuongeza kwa kadri tunavyoweza, nchi hii tukifanya kazi kwa masaa 24, kila barabara ya Tanzania ilindwe, mtu aweze kusafiri kwa *bus* kutoka Mwanza aje Dar es Salaam na siyo kulazimika kupitia Nairobi, usiku na mchana malori yasafiri, Polisi wawapishe hawa wafanyabiashara wadogo wadogo wawapishe njiani wapite tutaweza kukuza uchumi wetu. Rais Jakaya Mrisho Kikwete anasema ni kasi na mtu anasimamishwa mara 20 na ninawaomba wote wanaohusika wawapishe hawa watu wapite. Kasi ya uchumi ikiweza kukua mara mbili, nchi hii itatisha. Sasa hivi sisi tunafanya *reserve order,* tunachukua baadhi ya fedha ya *reserve* tunaziweka kwenye Bajeti kwa sababu hatujawa na fedha zaidi za kuongeza kwenye *reserve.*

Kama tukiongeza masaa ya kufanya kazi *as a function of economic development productivity,* tunachoweza kufanya kila mwaka Mheshimiwa Waziri wa Fedha atatuambia mwaka huu ninaweka kwenye *reserve* bilioni 200 tutapiga makofi. Ninajua Serikali inaanza kazi sasa hivi, sisi Waheshimiwa Wabunge tutajitahidi kuwaunga mkono. Lakini ninachowaomba ni kwamba wale *Planners* mnakokaa huko muangalie mbele zaidi ya miaka 50 kwa sababu *we are in competition,* huwezi ukaniambia mmeamua kwamba mpandishe bei ya *airtime simply* kwa sababu Wakenya wamefanya hivyo. *Those guys have the cheapest of everything.* Mafuta yao ni *cheaper.* Ndege nyingi zinatoka Ulaya zinaweka mafuta Kenya. Wamehakikisha kwamba anapokuja Kenya atafaidi *cheaper rate*, *hotel rates* zao ni *cheaper*. Hapa sisi wamekuja watu kila kitu wanachaji kwa *Dollar,* ni nchi gani utakwenda dukani mtu akwambie hii redio ni *dollar* 100 ngoja nikupigie nikupe bei ya Shilingi ngapi. Kwa nini msiwapige marufuku watu kuchaji *Dollar* wachaji Shilingi na kama ni *Dollar* walipe *equivalent* ya *dollar? (Makofi)*

Nchi hii ni mali ya nani? Azimio la kasi mpya, litawahitaji *Planners* wa nchi hii tuungane mkono na Wabunge ninatumaini azimio la kuhakikisha kwamba nchi hii

*planning* haifanyiki siku moja kesho ikabadilishwa. Anatokea mtu leo anasema tujenge nyumba za Serikali, Viongozi wakae *Oysterbay,* anatokea mwingine kesho analipuka anasema hizi nyumba tuziuze. Keshokutwa anakuja anasema tunaomba tununue nyingine, tujenge nyingine. *There must be planning,* hii ambayo naizungumzia ni lazima iwe *planning* ambayo tunaifanya, tunaizungumza na hatuibadilishi. Nchi isitawaliwe nusu siku. Nchi itawalike masaa 24, *productivity* iongezeke na tuhakikishe kwamba tunachoweza kukifanya sisi letu ni moja. Naomba nichukue nafasi hii kwa wenzangu wa Upinzani.

Upinzani unafanyika wakati wa kampeni tu. Naomba niwaambie wenzangu Waandishi wa Habari, unapokuwa na uzalendo unaandika habari ambazo zitakuwa na maslahi na tija ya nchi. *(Makofi)*

Watu wanapofanya *research* juu ya Tanzania, waangalie *productivity* iko wapi. Kila kitu kiko wapi, wanaangalia mnaripoti kiasi gani. Inaweza ikatokea historia ya jambazi ikaandikwa mara mia moja. Watu wanaanza kufikiri kwamba Tanzania ina ujambazi mwingi sana, kumbe kumetulia. Watu wanaandika habari za rushwa, wanaweza wakaandika habari za rushwa mara milioni moja na ikawa *exaggreted.* Nasema hakuna nchi iliyoendelea ambako waandishi wake waliacha kuwa na uzalendo na tutailinda hii nchi pamoja. Waandishi wa Habari andika habari zako sawa sawa. Lakini hakikisha unaitendea haki nchi ya Tanzania kwa sababu ni ya kwako wewe na watoto wako. *(Makofi)*

Mbunge atakaposimama kutetea hoja kama unaipinga hoja hakikisha unaipinga kimaslahi. Wakenya hawa bwana wanatengana tu hapa, lakini inapofika kwenye suala la maslahi ya Kenya wanakwambia wanaungana, hawawajui, wala hawaijui Jumuiya ya Afrika Mashariki, wala babu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima ninaomba nimalizie hoja na nijiweke wazi kwamba naiunga mkono hoja hii. Ninaiomba Serikali katika majumuisho, ituhakikishie kwamba katika suala la *planning* itabadilika na kwamba suala la *planning* ikiwezekana liongeze wadau wengi kila nchi kitu kinaitwa *think tank.* Tuna Watanzania wengi sana wana akili zao, wana uzoefu wamekaa kule. Tuwaite, tuwatumie. Kwa nini kila kitu tunawaita Wazungu? Tunawaita ma-*consultant* wanapewa mapesa! Mngewaita hapa ndugu zetu waliopo hapa hapa na *experiences* zao tukaungana, *we would take this country forward*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa nafasi hii na mimi naomba kwa niaba ya wananchi wa Singida Kaskazini niseme kwamba tunaiunga mkono hoja hii ya Serikali na niseme kwamba tutaendelea kuungana na Serikali kuhakikisha kwamba kila mahali ambako kuna bonde linasawazishwa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwekezaji kama zilivyowasilishwa. Aidha, nawapongeza Mawaziri hawa na timu ya Wizara zao nzima kwa kuandaa hotuba ambayo tuna hakika kwamba zitaendana

na kasma yetu ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya kwa kukidhi matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba pia kuchukua fursa hii kuwapa pole wale wote waliopoteza maisha na kuwapoteza ndugu, jamaa na marafiki zao kutokana na ajali mbaya iliyoua watu 54 Mkoani Arusha na Manyara hivi karibuni. Naomba sote tuungane kumwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema na kuwaombea wale wote walioua au kujeruhiwa uponaji wa haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuchangia maeneo matatu tu ya hotuba zote mbili. Eneo la kwanza, ningependa kutoa mchango wangu katika suala zima la MKUKUTA Tunaelewa kuwa huu ni Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi ambao utasaidia kupunguza umaskini. Sasa umaskini wa Taifa letu unatofautiana baina ya jamii na jamii kwa sababu naamini kwamba umaskini wa wananchi wa Dar es Salaam au wa Arusha Mjini ni tofauti kabisa na umaskini wa Vijiji vya ndani vya Mkoa wa Manyara.

Wataalam wa kupima vigezo vya umaskini kama umaskini wa Kati, umaskini uliokithiri wanaelewa kabisa kwamba vigezo hivyo ndivyo vinavyosababisha kuweka nchi yetu ama kui-*rank* nchi kuwa ya tatu ama ya nne kutoka mwisho kuwa nchi maskini na mwenzetu mzungumzaji aliyepita sasa hivi ameifafanua kwa upana kabisa kwamba sisi Watanzania ni nchi maskini na nadhani tutatafakari zaidi mazungumzo ambayo alituasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vigezo hivi vya kupima umaskini vya Taifa letu ndiyo inapelekea ku-*rank* nchi yetu kuwa ya pili ama ya ngapi kwa umaskini. Mimi nashauri kwamba Bajeti yetu ya mwaka 2006/2007 iweze kuongezwa zaidi katika suala hili zima la MKUKUTA ya kupunguza umaskini. Lakini ikizingatia maeneo ya vipaumbele jinsi ambavyo nilielezea kwamba umaskini katika nchi yetu umetofautiana baina ya jamii hadi jamii. Nina hakika kwamba katika nchi yetu sasa hivi hakuna kabila ambalo linaishi kwa mfano kwa kutumia au kwa kutegemea mizizi, ama kuwinda wanyama wadogo wadogo, ama kuvaa ngozi, ama vigezo kama hivyo ndiyo vinapelekea kupima nchi kwamba nchi hii ni maskini na ina watu maskini na umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali inapotekeleza mikakati hii ya MKUKUTA ni vyema basi ikaweka vipaumbele vya maeneo ya kuanzia ikizingatia umaskini wa nchi ya jamii zake na kwa ajili hiyo kwa jinsi ambavyo nilitaja Mkoa wetu wa Manyara bado una makibila yanayotegemea kuishi kwa kula mizizi na kwa kuwinda wanyama wadogo wadogo na kwa kuvaa ngozi kama watu wa zamani sana. Sisemi kwamba ngozi ni vazi baya.

Mheshimiwa Spika, vazi linapokuwa vazi la kudumu basi nadhani wananchi kama hao wana haki ya msingi kabisa ya kupewa maendeleo na kuweza kulengwa ili nao waweze kufaidi maendeleo kama hayo na kwa ajili hiyo basi, ningeiomba Serikali iweke vipaumbele maeneo ya kuanzia kwa ajili ya kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Mimi ningeomba katika utekelezaji wa MKUKUTA suala zima la kuwezeshwa wananchi kiuchumi usiwe kipaumbele. Mara nyingi

imetamkwa suala la kuanzishwa *SACCOS* na nadhani wengi wetu tumesikia hapa kila Mbunge anataka kuhakikisha katika eneo lake limeanzisha *SACCOS* ama mradi wowote wa kuweza kuwawezesha watu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nina hakika kwamba katika Mikoa mbalimbali haikosi Wabunge kuanzia watano, sita, kumi hadi kumi na tano katika Mikoa fulani, na kila Mbunge anategemea kwamba, kwa jinsi ambavyo nimesikiliza tangu tulivyoanza mijadala hii na jinsi ambavyo imehamasishwa kwamba kila mahala watu wahamasishwe kuanzishwa kwa *SACCOS* ama mikakati ya aina fulani ya kuanzisha ukopeshwaji kwa wananchi. Lakini angalizo ninalotaka kuwaeleza WaheshimiwaWabunge wenzangu ni kwamba kama kila Mbunge katika eneo lake ataanzisha *SACCOS* atamlenga mwananchi mmoja mmoja na kama kila mtu ataleta *SACCOS* ama ataleta mikopo ama suala lingine la kumkopesha mwananchi hususan wanawake, mama mmoja atalengwa na aina ya mikopo kama miwili, mitatu.  Sasa ninachotaka kusema ni kwamba, unapompa mwananchi mkopo zaidi ya mmoja ukamhamasisha kwa mbinu mbalimbali ya mikopo zaidi ya mmoja, nadhani badala ya kumnyanyua, atadidimia kwa sababu atashindwa kulipa mikopo zaidi ya mmoja.

Kwa hiyo, nilitaka kuweka angalizo hilo kwamba tunapolenga wananchi wetu, basi tusiwalenge wananchi kuwalundika mawazo ya mara moja ama mikakati ya mara moja, tuwe na sehemu ya mipango ama maeneo ya kuweza kuanza kitu kingine kipya. Kukianzishwa *SACCOS* Kijiji kimoja, basi sehemu nyingine iwe aina moja ya kumlenga mwananchi ili na yeye asiweze kuchanganyikiwa katika kufuatilia mawazo yale ambayo anapewa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba katika maeneo yetu tuna Taasisi mbalimbali ambazo zinawawezesha wananchi kiuchumi.  Mimi nadhani ni vizuri Serikali hasa Wizara ya Mipango na Uwezeshaji Uchumi ikaratibu shughuli za Taasisi hizo mbalimbali kwa sababu ninaelewa kwamba kuna Mashirika kama *Pride Tanzania, Thinker Tanzania* ambayo inatoa mabilioni ya fedha kuwawezesha wananchi kila mwaka,  Lakini katika kupima vipato vya watu wetu wananchi hususan wanawake mara nyingi Serikali inaangalia ile mikopo ya Shilingi milioni nne ambayo wanapewa Halmashauri na ambayo nina hakika urejeshaji na utekelezaji wake sio wa makini sana.  Kwa hiyo, isingekuwa vizuri labda kutumia kigezo cha mikopo kama hiyo, kupima vipato ambavyo vimeweza kuinua maisha ya watu Vijijini.  Ni vizuri ikaratibu pia shughuli za Taasisi nyingine za fedha.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la ueleweshwaji wananchi. Mimi nadhani ni vizuri kipaumbele katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 itaelekezwa zaidi katika kuinua uelewa wa watu zaidi na kujenga mazingira yale ambayo yanawawezesha watu kuweza kukopa.  Kwa mfano, nadhani sio vyema ikaanzishwa haraka haraka suala zima la kuwawezesha watu kiuchumi wakati kuna matatizo makubwa ambayo ni ya kipaumbele kwa mfano suala zima la maji.  Sina haja ya kuelezea umuhimu wa maji Vijijini.  Suala zima la umeme limezungumziwa sana, sio vizuri nikalirudia.  Lakini kama alivyoeleza mwenzangu, pia suala la *economic empowerment* ni suala ambalo linatakiwa.

Unapomwezesha mtu kumwinua kiuchumi kwa mfano anatakiwa afanye biashara, sasa kama suala la biashara atafanya mchana tu saa 12 amekwenda kulala itakuwa ni kazi ambayo siyo endelevu. Kwa hiyo, tungependa kipaumbele iwe nishati ya umeme Vijijini ili watu waweze kufanya kazi kwa muda mrefu zaidi, masaa mengi zaidi kuliko ambavyo mtu anafanya kazi saa za mchana peke yake. Suala la maji hususan kwa akina mama lipewe kipaumbele kabisa liweze kushughulikiwa katika Vijiji hasa Vijiji vile ambavyo viko pembezoni ambayo imezungumziwa kwa kirefu sana.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo ningependa kuzungumzia pia kwa kifupi ni suala la wafugaji. Kwa sababu mimi natoka maeneo ya wafugaji na hususan wanawake wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanawake wafugaji wasisahauliwe vile vile kuwezeshwa kiuchumi. Nao wana rasilimali zao ambazo ni za asili, wanaweza wakafanya kazi na biashara nzuri ambayo licha ya kuinua vipato vyao, itainua pia kipato cha Taifa. *(Makofi)*

Jinsi ambavyo Wizara ya Mifugo ina mikakati yake mizuri kama tulivyosikia, mimi nadhani tungeshauri wafugaji wawezeshwe ili waanzishe mashamba ya nyasi kwa ajili ya mifugo yao, suala ambalo lingeweza kuwasaidia kupunguza kuhamahama na kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa Kaskazini Unguja, nachukua nafasi hii kutoa shukrani kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti yetu hii ya kwanza tokea Watanzania kukirudisha Chama Cha Mapinduzi madarakani kwa kukipa ushindi mkubwa wa kishindo na tunasema ahsante sana na mwaka 2010 wembe kuliko ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nielekeze mchango wangu katika maeneo yafuatayo:- Mazingira. Tanzania tumekumbwa na janga kubwa la uharibifu wa mazingira na hii inatokana na mambo mawili makubwa. Moja, ni hali ya umaskini tuliyonayo. Watu walio wengi wanaona kuwa maisha yao na kipato chao kinategemea mazingira yaliyowazunguka. Ndiyo maana tunaishambulia miti, tunaikata, tunachoma mkaa, tunauza na kwa vile wateja wapo katika soko, hali hii itaendelea hadi hapo nishati mbadala itakapoweza kupatikana, kwa sababu wateja watanunua nishati nyingine badala ya hiyo ambayo inauzwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni uelewa mdogo wa Watanzania walio wengi juu ya mahusiano ya uharibifu wa mazingira ya maisha ya viumbe hai ambayo ni binadamu pamoja na mifugo, vile vile na uchumi wa nchi yetu. Kwani hawaelewi kuwa wakikata miti wanasababisha kukosekana kwa mvua na ndiyo ukame unatokea na hatimaye kutokea kwa janga la njaa.

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Serikali kwa juhudi kubwa iliyofanya kwa kushughulikia janga hili la njaa. Lakini vile vile hii ni elimu tosha kwa wananchi ya kuelewa kuwa uharibifu wa mazingira ndiyo kwa sehemu kubwa uliosababisha tatizo hili la njaa.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali vile vile kwa kutenga fungu ambalo litashughulikia utunzaji wa mazingira na hatua ambazo zimechukuliwa za kupunguza kodi katika baadhi ya bidhaa kama vile mitungi ya gesi. Vifaa vya umeme wa jua, *solar ernegy* pamoja na kupandisha kodi kwa mifuko ya plastiki, mifuko ya plastiki imekuwa kero! Lakini kwa kufanya hivi, itapungua kuingia nchini na itapungua kununuliwa kwa sababu itakuwa ni ghali na pengine itatoa nafasi ya ile mikoba na vikapu vya wazee wetu kule Vijijini navyo kuweza kupata soko. *(Makofi)*

Lakini vile vile kutawawezesha wale wenye uwezo wa kiasi fulani kutumia gesi na wengine kununua vifaa vya *solar* na kuweza kutumia. Lakini kubwa zaidi ni lile kutengwa fungu la kupima maeneo ya wafugaji. Tunaelewa kuwa wafugaji au wachungaji hawa wa kuhamahama ndiyo waharibifu wakubwa wa mazingira hasa katika vianzio vya maji. Lakini hatuwalaumu sana kwa sababu tumesema kuna uelewa mdogo walionao. Nao akilini mwao, imezungumzwa hapa kwamba ng’ombe ni utajiri. Ngo’mbe wengi ni alama ya utajiri ijapokuwa alama ile ya utajiri haionyeshi katika maisha halisi ya yule mwenye wale ng’ombe.

Kwa maana hiyo, kwa kuwatengea maeneo pengine picha hii inaweza ikabadilika. Kwa sababu badala ya kuona ni ng’ombe tu wako mbele wanaweza wakaona na mengineyo. Ilikuwa ngumu kuwaambia ondokeni mahali fulani mnaharibu mazingira lakini bila kuambiwa muondoke hapa, muende wapi? Lakini kwa kutengewa maeneo wanaweza wakakubaliana na Serikali kuwa ondokeni hapa mnaharibu mazingira, mnakosesha Watanzania walio wengi umeme, mnakosesha Watanzania walio wengi maji. Lakini mhame hapa nendeni eneo hili hapa mmeshatengewa, mtaendeleza maisha yenu pamoja na maisha ya ng’ombe wenu.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la mazingira nilikuwa nina ushauri ufuatao:- Kwanza, elimu ya mazingira iendelee kutolewa. Najua inaendelea kutolewa, lakini iendelee kutolewa kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Ili kila Mtanzania iweze kumfikia na sasa aelewe kuwa athari ya kuharibu mazingira ni moja, mbili, tatu, nne.

Pili, Serikali iendelee kwa nguvu zote kutafuta nishati mbadala kwa sababu hili litakuwa ni jibu la kupunguza kukata miti.

Mheshimiwa Spika, Kamati za Mazingira ziweko katika kila Kijiji na katika kila kitongoji. Tunaelewa kuwa katika baadhi ya Vijiji na Miji hizi Kamati zipo na hapa napenda kuipongeza Kamati ya Mazingira ya Mji wa Tanga ambayo imeweza kusimamia kidete utunzaji wa kianzio cha maji ya Mto Sigi ambao umetokea katika milima ya Usambara. Kwa maana hiyo, inawezekana kama kila mmoja akijitahidi kushughulikia hili jambo.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ni kuanzishwa kwa Kodi ya Mazingira. Kuna watu wanaharibu mazingira na wanakwenda hivi hivi tu. Kwa mfano kwenye sehemu ya Migodi wanaharibu mazingira, mashimo yapo pale! Sasa Serikali ingeanzisha hii kodi ya mazingira angalau kile kipato kinachopatikana kikaweza kutumika pale pale katika kutunza yale mazingira ya pale. Vile vile kuna malori makubwa yanapita yanaharibu tu barabara. Kwa hiyo, kuwepo angalau na *onmental text* ambayo inaweza ikasaidia vile vile kupatikana kipato cha kuweka mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa tatu, kuandaliwe mpango mahsusi wa ku-*restore*, kurudishia mazingira ambayo yameshaharibika. Umeshawaondoa wafugaji, umeshawapeleka katika maeneo mengine, pale utafanya nini? Inabidi pale kuwe na mikakati madhubuti ya kurudisha hali ya mazingira mazuri yaliyokuwepo ili kuondoa ile athari ambayo tayari ilikwishakutokea.

Halafu ushauri mwingine wa sita katika eneo hili ni kutayarisha mashamba darasa kwa wafugaji wa kienyeji, kama imewezekana katika upande wa kilimo kwa hiyo, itawezekana pia na katika upande wa wawafugaji. Watateuliwa watu wachache watakaopewa ile elimu, watafundishwa namna ya kuanzisha yale mashamba ya darasa ya kilimo ya ufugaji na wao wanaweza wakafuga vizuri.

Mheshimiwa Spika, ni hili eneo la ustawi wa jamii. Hili nimelichanganya katika maeneo mawili. Huduma za jamii zimepandishwa fungu lake mpaka asilimia 18.7. Lakini katika huduma za jamii kuna elimu, afya na maji. Wenzangu wamekwishakuja kueleza hapa matatizo ya elimu, matatizo ya afya na matatizo ya maji. Kwa hiyo, hapa Tanzania upande wa afya, madaktari ni wachache mno. Daktari mmoja anahudumia zaidi ya watu 30,000. Hii ni sawa sawa na kusema kuna wananchi walio wengi tu hawapati huduma nzuri za afya za Madaktari wanaohusika. Kwa hiyo, Waziri wa Elimu alikuja kutueleza mkakati wake wa kuongeza Walimu. Labda na Wizara ya Afya itakapokuja ije ituelezee mkakati wake wa kuongeza Madaktari.

Lingine ni uwezeshaji kwa kutoa mikopo. Hapa naipongeza *NMB* kwa kazi nzuri inayofanya ya kutoa mikopo kwa wafanyabiashara ndogo ndogo na kwa wafanyakazi. Kwa kweli ule mkopo unasaidia sana wafanyakazi kufanya mambo yao mengine mbali ya matumizi ya chakula tu.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya nyumba. Watanzania kwa kweli hatuna nguvu za kujenga kwa kutumia fedha zetu, ndiyo maana wengi bado wanatanga tanga tu, hawana pa kuishi. Umemaliza Shule miaka 25 umepata ajira miaka mitatu unatafuta kiwanja. Unajenga tofali moja moja miaka 20 miaka 48 ndiyo unaweza kuingia kwenye nyumba na tumeambiwa hapa maisha ya Mtanzania ki-a*verage* labda miaka 43. Kwa hiyo, unajenga nyumba ambayo wewe mwenyewe hutaikaa. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha hii mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakwenda mbio mbio muda umeniishia. Lakini nataka kuzungumzia kuhusu uchumi wa Zanzibar. Zanzibar ni uchumi mdogo, ni uchumi wa Visiwa. Vianzio vyake vya mapato ni finyu mno. Kwa maana hiyo, mapato

yanayopatikana ya ndani hayawezi yakatosheleza yale mahitaji ya ukuaji wa uchumi na kuleta maendeleo ya nchi. Maana inafika wakati inabidi mikopo kutoka nje na misaada ambayo ni mambo ya kimuungano yanahitajika katika ku-*finance* shughuli zake.

Sasa hapa kwa vile mambo haya ni ya Muungano ni lazima kuwe na mkakati mahsusi wa kuweza kusaidia upande wa pili kama ikileta maombi yake kutaka udhamini wa Benki Kuu mambo yaende haraka haraka, siyo yawe yanachukua muda mrefu mpaka kupata *approval* na kupelekwa kwa Wafadhili.

Kwani kuna ubaya gani kama Zanzibar ikiandaa programu yake, inajua programu hii itahitaji elfu *billion Shillings* na huku Bara programu ile ile ya sekta hii inahitaji *Z billion shillings* ikiunganishwa pamoja ikipelekewa kwa Wafadhili kuombewa fedha kama *package* moja na ikifika hapa itakuwa tena ya mgao 4.5 wakati hii tayari imeshapitwa na wakati**.** Kwa maana hiyo, ukirudi ule mradi kutoka kwa ufadhili, ukipata ufadhili tunajua X ni ya Zanzibar moja kwa moja na Z ni ya Bara moja kwa moja. Kwa hiyo hakuna *formula* ile ya 4.5, na *formula* ya 4.5 imeshapitwa na wakati. Kwa hiyo, tunaiomba hii Tume ya pamoja ya fedha ikae iandae *formula* ambayo itakubalika na upande wote ambao haitaleta matatizo itakubalika kwa pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hizi Bajeti za hawa Waheshimiwa Mawaziri wawili. Kwanza kabisa, naomba nianzie na upande wa Bajeti ya fedha ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Mama Zakia Meghji. Kimsingi naipongeza sana na naiunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

Nimefurahishwa sana na wananchi wa Ruvuma, ninauhakika wamefurahi kwa sababu Bajeti hii imezingatia sana hali ya mama. Naweza kusema ni Bajeti ambayo imezingatia *gender* kwa upande wa akina mama. Pia, Bajeti hii inazidi kusisitiza kwamba uwepo wa kinamama katika sehemu nyingi za maamuzi ndio suluhisho la matatizo ya wananchi Watanzania. Pamoja na shukrani hizo, pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa Kasi Mpya anayoifanya, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wake wote, nikizidi kukumbusha kwamba ile ngao iliyoko pale mbele yetu, ambayo inamwakilisha baba na mama Wamasai inanikumbusha kwamba tunadaiwa kuwa na asilimia 50 kwa 50 akina mama na akina baba. Vilevile inazidi kusisitiza utendaji mzuri wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoka umasaini, unalenga kwenye Kasi Mpya. Kwa hiyo, tutaendelea kuwapongeza. *(Makofi)*

Lakini pia inatukumbusha kwenye uumbaji wa dunia, kwamba Mwenyezi Mungu alipomuumba Adamu, akaona ajatosheleza kuwa peke yake, kwa hiyo, akasema awekewe msaidizi na akachagua msaidizi kuwa mwanamke. Kwa hiyo, naamini asilimia 50 kwa 50 itafikiwa kwa kuwa Chama cha Mapinduzi kama Chama Tawala kina dhamira ya dhati na ninaamini hata kule Upinzani nao wanaunga mkono. Kwa hiyo, tutaifikia hiyo asilimia 50 kwa 50. *(Makofi)*

Naomba niongelee hasa kuhusiana na tatizo la Bajeti hii ninavyoiona mimi, na uchangiaji ambao tayari umeshafanyika mpaka sasa hivi. *Percent* kubwa tunazungumzia hasa kuongezewa, kutengenezewa barabara, sio magari na mambo kama hayo. Lakini tusirudi nyuma kwamba sisi kama Watanzania tunao wajibu wa kufahamu kwamba tunapochota maji ndoo inapungua, kwa hiyo, lazima ijaziwe. Kwa sisi wanasayansi tunaamini kuwa sehemu yoyote ile iliyochukuliwa nafasi lazima kuwe na ujazo wake, ndio nadharia ya mada. Kwa hiyo, kupungua kwa kiasi kile kilichokwenda kwenye kupunguza kodi lazima kijaziwe katika maeneo mengine, ndio maana tumeona mapungufu hayo mengine ambayo yanatugusa pia. Lakini ni vizuri sana tukaangalia ni jinsi gani tutaweza kujazia ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa kama mjasiriamali na Serikali yako Tukufu ambayo pia naona imekaa kiujasiriamali katika kutimiza malengo yake na Waheshimiwa Wabunge ambao pia naona ni wajasiriamali, kwa sababu wajasiriamali wanakuwa wana kiu ya mafanikio, wajasiriamali wanathubutu, wanachukua *risk* lakini lazima ziwe ni *risk* ambazo zina mahesabu ndani yake. Pia, kwa wale wenzetu Wahasibu kuna suala la *Profit and Loss Account*, lipo sasa tumesikia hapa taarifa nyingi zipo kwenye Bajeti zetu zinazozungumziwa hasara mbalimbali zilizotokea. Lakini tukiangalia upande wa kundi kuu ambalo wakati wa uchaguzi ndio tulikuwa tunalitumia sana kuliomba kura, kundi la kinamama na kundi la vijana, tunao vijana wengi sana ambao hawana ajira na wamerudi kuwa ni mzigo kwa akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ziara yangu niliyopitia katika mashule, nimegundua kuwa pia katika kuangalia vijana ili waweze kuchukua hatamu ya uchumi, hata watoto wa Shule wako tayari kuendeleza uchumi wa nchi hii hata kwa kujitafutia hata ada zao. Lakini tumezingatia sana kutaka kuwawezesha kwa njia ya mikopo. Nimeangalia Bajeti hii inazungumzia zaidi wafanyakazi waongezewe maslahi, lakini ajira zetu tumezitafsiri katika aina mbili. Kuna ajira zile za Serikalini na kwenye Mashirika na kuna ajira ambazo ziko katika Sekta Binafsi.

Sasa hizi Sekta Binafsi hazikui kwa sababu kodi za wale ambao wamejitosa kwenye Sekta Binafsi tunazitumia kuboresha maslahi ya wafanyakazi ambao wako kwenye Sekta za Umma. Lakini hawa wadogo zao sasa ambao wanatakiwa kuikuza Sekta ya Biashara kwa mfano, au ya Kilimo, hawawezeshwi, badala yake wanawekewa masharti magumu na kuambiwa kwamba wapewe mikopo. Kwa nini sisi kama wajasiriamali tusitenge kwa mfano bilioni kama 10 hivi tukasema potelea kwa mbali mwaka huu tutachukua *risk* tuwawezeshe hawa watu wetu kwa kusema kwa mfano kila Mkoa vijana angalau 1000 au 2000 wapewe mikopo ya 200,000 isiyo na masharti magumu ili waweze kuanzisha shughuli zao?

Tumeshaongea na vijana, tumeshaongea na akina mama na utafiti unaonyesha wazi kuwa tunaolalamika hawarudishi pesa ni hawa wakopaji wakubwa wakubwa ambao ni wachache. Hao wadogo wadogo ambao wana nia ya dhati ya kuendesha mahitaji yao binafsi hatuwawezeshi, tunasema mpaka wakopeshwe. Matokeo yake tunasema *GDP* ni ndogo, matokeo yake tunasema kwamba hakuna uwezekano hata wa kupata mkate.

Lakini mimi nadhani ni uwongo. Tukienda kule Vijijini, wao hawawezi kupimwa kwa mkate, watapimwa kwa kande au maharage wanayokula.

Kwa hiyo, nafikiri tunajirudisha nyuma sana kwa kuzidi tu kusema uchumi wetu uko nyuma kiasi kwamba tunaogopa kwamba sisi ni maskini sana lakini hatujawa na huo umaskini wa kiasi cha kushindwa kulipa kama tutawezeshwa kianzio. Tupewe *revolving fund* watu waweze kupata angalau Sh.200,000/= au laki moja kwa wale ambao tayari tumeshaona wana mipango ambayo ni thabiti tuwape mwaka mmoja. Ni uhakika pesa zote zitarudi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kwa upande wa uchumi, katika miradi inayozungumzwa, nadhani tuwe na *target* sasa ya kuangalia tunazingatia mradi upi ambao tukiufanya utakuwa na *impact* kubwa kwa Watanzania, badala yakuendelea tu kuwa na mipango mingi ambayo ni ya hadithi za Abunuwasi. Kwa mfano mara ya mwisho nawashukuru Waheshimiwa baada ya kwenda katika *forum* ile ya *SADC Parliament* nilikuja kuona kwamba Msumbiji nchi ambayo imekuwa ikipigana siku zote imeweza kuwa na kiwanda kikubwa sana ambacho naamini Tanzania hatuna. Kiwanda kile ambacho kinahusika na usafishaji wa chuma kinachangia *percent* saba ya *GDP* ya nchi nzima. Kinakula umeme *megawatt* 900 sawa na matumizi mara tano ya nchi nzima, ni sawasawa na matumizi ya Tanzania mara mbili.  Vile vile, kile kiwanda kinaweza kuchangia milioni mbili na nusu US$ katika *social activities*.

Mheshimiwa Spika, kuna miradi kama mchuchuma, tunasema umeme, sawa. Kuna umeme wa gesi upo tunategemea tutapata kutoka Kiwira, kutoka Songo Songo, lakini mradi ule wa mchuchuma kama tutapata *serious investor,* nasema *serious investor* akaweza kuwekeza katika mradi ule tukapata umeme, hata kama hautafika Dar es Salaam au maeneo mengine, tayari mlaji yuko pale ambapo pana chuma cha Liganga na chuma kile kina sifa kwamba sio sawa na chuma cha kawaida, ni sawa na kusema unachoma mninga.  Kama utaamua kutumia kama chuma cha kawaida ni sawa kwa kuchoma mninga kwa ajili ya mkaa. Chuma kile kina *vanadium* na *titanium.* Wataalam wetu waliobobea wako *NDC,* lakini hatuwazungumzi hapa, wanaonekana kama hawajafanya kazi yao, kwanini tunajisahau tunazungumzia matumizi hatuzungumzi miradi ya kutuzalishia? Naomba tuzingatie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie upande wa *TANESCO. TANESCO* tutailaumu, lakini *TANESCO* tuipongeze, ni Shirika peke yake ambalo limeshindwa kuuzika kutokana na utajiri wake. Naomba kwanza tuwapongeze ndugu zanguni.  Kila mtu anapozungumza hapa umeme Vijijini anaizungumzia *TANESCO*. Lakini kuna matatizo ya maamuzi.  Kwa mfano maamuzi yaliyofanyika ya kuhitaji umeme wa *IPTL*, mimi binafsi nasema yalikuwa mazuri kwa sababu tulikuwa na matatizo ya umeme na ninyi wenyewe mmeshuhudia bila zile *megawatt* 100 kutoka *IPTL* tusingefika hapa. Lakini tatizo kubwa ni jinsi gani ya ku-*bargain* bei za kuweza kununua, pale ndio kulikuwa na matatizo, na mara nyingi sana tumekuwa na maamuzi ambayo yanaingilia katika shughuli za kiufundi, ilimradi mtu amewaza jambo fulani, basi analipeleka bila hata kulifikiria zaidi.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri kwamba turudi sasa katika kila watu na fani zao tuwape nafasi waweze kutenda ili yale yanayoamriwa yawe ni mambo ambayo ni ya usahihi na yanakubalika. Kwa upande wa *TANESCO* wafanyakazi wenzangu mnanisikia huko mliko, tuondoe ubabaishaji, hali halisi sasa hivi wenzetu wamebadilika, tujitahidi tumsaidie mtendaji wetu pale inapohitajika. Lakini hata ukuaji wa *TANESCO* umekuwa *horizontal*, sio *vertical* kwa sababu una *activities* nyingi zinazohusiana na *TANESCO*. Kwa nini kusiundwe chombo kingine kitakachoshughulikia tu umeme Vijijini? Hawa *TANESCO* tukawaachia yale majukumu mengine wanayoendelea nayo. Mimi nadhani tuangalie uwezekano wa kukarabati lile Shirika ili badala ya kuwa na lawama tuweze kufaidika nalo.

Baada ya kuzungumza hayo, napenda kusema kwamba nashukuru kwa kupata nafasi hii na naiunga mkono Bajeti hii na nazidi kuwaomba wananchi tuchukue majukumu yetu ya kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi hii utajengwa na nchi hii, utajengwa na sisi, sio kama *sacrament* utapewa tu mdomoni. Tusiwadanganye wananchi wetu, tunasema Serikali itafikia mahali watu watashindwa kufanya shughuli zao kwa kuamini kwamba kila kitu wataletewa.

Mheshimiwa Spika, hii chachu ya Bajeti tuliyopewa ikatumike vizuri katika kuhakikisha kwamba wananchi wetu inawezesha katika kusonga mbele kiuchumi. Wananchi wa Ruvuma wako tayari wameshajipanga na miradi yao, Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha na wale vijana kule mlituomba tukawahamasishe, wapo tayari, tunaamini hamtatuangusha kule Ruvuma mtapeleka ile *Revolving Fund* na wananisikia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nalazimika kuwasomea kanuni ya 53 (c) kwa sababu kumekuwa na ukiukaji wa mara kwa mara wa kanuni hiyo, hususan katika mjadala huu. Kanuni ya 53(c) inasema hivi: “Mbunge aliyepo Bungeni wakati wa mjadala hatapita baina ya kiti cha Spika na Bunge anayesema.” Lakini pia labda nisome na 53(b), nayo wengine wanaikiuka. Kanuni ya 53(b) inasema: “Mbunge aliyepo Bungeni wakati wa mjadala, atatulia na kukaa kwa heshima mahali pake na hatatangatanga katika Ukumbi wa Mkutano bila sababu.” Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, atafuatiwa na Mheshimiwa Phares Kabuye na ninadhani kutakuwa bado na muda, atakayefunga dimba kwa leo ni Mheshimiwa Victor Mwambalaswa. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nami nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Ludewa walioniwezesha kuja hapa, wakawa wameniamini kwamba nitasimama kidedea, nitawatetea masuala yao na tutawasaidia kuhakikisha kwamba maendeleo ya Wilaya ile yanapatikana.

Pili, nitoe pongezi kwa safu nzima ya uongozi wa Serikali kuanzia Rais Kikwete, Waziri Mkuu, Mawaziri na sisi Wabunge kwa kuanza vizuri kufanya kazi ambazo wananchi wanategemea tuzifanye.

Tatu, niwapongeze Mawaziri wawili ambao wametuletea hoja hapa ambazo tunazijadili, ni hoja nzuri na mimi napenda sasa kutoa mawazo yangu. Katika kutoa mawazo yangu nitajikita zaidi kwenye masuala ya Jimbo la Ludewa kwanza, halafu nikipata muda nitazungumzia masuala ya jumla.

Mheshimiwa Spika, nianze na mpango unaopendekezwa na Waziri wa Mipango na kuna kipande pale cha misingi na malengo ya mpango wa muda wa kati. Natambua vilevile na wengi mmesoma kwenye magazeti, mmeona kwenye TV, kwamba Waziri wa Nishati na Madini alikwenda Ludewa, aliongea na wananchi kwenye Mikutano mikubwa tu na akaahidi kwamba miradi ya Liganga na Mchuchuma itaanza mara moja. Katika kipindi hiki cha miaka mitano lazima iwe imeanza, ndivyo alivyowaambia wananchi wa Ludewa. Nilichoshangaa ni kwamba katika mpango wa kati, ndugu yangu Mheshimiwa Ngasongwa wala halitaji! Haukutajwa kabisa Liganga wala Mchuchuma! Sasa labda tu nilidhani nieleze kidogo hisia za wananchi wa Ludewa.

Mimi nimezaliwa nasikia habari ya liganga na mchuchuma mpaka nazeeka. Kuna waliozaliwa, wamekufa, hawaoni matokeo ya kukaa na chuma kile na mkaa ule, wanauliza; kulikoni? Kwa nini haya madini hayachimbwi? Watu wanazaliwa, wanakufa ,wanayaacha. Kwa nini na umasikini umejaa kwenye Wilaya?

Sasa watu wa Ludewa wanasema hivi, miradi ile ni mikubwa sana, ni kweli inahitaji Wawekezaji wakubwa sana. Kama hilo limeshindakana miaka yote hii, migodi ile igawanywe kwenye vitalu, wapewe wawekezaji mbalimbali. Hiyo itawezekana kwa sababu haihitaji fedha nyingi sana, lakini vilevile italeta mashindano, kati ya Wawekezaji. Tukiwa na mashindano na wawekezaji, itachochea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, watu wa Ludewa ni laki moja na *point* mbili tu. Miradi ile ikianza, kwa sababu ni watu wachache, faida itakayokwenda kwenye Halmashauri na Wilaya pale ni kidogo sana kwa sababu watu wachache ni kama ajira. Kwa kweli ni Wilaya zinazozunguka na Mikoa inayozunguka *Mtwara Corridor* na Taifa ndio litafaidika kwa ajili ya uchumi pamoja na ajira. Sasa najua hatuwezi kuanza safari hii pengine hatukuweka hela, lakini ingetajwa, kwa sababu tupo katika mpango wa kati mpaka mwaka 2005 hii miradi itaanza kutekelezwa. Hilo tu ndio nililokuwa naomba Ndugu Ngasongwa.

Ukija kwenye miundombinu Mheshimiwa Waziri wa Fedha anazungumzia kuhusu *resources* zetu kwamba ni kidogo sana. Lazima tuzi-*concentrate* tuzipeleke maeneo machache ambako kutakuwa na mapato makubwa na itawavutia Wahisani wengi. Sasa nashangaa kwamba kilichofanya Wilaya ya Ludewa iwe masikini na kwa kweli haipitiki, Wabunge waliokwenda wa Kamati ya Uwekezaji ni mashahidi ina utajiri lakini ina ufukara mwingi sana. Lakini nani atakayetujengea hizi barabara? Mimi nilidhani tunaweza kwa makusudi kabisa kama Serikali kuamua tuanze basi kuwekeza katika barabara katika *infrastructure* wakati miradi hii itakapoanza sijui mwaka kesho au mwaka huu kama anavyosema Waziri wa Nishati, *infrastructure* fulani fulani zipo. Lakini haitajwi, hakuna kinachoendelea wala hakuna wazo hata la kufikiria kuanza kuweka barabara. Barabara zenyewe kutoka Mabanda mpaka Mchuchuma au mpaka

Liganga haifiki kilomita 50, kutoka Madaba ambayo kuna barabara ya lami. Kutoka njia panda Mabanda mpaka Mchuchuma hazizidi kilomita 100, ni kilomita chache sana.

Tungeweza kwa makusudi kabisa tuka-*invest* katika kutengeneza miundombinu pale ili wawekezaji hao wavutiwe ili waweze kuja kuwekeza pale. Lakini sisi wote tunakaa tunasubiri mpaka mwekezaji aje lakini hatu-*invest* kwenye miundombinu, haitawezekana! Haitatokea! Mimi ushauri wangu nilidhani tungeweka hata kwa kuanzia tu, nasema kwamba basi tutaweka hela kidogo, tutaanza kidogo kidogo kilomita mbili, tatu, nne mwaka hadi mwaka ifikapo baada ya miaka kumi barabara ile itakamilika na itawavutia wawekezaji.

Nilikuwa naomba tu hili, Mheshimiwa Waziri wa Mipango huko huko Ludewa, nizungumzie kidogo tu nichepuke kwenye upande wa mwambao. Kule kuna meli nyingi *MV Songea* na *MV Iringa.* Meli zile ni chakavu kweli kweli! Sasa hivi inafika katikati ya mawimbi na Ziwa lile ni kati ya Maziwa ambayo yana dhoruba kali katika Ukanda wa Maziwa Makuu na mtakumbuka mwaka 1977 meli ya *MV Mbeya* ilizama Makonde, kwa sababu ya dharuba. Vyombo vile sasa hivi vinafika mahali vinazima katikati ya Ziwa na watu maisha yao yanakuwa katika hatari. Inawezekana Waziri wa Miundombinu hajawahi kufika kule, hajawahi hata siku moja kuangalia ratiba inafuatwa.

Baada ya hapo nitumie muda kidogo kuzungumzia juu ya Sekta ya Kilimo. Ndugu zangu, wengi wamezungumzia habari ya kilimo, tunasema tunataka kilimo cha kisayansi. Mimi pale Chuo Kikuu nilikuwa nafundisha mambo ya *sustainable development* na tunasema kwenye kilimo nchi zilizoendelea kuna *Agro Ecological Zones.* Kisayansi tunasema, pale tutalima hiki kwa sababu udongo, mvua na hali ya hewa inaruhusu ndio kigezo. Hakuna sababu nyingine, ni sisi Tanzania sijui kwa nini miaka nenda, miaka rudi mahindi yatalimwa kila mahali, kila mahali tunapeleka pembejeo, kila mahali tunapeleka wataalam.

Kwa nini tusichague na Wabunge wengi wamesema tuchague maeneo machache, kama Mikoa ya Nyanda za Juu ina hali nzuri ya hewa, ina udongo mzuri, ina mvua ya kutosha tuna uhakika pale tukipeleka pembejeo na mbolea hizi za ruzuku tu-*concentrate* pale tupate mavuno ya uhakika. Inawezekana! Nashukuru kwamba Waziri wa Kilimo ni mtu wa huko Nyanda za Juu, tunategemea kwamba ni suala tu la Wizara kuamua tuanze sasa kufuata *Agro Ecological Zones* hapa tutalima zao hili, huku tutalima hili, tukipata hela kwenye pamba watanunua mahindi kutoka Iringa, Mbeya na Rukwa, ndio utaratibu. Sio lazima wote tulime mahindi.

Kwa hiyo, mimi utalaam wangu ni kwamba tufuate *Agro Ecological Zones* zinasemaje na zipo. Nchi hii imekuwa *mapped* kwa *Agro Ecological Zones* na mazao yanayostahimili kila eneo yanajulikana. Kwa nini tusifuate hilo tukapunguza gharama za Serikali za kusambaza pembejeo kila mahali, Tanzania wataalam kila mahali, lakini matokeo yake hakuna kitu. Mimi hilo nilikuwa naliomba sana.

Mwisho kuhusu uchukuzi, Wabunge wenzangu wa Kusini wamezungumzia kuhusu Kiwanja cha Songwe. Ni kweli kiwanja kile kitakuwa *white elephant.* Wenzetu

kiwanja cha *KIA* na *DIA* vinategemea utalii, sisi utalii kule Kusini haujakuwa *developed*. Hatuwezi kutegemea kiwanja kile kitaendelea kwa utalii, haiwezekani! Kitaendelea kwa kilimo! Ni muhimu tuangalie *integrated road infrastructure* itakuwaje. Ile kupenyezwa kwa wakulima katika maeneo mbalimbali ya Nyanda za Juu kutepu mazao hayo iwe maua, mahindi, *whatever* yasafirishwe, mboga mboga kupeleka nje, ndipo kiwanda kitafanya kazi, la sivyo ni hasara tupu tumepoteza pesa. Kwa hiyo, naomba katika hilo tuweke hela mahali pamoja ambapo tuna uhakika tutazalisha. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo na kutokana na maangalizo niliyoyatoa, naunga mkono hoja lakini kwa asilimia tisini na tisa *point* tisini na tisa. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kusema machache, ingawa niliyokuwa nimepanga mengi yameshazungumzwa na sio vibaya sana nikiyarudia. Kwa kawaida mimi huwa nasifu mtu baada ya kutenda. Sasa kuna watu wawili ambao nitawapongeza na kuwashukuru sana.

Kwanza, napongeza sana watu waliopeleka kesi ya takrima Mahakamani, halafu napongeza Majaji waliotuondolea balaa ya takrima. Pia, naipongeza Serikali iliyokubali kwamba kweli takrima ilikuwa fedheha na ifutiliwe mbali. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Takrima ilikuwa fedheha, ilikuwa imelipeleka Taifa letu mahali pabaya, maadili yote yalikuwa yamemomonyoka. Leo hii na mnyonge maskini amepewa njia. Sasa hivi wanyonge wataweza kuwa Madiwani, wanyonge wataweza kuwa Wenyeviti wa Vijiji na kwa kweli nadhani Mwenyezi Mungu ameliona, nchi yetu sasa imeoshwa. Lakini wasibunibuni mengine yanayofanana na hilo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hongo ya wanasiasa huwa ni maendeleo. Ndiyo hongo nzuri na kwetu sisi hongo inayoweza ikawasaidia wananchi ni kuwaondolea kwanza ujinga; pili, maradhi; tatu, umaskini na hii ndiyo ahadi tuliyowaahidi wananchi wakatusaidia katika vita vya kumwondoa mkoloni. Je, sasa tegemeo lao limetimizwa? Hawana ujinga? Kwa nini ujinga haujatoka na huyu adui tulimfahamu miaka 45 iliyopita? Hivi kweli tunapigana vita na ujinga! Maana ilikuwa ndiyo adui wa pili. Hivi leo hii maradhi yamekwisha?! Umaskini ndiyo unaota mizizi, ujinga kwa kweli unajionyesha, maana huwezi ukaondoa umaskini kama wewe ni mjinga au ni mgonjwa, huwezi! Itakuwa ni ubabaishaji! Ninyi wenyewe mnaona watu wengi katika Tanzania wana elimu ya Darasa la Saba, lakini wameweza kujiondolea umaskini? Elimu tuliyowapa, imewasaidia kuondoa umaskini? Wanaona wenyewe!

Maradhi, mpaka leo Tanzania inapoteza akina mama wanaojifungua 8,000 kwa mwaka. Kwa miaka 10, si mauaji ya halaiki!! Watu wanasema eti sisi pingapinga hatusifu, hapana. Mazuri tunayasifu na mabaya tunayalaani. Kila siku akina mama 25 wanaojifungua, wanne wanakufa, halafu tusifusitu! Malaria ambayo inaweza ikatibika, mbu wanaweza wakawindwa wakapotea, lakini wanaua maelfu ya Watanzania, khe! Halafu tusifusifu hapa! Labda kama wanaokufa sio binadamu. Leo hii UKIMWI umekuwa ndiyo ugonjwa kwa sababu una Wahisani, ni kitega uchumi. Ndugu zangu wanasema hii sio kwa sababu ya kuokoa Watanzania, ni kwa sababu Wahisani

wanaangalia na wanatoa pesa kwa uchumi, ni kitega uchumi. Mbona Malaria inayoua zaidi ya UKIMWI hatuihangaikii sana? Ndugu zangu, kweli Bajeti hii sina matatizo nayo, lakini kazi yake lazima iwe kuondoa ujinga, maradhi na umaskini. Kwani ni nani wanaoondolewa maradhi? Nani wanaoondolewa ujinga ama umaskini? Wako katika tabaka mbili. *(Makofi)*

Tabaka la kwanza ni wakulima wanyonge wa nchi hii. Ukiwatafuta maskini wa kwanza hawawezi kutoka kwa wafanyakazi, bali wanatoka kwa wakulima. Mkulima kwa hospitali ndiyo anakaa kwenye mstari, lakini mfanyakazi utasikia ah! Bwana ingia halafu mkulima ndiye anakaa kwenye mstari. Hata ndani ya *bus* mfanyakazi ana kiti, lakini mkulima anashindiliwa na ngumi, sogea. Mkulima ana taabu katika nchi hii Ndugu zangu! Ana shida na taabu sana! Masikini hana lake katika nchi aliyopewa na Mwenyezi Mungu. *(Makofi/Kicheko)*

Kwanza kuwasaidia ni lazima tuwaelewe. Watu tunajifunza jiografia lakini tunabaki kubabaisha. Hivi kweli nani hajui kwamba Dodoma hata ungefanyaje haiwezi ikapata mvua kama Iringa? Hatulijui hili? Tunawasaidiaje hawa? Tunajua kwamba hata tukifanyaje Dodoma ni kame na kijiografia inaeleweka. Tunafanyaje miaka yote hii kukabili hili jambo? *Central Province,* hamjui hili? Tunakuja kufanyafanya baada ya kupigwa na njaa kana kwamba tulikuwa tumelala, sasa njaa inatuamsha.

Hivi wale Wakoloni waliokuwa wameweka visima vya *Windmill* vya kuvuta maji mlifikiri wajinga? Walikuwa wamechimba malambo, mlifikiri wajinga? Walijua ni lazima tujue Musoma ikoje, Singida ikoje, Kagera ikoje na tukishajua, mganga akijua ugonjwa wako ni sehemu ya kuutibu. Tukijua hali za watu wetu na ardhi yetu, itakuwa ndiyo mwanzo wa kuwasaidia. Tanzania ni *poor!* Niwaambieni *naturally* watu wasiwadanganye! Ni sehemu chache ambazo ni *fertile.* Dodoma ni *fertile* lakini ni kame, lazima tujue hayo. Lakini tunaanza kuwahangaisha. Sasa ni zimamoto baada ya njaa, ooh, vyanzo! Hivi vyanzo vya maji hamkujua tangu zamani? Mpaka njaa iwapige ndiyo mjue vyanzo? Yaani mpigwe kwanza ndiyo mjue mazingira yanaharibika! Mnalala usingizi wa vipi? Sasa hili nalo la vyanzo vya maji msipoliangalia itakuwa kero. *(Makofi)*

Kwa mfano sisi Kagera tuna mabonde, tunalima mara tatu. Tuna vuli, masika na kiangazi, tunakwenda mabondeni! Hayo mabonde Mjerumani amekuta yanalimwa, leo hii ni kero? Vyanzo vya maji vinachanganywa na mapito ya maji. Mtu analala kesho yake anakuta aha, hapa bwana ni chanzo cha maji. Maji ni yako wewe! Si uulize wenye maji! Maji yako wewe?! Tangu tuwepo, Serikali ilishahemelea watu maji. Ulizeni hapa, mnatoa wapi maji? Watakuonyesha chanzo, mshirikiane nao wenye maji, lakini tuwe na mipango na tujue nchi yetu na watu wake. Kwa hiyo, mipango iwe ya mapema. Vyanzo tushirikiane.

Mambo ya mazingira na miti, hivi mnafikiri miti ndiyo inayoleta mvua tu? Kama miti inaleta mvua, nadhani Tabora misitu ingekuwa na mvua kuliko Kagera na ninadhani Dodoma hii miti iliyopandwa kungekuwa na mvua sana. Hii ni *element* moja. Lakini hata hiyo miti ninyi mnafanyaje? Hivi kweli kama tangu mwanzo tungehimiza Kijiji

kiwe na shamba la miti, Kata iwe na miti, Tarafa iwe na miti, Halmashauri iwe na miti na Serikali iwe na miti, hivi kweli nchi yetu ingekuwa haikujaa miti? Sasa mnaona miti ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu ametupa haya mamiti ya porini, tutayakata! Mlie tu! *(Kicheko?Makofi)*

Ni nani amekwenda kukata mkaa kwenye mashamba ya Mufindi? Nani amekata mkaa kwenye mashamba ya Njombe ambako wamepanda wenyewe? Nani atakata kwenye msitu wa Serikali au kwenye msitu wa Kijiji? Hii misitu ya Mwenyezi Mungu utailindaje? Wewe Tabora, misitu itakugharimu na itakwisha. Hata Ulaya miti ya asili ilikuwepo ikaisha. Kwa hiyo, njia ni kupanda miti. Kila mtu apande miti. Serikali wana msitu, Tarafa wana msitu, Kata ina msitu, Halmashauri ina misitu, lakini mnahangaika hangaika na hii ya Mwenyezi Mungu, we!

Kwanza, mtu kukata mkaa ni dhiki. Hivi wewe unaweza ukakata mkaa? Unafikiri kukata mkaa ni lelemama! Huyu mtu anaamua kufa au kupambana na mti, hana pa kujifunzia, anakwenda kubahatisha, hajui utaanguka wapi! Mimi nimekata mkaa. Ni kazi kubwa kabisa kuangusha mti, kuuchanachana, kuupanga, sasa unalunda lundo na kulifukia halafu usiku unalala pale unakoka moto. Moto unakubabua huna hata maziwa ya kunywa. Wewe unafikiri nini? Ni shida! Watu wetu miaka 45 bado wanachoma mkaa. Hivi kweli wangelikuwa wamewezeshwa, wewe hiyo balaa ya mkaa unaweza ukachoma wewe? *(Makofi/Kicheko)*

Halafu kama mimi ningelikuwa na uwezo nikasema kwa muda wa wiki moja watu wote wasichome mkaa, hapa Dodoma hatuwezi kukaa. Wabunge tutapigwa hapa! Watu watafikiria nini? Ikulu haitakalika kama Dar es Salaam haina mkaa. Sasa tusifanye vitu kama vya kutambia, bali tufanye vitu kabisa tunavyovijua vinaweza vikasaidia watu, twende nao tuwawezeshe halafu wapande miti. Miti iliyopandwa na watu hakuna mtu atakayeichezea. *(Makofi)*

Halmashauri zetu siyo Halmashauri, ni Idara za Serikali, *Local Government* ambayo watu ni *imported.* Watumishi wote wale wenyeji hawana habari nao! Halafu unasema Halmashauri ya Ludewa wale Madiwani wasiwe kwenye ajira, wasiwe kwenye *tender*, yaani Msubi kutoka Biharamulo ndiye akae kwenye *tender* ya Mgogo, ndiye mwaminifu yeye kuliko Wagogo waliochaguliwa? Nini tunafanya hivyo?

Naomba dakika zilizomalizika muangalie wafanyakazi nao. Wafanyakazi wana taabu! Mshahara wa Sh. 61,000/=, hebu wewe Ndugu yangu Waziri Mkuu tukupe Sh.65,000/= ukae nazo wiki, haki ya Mungu utakufa! Huwezi ukamaliza wiki kwa Sh. 65,000/=, mke wako ale hizo, watoto wale na wewe ule hizo Sh. 65,000/=? Hivi watu mnaowafanyia hivi na wao si binadamu jamani? Sh. 65,000/= hawana nyumba! Naomba sana wasaidieni kweli.

Mheshimiwa Spika, Mahakimu hawana nyumba, wanapangisha nyumba. Wakiamua kushika mtu wa gongo, mwenye nyumba anasema kama ni hivyo bwana toka kwenye nyumba yangu. Hawafanyi kazi vizuri! Polisi nao hivyo hivyo! Sasa kwetu Mji

wa Biharamulo unageuka jangwa. Magereza hawana gari, ni kukata miti tu na kuweka kichwani. Jamani angalieni watu. *(Kicheko/Makofi)*

Mtu akistaafu, kupata kupata kiinua mgongo ni balaa. Anakwenda Dar es Salaam anakemewa! Mimi huwa nakwenda, si mnaona umri wangu! Nikivaa vibaya Ofisini hawanielewi! Nimeshatukanwa, mwisho naona hapa nikizidi kuficha nitapigwa. Najitambulisha. Mimi ni Mbunge bwana. Utasikia wanasema ooh, samahani sana. Nisingekuwa Mbunge! Watu tunawafanyia nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama nilivyosema, mengi wameyamaliza wenzangu, lakini naomba Polisi waangaliwe. Wana vinyumba aina ya msonge vilivyoachwa na mkoloni, sijui kama una mke na watoto wakubwa sijui mazungumzo mnayafanyaje! Jamani, jamani, mambo yanakwendaje haya? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, itakuwa sijamtendea haki Msemaji ambaye angefuata kwa sababu muda nauona hauwezi kumpa ile robo saa ambayo ni haki yake. Sio vizuri, kwa hiyo, Mheshimiwa Mwambalaswa ataanza kesho asubuhi.

Kwa sasa ninayo matangazo yafuatayo:-

Kwanza, kama nilivyosema, wakati nasitisha shughuli za Bunge pale asubuhi, kesho tuna mgeni mashuhuri, Rais wa Jamhuri ya Ireland, nchi rafiki sana kwetu. Rais huyo ataambatana na mwenyeji wake Rais wetu mpendwa Jakaya Mrisho Kikwete na watakuja hapa Bungeni saa sita kasorobo.

Mapokezi yameandaliwa, wafanyakazi wote wa Bunge watakuwa nje ya Ukumbi wakiwa na Bendera za Tanzania na Ireland kama ishara ya urafiki. Pale nje zitapigwa nyimbo za Taifa la Tanzania na Ireland. Lakini tunaomba Waheshimiwa Wabunge mbaki humu ndani ukiacha Wenyeviti wa Kamati ya *Steering Committee* na Tume ya Huduma za Bunge, Makamishna hawa ndiyo watakuwa kwa niaba yetu pale nje kuweza kumlaki mgeni pamoja na sisi, Spika na Naibu Spika. Haitachukuwa muda wataingia Marais, yaani Rais mgeni na Rais wetu. Maandalizi ya Viti maalum yatakuwa tayari pamoja na bendera za Rais wetu na Rais wa Ireland.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Rais wa Ireland itakuwa ni dakika 35 na kwa hiyo, shughuli zetu ukichanganya mambo yote zitaisha saa 06:45 na itakapofika hapo sasa itanibidi nisitishe Shughuli za Bunge hadi saa 11:00 jioni. Huo ndio mpangilio na ninatumaini mambo yote yatakwenda vizuri.

Taarifa ya pili ni kwamba, kwa masikitiko tena, natoa taarifa ya wenzetu watu wa habari gazeti la Mwananchi la leo limedai katika ukurasa wa tatu kwamba Bunge limepoteza Shilingi bilioni 35. Ukweli na *Hansard* ninayo hapa ya Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir alipochangia hapo jana. Mheshimiwa alisema hivi: “Ofisi ya Spika

ukiwemo na wewe mwenyewe mnadaiwa Shilingi milioni 170 ikiwa ni masurufu, yaani *imprest* ambayo haikufika kwa Mkaguzi Mkuu kwa wakati, hivyo usishangae Mheshimiwa Spika ndiyo uhalisi ulivyo."

Fikirieni, hii inageuzwa kwa sababu tunaanza kuona labda baadhi ya watu hawa wana nia mbaya tu. Unawezaje kutokana na hili lililosemwa na Mheshimiwa Mbunge ukasema Bunge lenyewe sasa? Yaani Kasma ya Bunge imepoteza bilioni 35, ni sawasawa na Bajeti nzima ya Bunge kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuwaasa wenzetu Waandishi wa Habari na kwa Bunge, nadhani tulikuwa tu rahimu sana chini ya Sheria kulisingizia Bunge mambo ya hovyo hovyo ama kulidhalilisha *Parliamentary Powers and Privileges Acts* ni kosa la jinai. Tumeona tu ni mapema lakini leo nalazimika kutoa onyo hili kwa sababu sasa imeanza kuwa ni mchezo.

Juzi nadhani kuna gazeti, ni hilohilo la Mwananchi lilisema kwamba kuna Wabunge 10 wanahojiwa na Polisi kwa kughushi vyeti na kwamba walikuwa wanapelekwa Ofisi za *CID* kwa magari yaliyo *tinted glass* ili wakahojiwe. Waheshimiwa Wabunge hakuna kitu cha namna hiyo. Unashangaa huu uandishi ambao unalenga tu kudhalilisha Taasisi ya nchi!

Nadhani kuna Mheshimiwa mmoja leo amezungumzia juu ya uzalendo, nadhani ni Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, sijui wenzetu hawa wanapata raha ipi katika uandishi unaosingizia na kudhalilisha Taasisi kama hii.

Ndugu waandishi, inawezekana mtu mmoja au mwingine, Mbunge mmoja au mwingine yule anakukera, lakini Bunge ni Taasisi, siyo uwe unamlenga Mbunge mmoja na kwa kufanya hivyo ukadhalilisha Bunge zima.

Namwomba Katibu wa Bunge kuanzia sasa, tafadhali sana sheria ichukue mkondo wake kwa hawa ambao wameng'ang'ania kulisema Bunge kwa namna ambayo inadhalilisha nchi, tena kwa kukusudia kabisa na kwa taarifa za uongo kabisa za kubuni, itabidi nchi ichukue hatua. Bunge siyo chombo kidogo tu cha kuchezewachezewa halafu basi tu, mtu ajisikie vizuri, haiwezekani! Nchi inaendeshwa kwa Katiba na Sheria.

Baada ya maneno hayo, na kwa kuwa muda wa Bunge haujafikia mwisho wake namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi atoe hoja ili tuweze Kuahirisha Bunge kabla ya wakati wake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe dakika tatu kabla ya muda wake wa kuahirisha Bunge, kwa sababu nafasi hii haiwezi kumtosha mchangiaji kuchangia. Naomba kutoa hoja ili Bunge liahirishwe sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 01:45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 22 Juni, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*